# KATIBA YA CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CHADEMA) YA MWAKA 2006

## Toleo la 2019

**Toleo hili la Katiba ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ya mwaka 2006 limezingatia na kuweka pamoja marekebisho yaliyofanywa katika Katiba hii tangu ilipotungwa mwaka 2006 hadi tarehe 18 Desemba 2019.**

# YALIYOMO

**uk**

**1. UTANGULIZI** ........................................ **ix**
**2. FASILI NA UFAFANUZI** ........................................ **xi**

**3. SURA YA KWANZA**
JINA ........................................ 1

**4. SURA YA PILI**
KATIBA, KANUNI, MAADILI NA ITIFAKI ........................................ 2

**5. SURA YA TATU**
FALSAFA NA ITIKADI ........................................ 4

**6. SURA YA NNE**
MADHUMUNI YA CHAMA ........................................ 8

**7. SURA YA TANO**
UANACHAMA ........................................ 13

**8. SURA YA SITA**
MUUNDO, VIKAO NA UONGOZI WA CHAMA ........................................ 17

**9. SURA YA SABA**
NGAZI ZA UONGOZI ........................................ 27

**10. SURA YA NANE**
MAPATO, MALI NA WADHAMINI WA CHAMA ........................................ 75

**11. SURA YA TISA**
MAMBO YA JUMLA KUHUSU KATIBA NA CHAMA ........................................ 77

**KANUNI ZA CHAMA**

**UTANGULIZI** .................................................. **83**
**FASILI NA UFAFANUZI**.................................................. **84**

**12. SURA YA KWANZA**
Jina, Nembo, Bendera na Makao Makuu ya Chama .................................................. 86

**13. SURA YA PILI**
Katiba, Kanuni na Maadili.................................................. 89

**14. SURA YA TATU**
Itikadi na Falsafa ya Chama.................................................. 90

**15. SURA YA NNE**
Madhumuni ya Chama. .................................................. 91

**17. SURA YA TANO**
Uanachama .................................................. 93

**18. SURA YA SITA**
Muundo, Vikao na Uongozi wa Chama. .................................................. 97

**19. SURA YA SABA**
Majukumu ya Vikao na Uongozi wa Ngazi za Chama. .................................................. 101

**20. SURA YA NANE**
Mapato, Mali na Wadhamini wa Chama.................................................. 122

**21. SURA YA TISA**
Mambo ya Jumla Kuhusu Katiba na Chama. .................................................. 124

**22. SURA YA KUMI**
Maadili ya Viongozi, Sifa Mahususi za Viongozi na Maadili ya Wanachama .................................................. 126

**23. SURA YA KUMI NA MOJA**
MAMLAKA YA MAKAO MAKUU KUTOA MIONGOZO ..................... 131

**24. SURA YA KUMI NA MBILI**
ITIFAKI NDANI YA CHAMA.............................................................. 132

**25. MIONGOZO MBALIMBALI ............................................................. 140**

**26. MWONGOZO WA MABARAZA YA CHAMA.................................. 191**

**MWONGOZO WA BARAZA LA WANAWAKE**
UTANGULIZI............................................................................ 195
FASILI YA UFAFANUZI ............................................................. 195
**1. SURA YA KWANZA**
JINA............................................................................................ 197
**2. SURA YA PILI**
UANACHAMA.............................................................................. 199
**3. SURA YA TATU**
MUUNDO, VIKAO NA UONGOZI WA BARAZA............................... 202
**4. SURA YA NNE**
NGAZI, UONGOZI NA MAJUKUMU YA VIKAO ............................... 205
**5. SURA YA TANO**
MAJUKUMU YA VIONGOZI ......................................................... 225

**MWONGOZO WA BARAZA LA WANAWAKE**
UTANGULIZI............................................................................ 228
FASILI YA UFAFANUZI ............................................................. 228
**1. SURA YA KWANZA**
JINA............................................................................................ 229
**2. SURA YA PILI**
MAADILI NA ITIFAKI.................................................................. 229

**3. SURA YA TATU**
LENGO KUU LA BARAZA......230
**4. SURA YA NNE**
Uanachama......232
**5. SURA YA TANO**
Muundo......233
**6. SURA YA SITA**
VIKAO NA UONGOZI WA BARAZA......234
**7. SURA YA SABA**
NGAZI, UONGOZI NA MAJUKUMU YA VIKAO......239
**8. SURA YA NANE**
MAPATO YA BARAZA......261
**9. SURA YA TISA**
MAMBO YA JUMLA KUHUSU......262
**10. SURA YA KUMI**
NAMNA YA KUMPATA MBUNGE/MWAKILISHI
NA DIWANI WA VITI MAALUM......263

## MWONGOZO WA BARAZA LA VIJANA

UTANGULIZI......266
**1. SURA YA KWANZA**
JINA......267
**2. SURA YA PILI**
MISINGI, MAADILI, ITIFAKI NA KAULIMBIU......268
**3. SURA YA TATU**
LENGO KUU LA BARAZA......269
**4. SURA YA NNE**
UANACHAMA......271
**5. SURA YA TANO**
MUUNDO NA MAJUKUMU YA VIONGOZI......275

**6. SURA YA SITA**
NGAZI, VIONGOZI VIKAO NA MAJUKUMU YA
VIKAO ........................................................................................ 283
**7. SURA YA SABA**
MAPATO NA MATUMIZI YA BARAZA ................................................ 303
**8. SURA YA NANE**
MAMBO YA JUMLA KUHUSU MWONGOZO HUU ........................... 304

# UTANGULIZI

**KWA KUWA**

Nchi yetu imeridhia mfumo wa utawala wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kupitia sheria iliyopitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hivyo kutambulika rasmi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyorekebishwa mwaka 1992, Sehemu ya Kwanza, Ibara ya Tatu, Ibara ndogo ya Kwanza na ya Pili;

**NA KWA KUWA**

Sisi wajumbe wa Mkutano Mkuu tukiwakilisha wanachama wa Chama chetu cha siasa kinachoitwa "CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CHADEMA)", kama sehemu ya Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kuona umuhimu wa kukuza demokrasia ya kijamii bila kubagua kwa misingi ya rangi, ukabila, ukanda, jinsia, itikadi, umri au dini;

**NA KWA KUWA,**

Tumetambua athari ambazo nchi yetu imekumbana nazo kutokanana mfumo wa Ki-imla uliotokana na Chama kimoja cha siasa na kusababisha kukosekana kwa uhuru na usawa wa mawazo sambamba na kukandamizwa kwa haki za msingi za kijamii na za kibinadamu kwa mujibu wa Tamko la Dunia la Haki za Binadamu na kusababisha kudorora kwa uchumi pamoja na huduma zote za jamii;

**NA KWA KUWA,**

Uzoefu wa miaka kumi na nne ya mfumo wa utawala wa vyama vingi na nia ya kweli ya kuleta demokrasia kutoka kwa walio na madaraka;NA

**KWA KUWA**

Tunatambua na kuamini kuwa Falsafa ya **“Nguvu na Mamlaka ya Umma”** ndiyo njia itakayoleta jamii HURU na yenye AMANI YA KWELI;

**HIVYO BASI**,

Sisi wajumbe wa Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 13/8/2006, Mjini Dar es Salaam tumeamua kuifanyia mabadiliko Katiba ya 2004 ya Chama chetu cha Siasa kinachoitwa CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO ili kuipa sura inayoendana na mtazamo na msukumo mpya wa FALSAFA yetu ya NGUVU NA MAMLAKA YA UMMA na Dira na Dhamira ya Chama kuanzia 2006 na kuendelea. Kuanzia sasa CHADEMA, kitaendeshwa kwa mujibu wa Katiba hii.

Sambamba na Kanuni, Taratibu na Maadili ya Chama vitavyotungwa kwa mujibu wa Katiba hii, ili kuimarisha kutetea, kudumisha, na kuendeleza DEMOKRASIA ya kweli, na HATIMAYE kuweza kuleta MAENDELEO ya kweli ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa jamii nzima ya Taifa la Tanzania.

# FASILI NA UFAFANUZI

Katika Katiba hii maneno yafuatayo yatakuwa na maana inayoelezwa hapa chini kwa kila neno.

| | | |
|---|---|---|
| **BARAZA KUU** | – | Ni chombo cha ngazi ya Taifa cha Utendaji cha Mkutano Mkuu wa Taifa. |
| **BODI YA WADHAMINI** | – | Ni chombo kinachoundwa na Chama kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kusimamia mali za Chama. |
| **FALSAFA YA CHAMA** | – | Ina maana ya imani na mtizamo wa chama kama ilivyoainishwa kwenye Katiba. |
| **HAMASA** | – | Ni uhamasishaji wa wanachama kwa njia ya vikundi vya kushirikiana kiuchumi, kijamii na au kiutamaduni |
| **ITIKADI** | – | Ina maana ya mwelekeo wa chama kisiasa, kiuchumi na kijamii. |
| **JIMBO** | – | Ni Jimbo la chaguzi za kiserikali kwa mujibu wa sheria za nchi. |
| **KANDA** | – | Ina maana ya muunganiko wa Mikoa kuunda ngazi ya Chama kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu. |
| **KAMATI KUU** | – | Ni cha cha utendaji cha Baraza Kuu. |

| | | |
|---|---|---|
| **KANUNI** | – | Ni taratibu za uendeshaji chama kwa msingi wa Katiba ya chama. |
| **KATIBU MKUU** | – | Ni Mendaji Mkuu wa Chama. |
| **KURUGENZI** | – | Ina maana ya muundo wa utendaji wa Makao Makuu unaoundwa na Kamati Kuu kwa kuzingatia mahitaji ya Chama. |
| **MABARAZA** | – | Ina maana ya muundo wa makundi yajamii kiumri na kijinsia ndani ya Chama. |
| **MKUTANO MKUU** | – | Ina maana ya chombo cha juu kuliko vyote kwenye ngazi husika ndani ya Chama. |
| **MWENYEKITI** | – | Ni kiongozi mkuu wa chama ngazihusika ndani ya Chama. |
| **SEKRETARIAT** | – | Ni chombo cha utendaji wa shughuli zakila siku kwa ngazi husika. |
| **TEHAMA** | – | Ni teknolojia ya habari na mawasiliano. |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 JINA

Jina na Makao Makuu

**1.1 Jina la Chama litakuwa**
CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CHADEMA)

**1.2 MAKAO MAKUU YA CHAMA**
Makao Makuu ya Chama yatakuwa Dar es Salaam na patakuwa na Ofisi ya Makao Makuu ya Zanzibar

# SURA YA PILI

## 2.0 KATIBA, KANUNI, MAADILI NA ITIFAKI

Katiba ya Chama

### 2.1 KATIBA

Katiba ya Chama ndiyo itakayokuwa sheria mama ya Chama na dira ya uendeshaji wa shughuli za Chama kulingana na muundo wa ngazi mbalimbali za uongozi na utendaji. Katiba hii ndiyo pia itaongoza uundwaji na uendeshaji wa shughuli za Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee pamoja na wanachama wa CHADEMA.

### 2.2 KANUNI

Kanuni za Chama ndizo zitafafanua na kuainisha utaratibu wa utekelezaji na uendeshaji wa shughuli za Chama kwa wanachama, viongozi na watendaji katika ngazi mbalimbali za muundo wa Chama. Miongozo ya Mabaraza ya Vijana, Wanawake, Wazee na miongozo mingine itahesabiwa kama sehemu ya Kanuni za Chama.

### 2.3 MAADILI

Maadili ya Chama ndiyo yatakayoainisha sifa, nidhamu, utii, uwajibikaji na dhamira ya wanachama, watendaji na viongozi wa Chama katika ngazi zote. Maadili haya yanajumuisha uongozi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee.

## 2.4 ITIFAKI

CHADEMA kama Chama kinachokua na kupanuka kwa kasi kitaifa na chenye nia ya kuchukua dola wakati wowote hakina budi kujiwekea taratibu mbalimbali ambazo zitakisaidia Chama kuendesha shughuli zake za Chama katika mtiririko wa aina fulani bila kuonyesha utofauti kati ya viongozi na ngazi mbalimbali za Chama. Nia ya kuweka taratibu hizi ni kuleta umoja na mshikamano ndani ya Chama na kukitambulisha CHADEMA kama Chama kimoja. Kwa hiyo itifaki ya Chama inajumuisha pia uongozi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee ambayo ni sehemu tu ya muundo na uongozi wa chama.

# SURA YA TATU

## 3. 0 FALSAFA NA ITIKADI

Falsafa na Itikadi ya Chama

### 3.1 Falsafa ya Chama

3.1.1 Falsafa ya Chama ni kuamini katika "Nguvu na Mamlaka ya Umma" (The People's Power) katika kumiliki, kuendesha, kubuni, na kuendeleza maamuzi, mawazo, rasilimali, uchumi na siasa ya nchi yao.

3.1.2 Aidha falsafa ya "Nguvu na Mamlaka ya Umma" ndiyo msingi na chimbuko la kuundwa dola ya nchi, na kuwa Umma ndio wenye madaraka ya mwanzo na ya mwisho katika kuamua hatima ya nchi na Taifa pasipo kuingiliwa, kudanganywa au kughilibiwa na viongozi, watawala au wageni.

3.1.3 Ujenzi na udumishaji wa Demokrasia na Maendeleo nchini vitatokana na Nguvu na Mamlaka ya Umma wa Watanzania. Nguvu na Mamlaka ya Umma itabainishwa, kuainishwa na kulindwa katika Katiba ya nchi na Umma ndiyo utakuwa chimbuko la Katiba hiyo.

3.1.4 Historia inaonyesha kuwa "Umma" wa Watanzania haujawahi kuwa na sauti, mamlaka na madaraka juu ya maamuzi

ya hatima ya maisha ya watu. Uhuru, nguvu, mamlaka na madaraka wakati wote, tokeaenzi za ukoloni mpaka leo, vimekuwa vikihodhiwa na kumilikiwa na watu wachache ambao wana mamlaka ya kuongoza Serikali na kuwakandamiza wananchi.

3.1.5 CHADEMA inaamini kuwa mifumo na miundo ya utawala wa nchi yetu haupo kwa ajili ya kuutumikia umma, bali umma ndiyo huzitumikia serikali hizo ambazo ni mali ya watu wachache wanaopoka "Nguvu ya Umma". Sambamba na hilo, umma wa Watanzania umekuwa hauna mamlaka ya mwisho ya kuhoji maamuzi ya serikali yanayowaathiri watu, na hivyo kujikuta hauna mamlaka juu ya rasilimali, sheria, utawala, na uendeshaji wa nchi. Aidha, Katiba ya Nchi imekuwa miliki ya Serikali kwa kutumia Bunge ambalo linatawaliwa na mawazo kongwe ya ukiritimba wa enzi za mfumo wa Chama kimoja cha siasa nchini.

3.1.6 CHADEMA inaamini na kutambua kuwa "kuchaguliwa" kuunda utawala wa kuongoza nchi hakumaanishi wachaguliwa kujitwalia mamlaka ya UMMA na kisha kuyatumia mamlaka hayo kuwakandamiza "waliowachagua" kwa sababu tu ya kutetea maslahi binafsi badala ya maslahi ya umma.

3.1.7 Falsafa ya "Nguvu na Mamlaka ya Umma" inalenga kuwaamsha, kuwahamasisha, kuwaelimisha, kuwa shawishi na kuwaandaa watanzania wachukue hatua

ya kuimiliki, kuitawala, kuilinda na kuifaidi nchi yao tofauti na kipindi cha miaka mingi chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa na miaka kumi na nne ya mwanzo ya mfumo wa vyama vingi.

3.1.8 Hivyo basi, falsafa ya "Nguvu na Mamlaka ya Umma" uongozi unaoweza kumilikiwa, kuhojiwa, na kuwajibishwa na umma kwa kutumia vyombo vilivyopatikana kwa utashi wa wengi kupitia chaguzi huru na za haki.

**3.2 Itikadi ya Chama**

3.2.1 CHADEMA ni Chama cha itikadi ya MRENGO WA KATI (Center Party).

3.2.2 CHADEMA ni Chama kinachoamini kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi kwa kutumia rasilimali za nchi yetu bila kuathiri uhuru wa Taifa, na kuhakikisha kuwa umma kwa ujumla unanufaika na rasilimali zao.

3.2.3 CHADEMA inaamini katika kujenga na kuimarisha uchumi wa soko jamii (social market economy), utakaoheshimu na kulinda haki na mali za watu, biashara huru na sekta ya watu binafsi bila kupoka mamlaka ya umma katika maeneo nyeti hususani pale penye hitilafu ya soko au penye maeneo nyeti ya kiuchumi. Tunaamini katika soko huru si katika soko holela.

3.2.4 CHADEMA inaamini katika kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali asilia za nchi ili zichangie kikamilifu katika pato la Taifa na hasa kuboresha huduma za kiuchumi

zinazotumiwa na wananchi wote.

3.2.5 CHADEMA inaamini katika uzalendo na kuthamini mila na desturi zetu zilizo nzuri.

3.2.6 CHADEMA inaamini katika uhuru chini ya sheria zilizo za haki.

3.2.7 CHADEMA inaamini katika siasa ambazo ziko juu ya vyama zenye kusimamia zaidi maslahi ya Taifa.

3.2.8 CHADEMA inaweka umuhimu wa pekee katika familia kama moja ya taasisi muhimu ya kijamii.

3.2.9 CHADEMA inaamini katika umuhimu wa uhuru wa kuamini katika kujenga maadili ya mwanajamii mmoja mmoja bila kuifanya dini kuwa sehemu ya dola.

3.2.10 CHADEMA inaamini Taifa linaundwa na watu, hivyo uhai wake unawategemea watu, na mabadiliko yake yanatokana na watu.

3.2.11 CHADEMA inaamini katika kujenga uwezo wa wazawa katika kumiliki na kuendesha uchumi.

3.2.12 CHADEMA inaamini kumiliki rasilimali na mali miongoni mwa wananchi kunawapa uhuru zaidi hivyo tunataka kujenga Chama na baadaye Taifa lenye kutoa fursa, ambapo kila mtu bila kujali asili na hali yake anaweza kutimiza na kufanikiwa kadiri ya vipaji vyake.

# SURA YA NNE

## 4.0 MADHUMUNI YA CHAMA

Madhumuni

### 4.1 Madhumuni ya Kisiasa

4.1.1 Kuhakikisha kuwa Chama chetu kinashinda chaguzi za Kiserikali na kushika dola kwa njia ya kidemokrasia ili kuleta maendeleo endelevu kwa Taifa.

4.1.2 Kukuza, kulinda, kuelimisha na kutetea haki za binadamu katika misingi ya Tangazo la Ulimwengu la Haki za Binadamu na mikataba yote ya kimataifa inayolinda haki hizo na inayofutilia mbali ukandamizaji wa watu katika misingi ya rangi, jinsia, ukanda, umri au itikadi.

4.1.3 Kuhakikisha kila mtu ana haki na uhuru wa kuabudu kwa minajili ya dini, madhehebu au imani yoyote anayotaka, bila kuathiri amani na/au utulivu wa mwenzake na jamii.

4.1.4 Kuendeleza na kudumisha Demokrasia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, kujenga utamaduni wa demokrasia katika jamii kwa kutambua haki za wengi katika maamuzi na pia kutambua haki za wachache sikilizwa, kuheshimiwa na

kulindwa, sambamba nakukubali ushindani huru, wa haki na wa wazi katika uchaguzi.

4.1.5 Kuhakikisha mtu ana uhuru wa kwenda mahali popote ndani ya mipaka ya nchi na kwamba anaweza kushirikiana na mtu yeyote ndani na nje ya nchi katika kuendeleza maslahi halali ya washirika na kuwa kuna uhuru wa kukutana na kuandamana kwa amani ili kuendeleza hayo maslahi kwa masharti ya sheria za haki.

4.1.6 Kudumisha uhusiano wa kirafiki na mataifa jirani, Afrika na duniani kote; kuyaheshimu maamuzi yote ya kimataifa kulingana na kanuni zilizopo za kimataifa na mikataba ya Umoja wa Mataifa na ya nchi yetu na nchi zingine kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

4.1.7 Kukuza na kuendeleza uraia mwema, uzalendo na mapenzi ya nchi yetu.

4.1.8 Kuhakikisha kwamba Chama kinatumia TEHAMA kuhamasisha umma kukiunga mkono.

## 4.2 Madhumuni ya Kiuchumi

4.2.1 Kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi kwa kutumia rasilimali za nchi yetu bila kuathiri uhuru wa Taifa, na kuhakikisha kuwa umma kwa ujumla unanufaika na rasilmali zao.

4.2.2 Kujenga na kuimarisha uchumi wa soko huru, utakaoheshimu na kulinda haki na mali za watu, biashara huru na sekta binafsi bila kupoka mamlaka ya umma katika maeneo nyeti.4.2.3 Kujenga na kuimarisha kilimo, hususani cha umwagiliaji, na ufugaji katika lengo la kutosheleza Taifa kwa chakula na kwa ajili ya masoko ya biashara ya ndani na ya nje ili kuboresha maisha ya wakulima na wafugaj na kuendeleza sera ya kulinda ardhi, maliasili na mazingira kwa manufaa ya kilimo na ufugaji endelevu.

4.2.4 Kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali asilia za nchi ili zichangie kikamilifu katika pato la Taifa na hasa katika kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii zinazotumiwa na wananchi wote.

4.2.5 Kujenga misingi imara ya ajira kwa kuongeza fursa na uwezo wa wananchi kujiajiri wenyewe.

4.2.6 Kujenga mazingira ya kupanuka kwa sekta binafsi na kuhakikisha kipato cha waajiriwa katika sekta rasmi za uchumi na huduma kinalingana na jasho au juhudi za mwajiriwa.

4.2.7 Kutoa mkazo katika utafiti, sayansi na teknolojia na kusambaza matokea yake kwa walengwa ili kuchochea maendeleo endelevu.

4.2.8 Kutengeneza sera makini zitakazowezesha kukuza maendeleo ya viwanda vya aina zote hasa vinavyotumia malighafi inayopatikana nchini kwa lengo la uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi ya ndani na biashara ya nje.4.2.9 Kuimarisha miundombinu muhimu ya sekta ya usafiri na mawasiliano hususani barabara, reli, bandari, anga na simu, mabwawa, mifereji ya maji na umeme.

4.2.10 Kulipa kipaumbele suala la hifadhi na ulinzi wa mazingira katika mipango yote ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

4.2.11 Kuongeza mapato ya Chama kwa njia ya TEHAMA"

**4.3 Madhumuni ya Kijamii**

4.3.1 Kuendeleza juhudi za kuhakikisha haki za wanawake, watoto na mila potofu za ukandamizaji wa kijinsia, kuwanyima watoto haki za malezi bora na za kupata elimu ya kutosha, umuhimu wa kuwajali wenye ulemavu na kuwatimizia mahitaji yote ya msingi, pamoja na kutekeleza makubaliano na mikataba ya kimataifa kuhusu haki za watoto, wanawake na walemavu.

4.3.2 Kuboresha, kutunza na kutoa huduma za jamii, kwa mfano Afya, Elimu, Maji, Makazi na Usalama wa Raia, kwa ajili ya kukuza hali ya maisha ya watu.

4.3.3 Kuhifadhi na kuboresha utamaduni wa Taifa ili kujenga hadhi na heshima ya watanzania na kuendeleza nyanja zote za utamaduni, burudani, michezo, sanaa na historia ya nchi.4.3.4 Kutoa huduma za kukidhi maisha kwa wastaafu na makundi yasiyojiweza katika jamii hususan wenye ulemavu, watoto yatima na wazee, ambao hawapo katika mkondo wa kujipatia kipato cha kujitosheleza.

4.3.5 Kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na janga la VVU / UKIMWI (HIV/AIDS) sambamba na kutoa huduma muafaka kwa waathirika.

4.3.6 Kuhakikisha taarifa mbalimbali za Chama zinawafikia wananchi na wanachama kwa wakati kwa njia za TEHAMA."

# SURA YA TANO

## 5.0 UANACHAMA

Sifa, Haki na Wajibu wa Mwana chama

### 5.1 Sifa za kuwa Mwanachama

5.1.1 Awe raia wa Tanzania.

5.1.2 Awe na umri wa miaka 18 au zaidi

5.1.3 Awe na akili timamu

5.1.4 Awe anakubaliana na Katiba, Sera, Kanuni na Maadili ya Chama.

5.1.5 Awe anakubaliana na Itikadi na Falsafa ya Chama.

5.1.6 Asiwe mwanachama wa Chama kingine cha siasa baada ya kujiunga na CHADEMA.

5.1.7 Kuwa mwanachama wa CHADEMA itakuwa ndio sifa ya msingi ya kujiunga na Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee.

### 5.2 Haki za Mwanachama

Kila Mwanachana atakuwa na haki kama ifuatavyo;

5.2.1 Kuchagua viongozi wa Chama wa ngazi anayohusika kwa mujibu wa Katiba.

5.2.2 Kuchaguliwa kuongoza na kuwakilisha Chama katika ngazi yoyote kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa ya sifa za uongozi.

5.2.3 Kushiriki vikao vya Chama vinavyomhusu na kutoa mawazo yake kwa uhuru kwa kuzingatia taratibu za vikao.

5.2.4 Kujitetea, kusikilizwa na kukata rufaa anaposhitakiwa ama kuchukuliwa hatua za kinidhamu kichama.

**5.3 Wajibu wa Mwanachama**

5.3.1 Kushiriki kikamilifu katika vikao vinavyomhusu na katika shughuli zingine za Chama kadri atakavyotakiwa

5.3.2 Kuchangia gharama za uendeshaji Chama kwa njia ya ada ya uanachama ya kila mwaka na kwa michango mingine inayoamriwa na vikao vya Chama.

5.3.3 Kutetea na kueneza Itikadi, Falsafa na Madhumuni ya Chama ndani ya jamii anamoishi.

5.3.4 Kushirikiana na wanachama na viongozi wengine wote katika kutekeleza sera na mipango ya Chama.

5.3.5 Kuwa tayari kupambana na namna yoyote ya uonevu, ukandamizaji, udhalilishaji na ubaguzi.

## 5.4 Kukoma kwa Uanachama

5.4.1 Kwa kujiuzulu mwenyewe kwa hiari yake.

5.4.2 Kutokana na kufariki.

5.4.3 Kuachishwa ama kufukuzwa na tawi lake ama ngazi nyingine ya Chama, kwa mujibu wa Katiba kwa kukosa sifa za kuendelea kuwa mwanachama ama kuwa na mwenendo usioendana na Itikadi, Falsafa, Madhumuni, Kanuni, Maadili na Sera za Chama. Mwanachama atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa ngazi ya juu kama hakuridhika na adhabu hiyo.

5.4.4 Bila kuathiri kifungu 5.4.3 cha Katiba, Kamati Kuu inaweza kumwachisha ama kumfukuza mwanachama yeyote kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

5.4.5 Kukosa sifa za uanachama.

5.4.6 Kufukuzwa uanachama wa Baraza la Vijana au Wanawake au Wazee kwa utovu wa nidhamu.

5.4.7 Taarifa ya mwanachama aliyefukuzwa na Baraza ngazi husika itawasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Utendaji cha ngazi hiyo na Kamati Kuu kwa ngazi ya Taifa.

5.5 Ada na Kiingilio cha Uanachama

5.5.1 Kutakuwa na kiingilio kwa kila mwanachama mpya

5.5.2 Kutakuwa na ada ya mwaka ya uanachama.

5.5.3 Mwanachama atalazimika kulipia kiingilio na ada ya uanachama kwa njia ya kielekitroniki au njia nyingine yeyote itakayowekwa kwa mujibu wa Kanuni za Chama."

# SURA YA SITA

## 6.0 MUUNDO, VIKAO, UONGOZI NA MAWASILIANO NDANI YA CHAMA

Muundo wa Uongozi na Vikao vya Chama

### 6.1 Muundo wa Chama;

6.1.1 Kutakuwa na ngazi saba za uongozi kwenye muundo wa Chama kama ifuatavyo:

(a) Ngazi ya Msingi

(b) Tawi

(c) Kata/Wadi

(d) Jimbo/Wilaya

(e) Mkoa

(f) Kanda

(g) Taifa

6.1.2 Uundaji wa ngazi moja ya juu utafanyika tu baada ya kuwa na muundo na uongozi katika ngazi ya chini kwa angalau 50% ya maeneo ya kiutawala yanayostahili kuwa na muundo na uongozi wa kikatiba wa Chama kwa ngazi hiyo.

6.1.3 Kwa kuzingatia Ibara 6.1.2 ya Katiba hii, ngazi ya juu ya chama itateua kamati ya muda itakayokuwa na wajibu wa kuratibu shughuli za chama na kuwaunganisha wanachama

katika uwezo wa kuwa na uongozi wa kikatiba.6.1.4 Kutakuwa na muundo wa Chama nje ya nchi kwa mujibu wa Kanuni zitakazotungwa na Baraza Kuu.

6.1.5 Kutakuwa na Kamati ya Hamasa katika kila ngazi ya Chama kwa mujibu wa kanuni zitakazotungwa na Baraza Kuu."

**6.2 Vikao na Uongozi wa Chama**

6.2.1 Kutakuwa na vikao vya aina nne;

(a) Vikao vikuu vya maamuzi ya kisera. Hii ni Mikutano Mikuu ya kila ngazi ya muundo wa Chama

(b) Vikao vya uongozi vinavyosimamia utekelezaji wa maamuzi ya kisera ya vikao vikuu. Kamati za Utendaji za ngazi husika na Kamati Kuu na Baraza Kuu ngazi ya Taifa, pamoja na vikao vya Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee wa Chama.

(c) Vikao vya utendaji wa shughuli za kila siku za Chama na utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya vikao vya uongozi. Hizi ni Sekretariat na vikao vya uongozi na Kamati za Utendaji za Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee wa Chama.

(d) Vikao vya mashauriano na uratibu katika ngazi za Mkoa na Wilaya.

6.2.2 Uhalali wa Vikao kwa ngazi zote;

(a) Kutahitajika akidi ya asilimia hamsini (50%) ya wajumbe kwenye kikao halali cha ngazi za kawaida.

(b) Lakini vikao halali vya kurekebisha au kubadilisha Katiba au vya uchaguzi na sera za Chama vitahitaji akidi ya asilimia sabini na tano (75%).

(c) Kamati ya Utendaji/Kamati Kuu inaweza kuitisha vikao halali vya Chama kwa kupunguza idadi ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria kufuatana na uwezo wa Chama kifedha ili mradi pawepo uwiano wa wawakilishi toka kila ngazi au kundi linalowakilishwa na kwa ujumla waalikwa wasiopungua 50% ya wajumbe wote wa kikatiba.

(d) Bila kuathiri aya ya (a) katika ibara hii, kikao ambacho kitaitishwa kwa mujibu wa aya (c), akidi itakuwa asilimia 75% ya wajumbe watakaoitishwa.

(e) Vikao vya Sekretariati na vya utendaji vya ngazi ya Taifa na Kanda vinaweza kufanyika kwa njia ya Tehama"

(f) Baraza Kuu litatunga mwongozo kuhusu matumizi ya TEHAMA kwenye uendeshaji vikao katika ngazi zote za Chama.

6.2.3 Kutakuwa na Viongozi wa aina nne;

(a) Viongozi wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu katika kila ngazi.(b) Viongozi wa kuchaguliwa / kuteuliwa na vikao vya uongozi yaani Kamati za Utendaji, Kamati Kuu ama Baraza Kuu

(c) Watendaji waajiriwa / watumishi

(d) Viongozi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee wa CHADEMA watakaochaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa Miongozo ya Mabaraza yenyewe.

**6.3 Uchaguzi wa Viongozi na Muda wa Uongozi**

6.3.1 Utaratibu wa Uchaguzi;

(a) Uchaguzi wa viongozi utazingatia taratibu na sifa za uongozi kama zilivyofafanuliwa katika Kanuni za Chama.

(b) Maombi ya uongozi yatafanywa kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum zilizoidhinishwa na Baraza Kuu la Chama.

(c) Majina ya wagombea wote wenye sifa zinazotakiwa yatapigiwa kura ya siri na kikao kinachohusika na mshindi atapatikana kwa uwingi wa kura zisizopungua 50% ya wapiga kura halali waliohudhuria kikao cha uchaguzi. Maombi ya uongozi

yanaweza kufanywa kwa njia ya mtandao.

(d) Uchaguzi wa viongozi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee utafanyika kwa kuzingatia masharti ya Ibara hii ya Katiba.

(e) Ikiwa katika chaguzi za Chama kura za wagombea zitalingana, Mwenyekiti wa uchaguzi atakuwa na kura ya turufu.

### 6.3.2 Muda wa Uongozi;

(a) Kila uongozi uliochaguliwa au kuteuliwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Chama utashika wadhifa wake kwa kipindi cha miaka mitano.

(b) Kiongozi aliyechaguliwa au kuteuliwa baada ya Uchaguzi Mkuu atashika wadhifa wake hadi kipindi cha Uchaguzi Mkuu kinachofuata.

(c) Kiongozi aliyemaliza muda wa uongozi ana haki ya kugombea na kuchaguliwa tena mradi awe anatimiza masharti ya kuchaguliwa kuwa kiongozi.

(d) Muda wa uongozi unaweza kufupishwa kama mamlaka iliyochagua au kuteua itaamua hivyo.

(e) Ibara hii itahusu pia viongozi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee wa CHADEMA.

6.3.3 Kurekebisha tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Chama;

(a) Tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Chama inaweza kurekebishwa kwa kusogezwa mbele kwa muda usiozidi mwaka mmoja toka mwisho wa uhalali wa uongozi uliopo. Mamlaka ya kufanya marekebisho haya yameachwa kwa Kamati Kuu.

(b) Kamati Kuu itapanga tarehe ya uchaguzi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee.

6.3.4 Kukoma kwa Uongozi

(a) Kwa kiongozi kujiuzulu kwa hiari yake

(b) Kwa kiongozi kuachishwa uongozi au kufukuzwa uanachama

(c) Kwa kiongozi kushindwa kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Kanuni au Maadili ya Chama.

(d) Kwa kufariki

(e) Ibara hii inahusu pia uongozi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee ya Chama.

6.3.5 Kuziba nafasi wazi za Uongozi

(a) Kamati ya Utendaji ya kila ngazi au Baraza Kuu itaziba kwa muda nafasi yoyote ya kiongozi aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa ngazi husika.

(b) Nafasi wazi za uongozi walioteuliwa zitazibwa na vikao husika kwa kufanya

uteuzi mpya katika muda usiozidi miezi mitatu tangu nafasi kuwa wazi.

(c) Muda wa uongozi kwa mujibu wa kifungu 6.3.5 (b) hautazidi mwaka mmoja.

(d) Bila kujali sharti la kifungu 6.3.5 (c) hakutafanyika uchaguzi rasmi wa kuziba nafasi kama kumebakia miezi sita tu au chini ya hapo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa kawaida wa Chama unaofuata kufanyika.

6.3.6 Mamlaka ya Nidhamu

(a) Kiongozi aliyechaguliwa na Mkutano

Mkuu; mamlaka yake ya nidhamu

itakuwa kama ifuatavyo::-

(i) Kiongozi ngazi ya msingi; mamlaka yake ya nidhamu itakuwa ni kamati tendaji ya tawi.

(ii) Kiongozi ngazi ya tawi; mamlaka yake ya nidhamu itakuwa ni Kamati Tendaji ya Kata/Wadi.

(iii) Kiongozi ngazi ya Kata/Wadi; mamlaka yake ya nidhamu itakuwa ni Kamati Tendaji ya Jimbo/Wilaya

(iv) Kiongozi ngazi ya Jimbo/Wilaya mamlaka yake ya nidhamu itakuwa ni Baraza la Uongozi la Mkoa.

(v) Kiongozi ngazi ya mkoa mamlaka

yake ya nidhamu itakuwa ni kamati tendaji ya kanda

(vi) Kiongozi ngazi ya kanda; mamlaka ya yake ya nidhamu itakuwa ni kamati kuu.

(vii) Viongozi wa kitaifa; isipokuwa mwenyekiti na makamu mwenyekiti mamlaka yao ya nidhamu itakuwa ni Kamati Kuu.

(viii) Mwenyekiti wa Chama Taifa na Makamu Wenyeviti mamlaka yao ya nidhamu itakuwa ni Baraza Kuu.

(b) Vikao vya Baraza la Mashauriano la Ngazi ya Mkoa na Baraza la Uongozi la Ngazi ya Kanda vitakuwa na hadhi ya Mkutano Mkuu katika ngazi hizo.

(c) Kiongozi aliyeteuliwa na vikao vya uongozi ataweza kusimamishwa au kuachishwa uongozi na kikao kilichomteua.

(d) Bila kuathiri masharti ya vipengele (a) na (c) hapa juu, kiongozi yeyote anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa au kuachishwa uongozi na kikao cha juu ya ngazi yake ya uongozi.

(e) Kiongozi aliyechukuliwa hatua za nidhamu na mamlaka yake ya nidhamu anayo haki ya kukata rufaa

ngazi ya juu ya ile ya mamlaka yake ya nidhamu na uamuzi wa ngazi hiyo utakuwa wa mwisho.

(f) Rufaa ni lazima ikatwe ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kupokea rasmi kwa maandishi maamuzi ya mamlaka iliyotoa adhabu.

(g) Viongozi wa ngazi ya kitaifa waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wanaweza kusimamishwa uongozi endapo theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza Kuu watapiga kura ya siri ya kutokuwa na imani na kiongozi husika. Baraza Kuu litakuwa na wajibu wa kuteua atakayeshika nafasi hiyo kwa muda hadi uamuzi wa mwisho kufanywa na Mkutano Mkuu.

(h) Bila kuzingatia masharti ya ibara 6.3.6(a)(vii)(viii)Kamati Kuu itakuwa na mamlaka ya kumsimamisha Kiongozi wa kitaifa kama kutakuwa na ushahidi kuwa maslahi na uwepo wa Chama upo hatarini.

(i) Bila kuathiri aya ya (c) na (h) katika ibara hii taarifa ya Kamati Kuu kuhusu hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya kiongozi wa kitaifa itawasilishwa kwenye Baraza Kuu.

(j) Bila kuathiri aya ya (h) na (i) katika ibara hii hatua zote za kinidhamu zitafanyika kwa mujibu wa Kanuni.

6.3.7 Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ndani ya Chama (TEHAMA);

(a) Teknolojia ya habari na mawasiliano ndani ya chama itakuwa ni mojawapo ya njia za mawasiliano rasmi ndani ya chama, kutunza kumbukumbu za vikao, mali, wanachama na kutafuta rasilimali.

(b) Utaratibu wa matumizi ya TEHAMA utawekwa kwenye mwongozo utakaoandaliwa na Baraza Kuu kwa ajili hiyo.

# SURA YA SABA

## 7.0 NGAZI ZA UONGOZI

Ngazi za Uongozi na Maju kumu yake

### 7.1 Ngazi ya Msingi

7.1.1 Ngazi ya chini kabisa katika muundo wa chama ni ngazi ya Msingi. Ngazi hii itaundwa katika eneo la Kitongoji kwa Vijijini, eneo la Mtaa mdogo wa kichama mijini kwa Tanzania Bara na katika sehemu ya Shehiya za kiutawala Tanzania Zanzibar yenye wanachama wasiopungua thelathini.

7.1.2 Ngazi ya Msingi itaundwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika kanuni zilizotungwa na Baraza Kuu la Chama.

7.1.3 Ngazi ya Msingi itakuwa na viongozi wafuatao;

(a) Mwenyekiti

(b) Katibu

(c) Wenyeviti wa Mabaraza ngazi ya Msingi

(d) Balozi wa kila Kaya kumi zilizopo ndani ya Msingi

(e) Mwenyekiti wa Kitongoji anayetokana na Chama.

(f) Kiongozi wa Kijiji anayeishi katika Kitongoji husika.7.1.4 Viongozi wa ngazi ya Msingi watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa ngazi ya Msingi kwa kuzingatia Kanuni zitakazotungwa na Baraza Kuu.

7.1.5 Ngazi ya Msingi itakuwa na vikao vifuatavyo;
(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Uongozi

7.1.6 Mkutano Mkuu ndio kikao kikuu kupita vyote na wajumbe wake watakuwa ni wanachama wote wa Msingi husika.

7.1.7 Mkutano Mkuu wa ngazi ya Msingi utafanyika mara nne kwa mwaka. Mikutano maalum/ dharura inaweza kuitishwa wakati wowote na Kamati ya Uongozi kadri itakavyolazimu.,

7.1.8 Kazi za Mkutano Mkuu wa ngazi ya Msingi;
(a) Kuchagua viongozi wa ngazi ya Msingi kama walivyoainishwa katika Ibara ya 7.1.3.
(b) Kupendekeza wagombea katika uchaguzi wa kiserikali wa Vitongoji na kuwasilisha kwa Kamati ya Utendaji ya Tawi kwa maamuzi ya mwisho.
(c) Kujadili taarifa za Kamati ya Uongozi na kutoa maamuzi au maelekezo/ mwongozo wa utekelezaji.

(d) Kujadili na kuzingatia hali ya uhai wa Chama.

(e) Kujadili na kuzingatia masuala ya kijamii katika eneo lao.

(f) Kuteua mabalozi wa nyumba kumi.

(g) Kazi za mabalozi wa nyumba kumi wanaotokana na Chama zitaainishwa kwenye Mwongozo utakaotungwa na Baraza kuu.

7.1.9 Wajumbe wa Kamati ya Uongozi watakua ni viongozi walioainishwa katika Ibara ya 7.1.3

7.1.10 Kamati ya Uongozi itakutana mara sita kwa mwaka; yaani kila baada ya miezi miwili. Vikao maalum / dharura vinaweza kuitishwa kadri itakavyolazimu.

7.1.11 Kazi za Kamati ya Uongozi ni:

(a) Kuendesha shughuli za kila siku za chama katika eneo lake.

(b) Kuandaa mikutano mikuu ya ngazi ya Msingi

(c) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Itikadi, Falsafa, Sera na Madhumuni ya Chama.

(d) Kuendesha na kusimamia kampeni za uchaguzi wa wagombea wa Chama katika chaguzi wa serikali.

(e) Kusimamia nidhamu ya wanachama katika ngazi ya Msingi na kuchukua

hatua kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na Maadili ya Chama.(f) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya ngazi husika.

(g) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.

**7.2 Ngazi ya Tawi**

7.2.1 Tawi litaundwa katika kila eneo la kijiji, mtaa au Shehiya ya kiutawala katika mamlaka za serikali za Mitaa.

7.2.2 Tawi litaundwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Chama zilizotungwa na Baraza Kuu la Chama.

7.2.3 Ngazi ya Tawi itakuwa na viongozi wafuatao:(a) Mwenyekiti

(b) Katibu

(c) Katibu Mwenezi

(d) Mweka Hazina

(e) Wenyeviti wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Tawi

(f) Makatibu wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Tawi

(g) Wataalamu wasiopungua wawili wa kuteuliwa na Mwenyekiti kulingana na mahitaji kwa kushauriana na Kamati ya Utendaji ya Tawi.

(h) Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa anaye tokana na Chama.

(i) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa viongozi wa serikali ya Kijiji/Mtaa husika kwa mujibu wa Mwongozo.

7.2.4 Viongozi (a) – (d) watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi na wale wa (e) na (f) watachaguliwa na Mabaraza husika kwa kuzingatia Kanuni za Chama zilizotungwa na Baraza Kuu la Chama.

7.2.5 Ngazi ya Tawi itakuwa na vikao vifuatavyo;

(a) Mkutano Mkuu

(b) Kamati ya Utendaji

7.2.6 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi watakuwa ni wanachama wote wa Chama katika Tawi.

7.2.7 Mkutano Mkuu wa Tawi utakutana mara mbili kwa mwaka. Mkutano Mkuu maalum/ dharura inaweza kuitishwa wakati wowote na Kamati ya Utendaji kadri itakavyolazimu.

7.2.8 Kazi za Mkutano Mkuu wa Tawi zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Kuchagua viongozi wa tawi kama walivyoainishwa katika ibara ya 7.2.3 (a) hadi (d).

(b) Kuchagua wawakilishi wawili wa tawi kuingia katika Mkutano Mkuu wa Kata.

(c) Kujadili taarifa ya Kamati ya Utendaji ya tawi na kutoa maamuzi au maelekezo / mwongozo wa utekelezaji.

(d) Kuzingatia na kutoa maelekezo kwa Kamati ya Utendaji ya tawi kuhusu utekelezaji wa maamuzi na maaagizo ya vikao vya juu.

(e) Kuzingatia na kujadili utekelezaji wa Itikadi, Falsafa, Sera na Mipango ya Chama inayohusu masuala ya jamii katika eneo la tawi yaani kijiji, mtaa au Shehiya.

(f) Kutoa mwongozo/maelekezo kwa wawakilishi wa Chama walio kwenye serikali ya kijiji au kamati ya mtaa au katika Shehiya.

(g) Kujadili na kuzingatia taarifa za utendaji wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee katika Tawi na kutoa maelekezo.

(h) Kuidhinisha Programu za Chama katika eneo lao.

(i) Kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti na wajumbe wa serikali za Kijiji/Mtaa.

7.2.9 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi watakuwa wale walioainishwa kwenye Ibara 7.2.3.

7.2.10 Kamati ya Utendaji ya Tawi itakutana mara nne kwa mwaka yaani kila baada ya miezi mitatu. Vikao maalum/dharura vinaweza kuitishwa kadri itakavyolazimu.

7.2.11 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Tawi:-

(a) Kufanya uteuzi wa awali wa wagombea wa Chama katika chaguzi za serikali za Mitaa/Vijiji na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji/Tawi kwa uteuzi wa mwisho.

(b) Kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea uenyekiti wa Vitongoji

(c) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Tawi

(d) Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Chama za kila siku tawini.

(e) Kusimamia na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wanachama na viongozi ngazi ya Msingi kwa mujibu wa masharti ya Katiba na kanuni za Chama.

(f) Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa Chama katika ngazi ya Msingi

(g) Kuandaa mikakati na kusimamia kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali.

(h) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Itikadi, Falsafa, Sera na Madhumuni ya Chama.

(i) Kutekeleza maamuzi ya vikao vya juu vya Chama.

(j) Kuweka kumbukumbu sahihi za uanachama katika madaftari ya wanachama kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(k) Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama kitawi na kuziwasilisha kwenye ngazi ya Kata kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(l) Kuweka katika majalada maalum kumbukumbu za vikao na nyaraka nyingine za mawasiliano katika Chama.

(m) Kufuatilia utendaji kazi wa vikao vya uongozi ngazi ya Msingi na kutoa ushauri ama msaada kadri itakavyowezekana.

(n) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya tawi husika.

(o) Kufuatilia utendaji na utekelezaji wa maelekezo ya Chama kwa viongozi wawakilishi wa Chama katika serikali za Vijiji, Mitaa na Shehia.

(p) Kutoa msaada kila inapobidi kwa viongozi wawakilishi wa Chama ndani ya Serikali za Vijiji, Mitaa na Shehiya.

(q) Kutayarisha na kusimamia programu za Chama katika ngazi husika.(r) Kumchagua mwakilishi wa Tawi katika Kamati ya Utendaji ya Kata.

(s) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.

(t) Kusimamia utendaji wa Mabaraza ya Vijana,Wanawake na Wazee kwenye Tawi husika.

## 7.3 Ngazi ya Kata/Wadi

7.3.1 Ngazi hii itaundwa katika eneo la Kata/Wadi ya kiutawala katika mamlaka zote za serikali za Mitaa, yaani za Vijijini na za Mijini.

7.3.2 Ngazi ya Kata/Wadi itaundwa kwa kuzingatia masharti ya kanuni zilizotungwa na Baraza Kuu la Chama.

7.3.3 Viongozi wa ngazi ya Kata/Wadi ni kama ifuatavyo:-

- (a) Mwenyekiti
- (b) Katibu
- (c) Katibu Mwenezi
- (d) Mweka Hazina
- (e) Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Kata.
- (f) Mjumbe wa Mkutano Mkuu aliyechaguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 7.3.7 (b) ya Katiba hii.

7.3.4 Vikao vya Kata/Wadi

- (a) Mkutano Mkuu wa Kata
- (b) Kamati ya Utendaji ya Kata
- (c) Sekretariat ya kata

7.3.5 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi watakuwa kama ifuatavyo;

- (a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya Kata.

(b) Wenyeviti wote wa matawi katika Kata.

(c) Makatibu wote wa matawi katika Kata.

(d) Wenyeviti wote wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee katika Kata.

(e) Makatibu wote wa mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee katika Kata.

(f) Viongozi wote wa Umoja wa Serikali za Vijiji/Mitaa ngazi ya Kata.

7.3.6 Mkutano Mkuu wa Kata utakutana mara mbili kwa mwaka. Mikutano maalum/dharura inaweza kuitishwa wakati wowote na Kamati ya Utendaji kadri itakavyolazimu.

7.3.7 Kazi za Mkutano Mkuu wa Kata:-

(a) Kuchagua viongozi wa Kata kama walivyoainishwa katika ibara ya 7.3.3. (a) – (d).

(b) Kuchagua mwakilishi wa Kata katika Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya.

(c) Kujadili taarifa za Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi na kutoa maamuzi au maelekezo kwa utekelezaji

(d) Kuzingatia na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi juu ya maamuzi na maagizo ya vikao vya juu

(e) Kuzingatia, kujadili na kuweka miongozo ya utekelezaji wa Falsafa na Sera za Chama katika Kata/Wadi.

(f) Kutoa mwongozo na maelekezo kwa wawakilishi wa Chama kwenye Halmashauri husika za Serikali za Mitaa.

(g) Kuzingatia na kutoa mapendekezo kwa ngazi za juu, kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayo jitokeza katika Kata na yanahitaji hatua za kichama ngazi za juu

(h) Kusikiliza na kutoa uamuzi au mapendekezo kwa ngazi ya juu, kuhusu masuala ya kinidhamu kwa wanachama au viongozi wa Chama kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Kanuni za Chama.

(i) Kuidhinisha Programu ya Chama katika Kata/Wadi.

(j) Kujadili na kuzingatia taarifa za utendaji wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee katika Kata/ Wadi.

7.3.8 Wajumbe Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi.

(a) Mwenyekiti

(b) Katibu

(c) Katibu Mwenezi

(d) Mweka Hazina

(e) Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Kata.

(f) Mwakilishi mmoja aliyechaguliwa na Kamati ya Utendaji ya kila Tawi.

(g) Mjumbe wa Mkutano Mkuu aliyechaguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 7.3.7 (b).

(h) Diwani wa Kata na Diwani wa viti maalum anayeishi katika Kata husika

(i) Mwenyekiti na Katibu wa umoja wa viongozi wa serikali za Mitaa na Vijiji ngazi ya Kata.

7.3.9 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi;

(a) Kufanya uteuzi wa awali wa wagombea wa Chama katika uchaguzi wa madiwani.

(b) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu ya Kata/Wadi.

(c) Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Chama za kila siku katika Kata/Wadi.

(d) Kusimamia na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wanachama, watendaji na viongozi wa Kata/Wadi kwa mujibu wa masharti ya Katiba na Kanuni za Chama.

(e) Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa Chama katika Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

(f) Kuandaa mikakati na kusimamia kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali.

(g) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Itikadi, Falsafa, Sera na Madhumuni ya Chama.

(h) Kutekeleza maamuzi ya vikao vya juu vya Chama.

(i) Kuweka kumbukumbu sahihi za wanachama na wafuasi wa Chama katika madaftari kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(j) Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama ngazi ya Kata/Wadi na kuziwasilisha kwenye ngazi ya Jimbo/Wilaya kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(k) Kuweka katika majalada maalum kumbukumbu za vikao na nyaraka nyingine za mawasiliano katika Chama.

(l) Kufuatilia utendaji kazi wa viongozi wa kiserikali waliotokana na Chama ngazi husika na kutoa ushauri kwa kadri inavyowezekana

(m) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya Kata/Wadi husika.

(n) Kufuatilia utendaji na utekelezaji wa maelekezo ya Chama kwa viongozi wawakilishi wa Chama katika Halmashauri za Serikali za Mitaa.

(o) Kutoa msaada kila inapobidi kwa viongozi wawakilishi wa Chama katika Halmashauri za Serikali za Mitaa.

(p) Kutayarisha na kusimamia programu za Chama katika ngazi husika.

(q) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.

(r) Kusimamia utendaji wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee katika Kata/Wadi.

7.3.10 Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi itakutana mara nne kwa mwaka yaani kila baada ya miezi mitatu. Vikao maalum/dharura vinaweza kuitishwa kadri itakavyolazimu.

7.3.11 Wajumbe wa sekretarieti ya kata watakua wafuatao;

(a) Katibu wa Kata atakuwa Mwenyekiti wa Sekretariat

b) Katibu mwenezi wa Kata

c) Mweka Hazina wa Kata

d) Makatibu wa mabaraza ya chama ndani ya Kata

e) Katibu wa umoja wa wenyeviti wa Serikali za vijiji/mitaa ngazi ya kata.

7.3.12 Kazi za Sekretariat ya Kata zitakuwa kama ifuatavyo:-

i. Uendeshaji wa shughuli za kila siku za chama.

ii. Uandaaji wa agenda, nyaraka kwa ajili ya vikao vya Kamati ya Utendaji na Mkutano Mkuu wa Kata.

## 7.4 Ngazi ya Wilaya/Jimbo la Uchaguzi

7.4.1 Ngazi za Wilaya/Majimbo zitakuwa na miundo ya aina mbili;

(a) Wilaya zenye Jimbo moja la Uchaguzi wa Bunge/Baraza la Wawakilishi

(b) Wilaya zenye zaidi ya Jimbo moja la uchaguzi

(c) Aidha katika miundo yote miwili, Wilaya/Majimbo ambayo yametimiza masharti yafuatayo yatajulikana kama Wilaya/Majimbo ya Chama:-

(i) Wilaya zenye muundo wa Chama uliokamilika toka katika ngazi ya chini kabisa hadi ya juu.

(ii) Wilaya/ Jimbo zenye timu kamili ya viongozi wa kuchaguliwa kikatiba katika ngazi zote za chini.

(iii) Wilaya/Jimbo zenye Uongozi wa Wilaya wa kuchaguliwa uliokamilika.

(iv) Majimbo ya Mkoa wa Dar es Salaam yatakuwa na hadhi ya Wilaya.

7.4.2 Ngazi ya Jimbo/Wilaya ya Jimbo itaundwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Chama zilizotungwa na Baraza kuu la Chama.

**Viongozi wa Wilaya yenye Jimbo Moja la Uchaguzi**

7.4.3 Viongozi wa Wilaya zenye Jimbo moja la uchaguzi watakuwa wafuatao;
(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Katibu mwenezi
(d) Mweka Hazina
(e) Wenyeviti wa Mabaraza ngazi ya kata katika Jimbo/Wilaya
(f) Makatibu wa Mabaraza ngazi ya Wilaya/Jimbo

7.4.4 Vikao vya Wilaya zenye Jimbo moja la Uchaguzi vitakuwa vifuatavyo:-
(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji ya Jimbo/Wilaya
(c) Sekretarieti ya Jimbo/Wilaya

7.4.5 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo/ Wilaya watakuwa;
(a) Wajumbe wote wa kamati ya Utendaji
(b) Wenyeviti wote wa kata za Jimbo/ Wilaya
(c) Makatibu wote wa kata za Jimbo/ Wilaya
(d) Makatibu Waenezi wote wa Kata za Jimbo/Wilaya
(e) Waweka hazina wote wa Jimbo/ Wilaya.
(f) Wenyeviti wa mabaraza ya Chama ngazi ya kata katika Jimbo/Wilaya

(g) Makatibu wa mabaraza wote wa kata/ wadi katika Jimbo/Wilaya

(h) Wajumbe wa kila kata waliochanguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 7.3.7(b)

(i) Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Chama katika Wilaya.

7.4.6 Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya utafanyika mara moja kwa mwaka. Mikutano maalum/ dharura inaweza kuitishwa wakati wowote na Kamati ya Utendaji kadri itakavyolazimu.

7.4.7 Kazi za Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya zitakuwa:

(a) Kuchagua viongozi wa Kamati ya Utendaji ya Wilaya/Jimbo na kupendekeza majina ya wanaopendekezwa kuwa Katibu wa Jimbo/Wilaya kwa Kamati ya Utendaji ya Kanda.

(b) Kuzingatia na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Kamati ya Utendaji ya Jimbo/Wilaya juu ya maamuzi na maagizo ya vikao vya juu.

(c) Kujadili taarifa za Kamati ya Utendaji ya Wilaya na kutoa maamuzi au maelekezo kwa utekelezaji.

(d) Kuzingatia, kujadili na kuweka miongozo ya utekelezaji wa Falsafa na Sera za Chama katika Wilaya

(e) Kutoa mwongozo na maelekezo kwa wawakilishi wa Chama katika Halmashauri za Serikali za Mitaa.

(f) Kuzingatia na kutoa mapendekezo kwa ngazi za juu, juu ya masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayojitokeza katika Wilaya na yanayohitaji hatua za kichama ngazi za juu.

(g) Kusikiliza na kutoa uamuzi au mapendekezo kwa ngazi ya juu, kuhusu masuala ya kinidhamu kwa wanachama au viongozi wa Chama kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Kanuni za Chama.

(h) Kuidhinisha Programu za Chama katika Jimbo/Wilaya.

(i) Kuchagua mwakilishi wa wilaya kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa.

7.4.8 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo/ Wilaya yenye Jimbo moja watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Mwenyekiti

(b) Katibu

(c) Katibu Mwenezi

(d) Mweka Hazina

(e) Wenyeviti wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Wilaya/Jimbo

(f) Makatibu wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Wilaya/Jimbo

(g) Mbunge/Mwakilishi wa Chama anayeishi katikaJimbo/Wilaya

(h) Mwenyekiti na Makamu wake wa Halmashauri inayoongozwa na Chama.

(i) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Wilaya au mwakilishi wa madiwani pale ambapo umoja huo haupo.

(j) Wajumbe wasiozidi wanne watakao chaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo/ Wilaya angalau wawili kati yao wawe wanawake.

(k) Wajumbe maalum wawili watakaoteuliwa na kamati ya utendaji ya wilaya/ Jimbo.

(l) Mjumbe wa Mkutano Mkuu Taifa aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo.

(m) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa Serikali za Vijiji/Mitaa ngazi ya Wilaya.

(n) Kutakuwa na Wajumbe maalum wawili, walioteuliwa na Kamati ya Utendaji ya Kanda kuingia Kamati ya Utendaji ya Jimbo/Wilaya.

(o) Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa wanaotokana na Mabaraza wanaoishi katika Jimbo/ Wilaya husika ”.

7.4.9 Kamati ya Utendaji ya Jimbo/Wilaya itakutana mara nne kwa mwaka yaani kila baada ya miezi mitatu. Vikao maalum/ dharura vinaweza kuitishwa kadri itakavyolazimu.

7.4.10 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Jimbo/ Wilaya:

(a) Kuthibitisha mapendekezo ya uteuzi wa wagombea udiwani katika Kata/ Wadi zilizo ndani ya Jimbo/Wilaya.

(b) Kutoa mapendekezo juu ya orodha ya wagombea wa udiwani wa viti maalum inayowasilishwa na Baraza la Wanawake ngazi ya Jimbo.

(c) Kuandaa na kuthibitisha agenda za Mikutano Mikuu ya Jimbo/Wilaya.

(d) Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Chama Jimbo/Wilaya.

(e) Kusimamia na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wanachama na viongozi wa Kata/Wadi kwa mujibu wa masharti ya Katiba na Kanuni za Chama

(f) Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa Chama katika Kata/Wadi.

(g) Kuandaa mikakati na kusimamia kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali.

(h) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Itikadi, Falsafa, Sera na Madhumuni ya Chama.(i) Kutekeleza maamuzi ya vikao vya juu vya Chama.

(j) Kuweka kumbukumbu sahihi za wanachama katika madaftari ya

wanachama kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(k) Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama katika Jimbo/Wilaya na kuziwasilisha kwenye ngazi ya Taifa kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(l) Kuweka katika majalada maalum kumbukumbu za vikao na nyaraka nyingine za mawasiliano katika Chama.

(m) Kujadili taarifa za Sekretariati ya Jimbo/Wilaya na kutoa maamuzi au maelekezo ya utekelezaji.

(n) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya Jimbo/Wilaya .

(o) Kufuatilia utendaji na utekelezaji wa maelekezo ya Chama kwa viongozi wawakilishi wa Chama katika Halmashauri za serikali za Mitaa na inapobidi kutoa ushauri na msaada pindi unapohitajika.

(p) Kutayarisha na kusimamia programu za Chama katika ngazi husika.

(q) Kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya rufaa za uchaguzi wa Chama katika ngazi ya Kata/Wadi.(r) K u f a n y a uteuzi wa awali wa wagombea Ubunge na Uwakilishi (Zanzibar).

(s) Kupendekeza kwa Kamati Kuu majina ya wagombea wa nafasi ya

Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti na Mameya/Manaibu Meya.

(t) Kupendekeza mgombea wa nafasi ya Meya/ Naibu Meya wa mamlaka ya Miji na Miji midogo.

(u) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.

(v) Kuthibitisha wajumbe wateule wa kamati ya utendaji waliopendekezwa na Mwenyekiti kwa kushauriana na Katibu wa Jimbo/Wilaya

(w) Kusimamia utendaji wa Mabaraza ya Vijana,Wanawake na Wazee katika Jimbo/Wilaya.

(x) Kumwachisha ujumbe wa Kamati ya Utendaji mjumbe mteule ambaye ataenda kinyume na Katiba, Kanuni na Maadili ya Chama ama hatakidhi matakwa ya kuteuliwa kwake.

7.4.11 Wajumbe wa Sekretariat ya Jimbo/Wilaya watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Katibu wa Jimbo/Wilaya

(b) Katibu Mwenezi wa Jimbo/Wilaya

(c) Mweka Hazina wa Jimbo/Wilaya(d) Makatibu wa Mabaraza ya Chama ndani ya Jimbo/Wilaya

(e) Katibu wa umoja wa madiwani wa Wilaya

(f) Katibu wa umoja wa Viongozi wa serikali za Vijiji/Mitaa Wilaya

(g) Mratibu wa Masuala ya sheria wa Jimbo/Wilaya.

(h) Mratibu wa TEHAMA wa Jimbo/ Wilaya.

7.4.12 Kazi za Sekretarieti ya Jimbo zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji wa shughuli za chama.

(b) Utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Kamati ya Utendaji.

(c) Uandaaji wa agenda, nyaraka kwa ajili ya vikao vya Kamati ya Utendaji na Mkutano Mkuu.

**Wilaya zenye zaidi ya Jimbo Moja la Uchaguzi**

7.4.13 Kutakuwa na vyombo viwili vya uongozi ambavyo ni:-

(a) Baraza la Uongozi la Wilaya

(b) Vikao vya Mashauriano vya Wilaya

7.4.14 Baraza la Uongozi la Wilaya litakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi Wilaya

(b) Katibu wa Baraza la Uongozi la Wilaya

(c) Wenyeviti wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Wilaya.

(d) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Wilaya au mwakilishi wa madiwani pale ambapo umoja huo haupo.

(e) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa Serikali za Vijiji/Mitaa ngazi ya Wilaya /Halmashauri.

7.4.15 Kazi za Baraza la Uongozi la Wilaya zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Kuwa kiunganishi baina ya Jimbo na Jimbo ndani ya Wilaya na Kati ya Jimbo na ngazi za juu.

(b) Kutoa ushauri na misaada ya kiutendaji kwa majimbo ndani ya Wilaya

(c) Kuratibu shughuli za kampeni ya wagombea Urais na Mgombea Mwenza wa Chama katika Wilaya nzima.

(d) Kuratibu na kuunganisha shughuli za mabaraza yote ya Chama katika Wilaya.

(e) Kuwa kiunganishi cha Chama na shughuli za Kiserikali ndani ya Wilaya.

(f) Kuratibu na kutoa taarifa kwa ngazi za juu za chama juu ya hali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutawala ngazi ya Wilaya husika.

(g) Kuandaa na kutayarisha mikutano ya vikao vya Mashauriano.

7.4.16 Vikao vya Mashauriano vya Wilaya vitakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe wote wa Baraza la Uongozi Wilaya

(b) Wenyeviti wa Majimbo ndani ya Wilaya

(c) Makatibu wa Majimbo ndani ya Wilaya

(d) Wenyeviti Mabaraza ya Chama ndani ya Wilaya

(e) Makatibu Mabaraza ya Chama ndani ya Wilaya

(f) Makatibu Waenezi wa Majimbo ndani ya Wilaya

7.4.17 Kazi za Vikao vya Mashauriano zitakuwa ni:

(a) Kujadili na kuweka msimamo wa pamoja wa kiutekelezaji kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii na kiutawala ndani ya Wilaya.

(b) Kujadili na kutoa ushauri ngazi za juu kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii na kiutawala yanayohitaji kuchukuliwa hatua na ngazi hizo.

(c) Kushauriana na kukubaliana juu ya ratiba ya kampeni ya wagombea Urais wa Chama na kujiwekea mgawanyo wa majukumu.

(d) Kujadili na kutoa ushauri kwa viongozi wa Chama wa Majimbo na kwa Mamlaka ya Utawala wa Serikali za Mitaa unaoongozwa na Chama.

(e) Kumchagua mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Wilaya.

(f) Kupendekeza kwa Kamati ya Utendaji ya Kanda jina la Katibu wa Baraza la Uongozi Wilaya.

(g) Kushughulikia rufaa za maamuzi ya kinidhamu kutoka ngazi ya Kata/Wadi.

## 7.5 Ngazi ya Mkoa

7.5.1 Ngazi hii itaundwa katika kila eneo la Mkoa wa kiutawala wa Serikali Kuu isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam. Katika ngazi hii ya Mkoa, patakuwa na Mikoa ya Chama ambayo imetimiza masharti yafuatayo:-

(a) Muundo wa Chama uliokamilika toka katika ngazi ya chini kabisa toka Wilaya hadi Mkoa.

(b) Timu kamili ya viongozi wa kuchaguliwa kikatiba katika ngazi zote.

(c) Wilaya za Dar es salaam zitakuwa na hadhi ya Mkoa.

7.5.2 Ngazi ya Mkoa itakuwa na vyombo viwili vya uongozi kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Uongozi la Mkoa

(b) Vikao vya Mashauriano kimkoa

7.5.3 Wajumbe wa Baraza la Uongozi la Mkoa watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi Mkoa

(b) Katibu wa Baraza la Uongozi Mkoa

(c) Wenyeviti wa Mabaraza ya Chama ndani ya Mkoa

(d) Mjumbe wa Kamati Kuu anayeishi katika Mkoa husika na aliyejisajili katika Msingi ndani ya Mkoa husika.

(e) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa madiwani ngazi ya Mkoa.

(f) Mwenyekiti na Katibu wa Wabunge ndani ya Mkoa

(g) Wajumbe wa Baraza Kuu wanaotokana na Mabaraza wanaoishi katika Mkoa husika.

7.5.4 Kazi za Baraza la Uongozi la Mkoa zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Kuwa kiunganishi baina ya Wilaya ndani ya Mkoa na Wilaya na ngazi za juu.

(b) Kutoa ushauri na misaada ya kiutendaji kwa uongozi wa Wilaya za Mkoa.

(c) Kuratibu shughuli za kampeni za wagombea urais katika Mikoa na mgawanyo wa majukumu ki-wilaya.

(d) Kuratibu na kuunganisha shughuli za mabaraza yote ya Chama katika Mkoa.

(e) Kuwa kiunganishi cha Chama na shughuli za kiserikali katika mkoa

(f) Kuratibu na kutoa taarifa kwa chama ngazi ya Kanda juu ya hali ya kisiasa, kijamii na kiutawala ndani ya Mkoa.

(g) Kuandaa na kutayarisha mikutano ya vikao vya Mashauriano.

(h) Kuwa mamlaka ya nidhamu kwa viongozi wa Jimbo/Wilaya.

7.5.5 Vikao vya Mashauriano Ngazi ya Mkoa vitakuwa na Wajumbe Wafuatao;

(a) Wajumbe wote wa Baraza la Uongozi la Mkoa.

(b) Wenyeviti na Makatibu wa Majimbo/ Wilaya katika Mkoa.

(c) Makatibu Wenezi wa Majimbo katika Mkoa.

(d) Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Jimbo/Wilaya.

(e) Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za uratibu za mabaraza ya Chama za Wilaya (yenye Jimbo zaidi ya moja).

(f) Makatibu wa mabaraza ya chama ngazi ya Mikoa.

(g) Wajumbe wa Baraza Kuu wanaotokana na Mabaraza wanaoishi katika Mkoa husika.

(h) Wabunge/ Wawakilishi wote ndani ya Mkoa husika.

7.5.6 Kazi za Vikao vya Mashauriano

(a) Kujadili na kuweka msimamo mmoja wa kiutekelezaji kuhusu maswala ya kisiasa, kijamii na kiutawala ndani ya Mkoa.

(b) Kujadili na kutoa ushauri ngazi za juu kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii na kiutawala yanayohitaji kuchukuliwa hatua na ngazi hizo.

(c) Kushauriana na kukubaliana juu ya utekelezaji wa ratiba ya kampeni

ya wagombea Urais na Mgombea Mwenza wa Chama na kujiwekea mgawanyo wa majukumu.

(d) Kujadili na kutoa ushauri kwa viongozi wa chama wa Majimbo, Wabunge/ Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa Mamlaka za Utawala wa Serikali za Mitaa unaoongozwa na Chama.

(e) Kumchagua Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi Mkoa.

(f) Kupendekeza kwa Kamati ya Utendaji ya Kanda jina la Katibu wa Baraza la Uongozi Mkoa.7.5.7 Vikao vya Mashauriano vitafanyika mara moja kwa mwaka lakini vikao maalum/ vya dharura vinaweza kufanyika kwa maombi maalum toka wilayani au kwa maelekezo kutoka ngazi ya Taifa.

## 7.6 Ngazi ya Kanda

7.6.1 Kutakuwa na Kanda za Chama kwa taratibu zitakazowekwa na Baraza Kuu kutokana na mahitaji ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

7.6.2 Ngazi ya Kanda itakuwa na vikao vitatu vya Uongozi.

(a) Baraza la Uongozi la Kanda

(b) Kamati ya Utendaji ya Kanda

(c) Sekretarieti ya Kanda

7.6.3 Wajumbe wa Baraza la Uongozi la Kanda watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya Kanda.

(b) Wajumbe wa Kamati Kuu ambao wamesajiliwa katika ngazi ya Msingi ndani ya Kanda husika.

(c) Wenyeviti na Makatibu wa Wilaya/ Majimbo ndani ya Kanda

(d) Wabunge/Wawakilishi wanaotoka katika Kanda husika.

(e) Wajumbe wote wa mabaraza ya Uongozi ya Mikoa ndani ya Kanda husika.

(f) Mameya/Wenyeviti wa Halmashauri wa CHADEMA ndani ya Kanda husika.

(g) Mwenyekiti na Katibu wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda.

7.6.4 Kazi za Baraza la Uongozi la Kanda zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Kitakuwa Chombo cha juu cha maamuzi ya kisera na kisiasa ndani ya Kanda.

(b) Kusimamia utendaji wa Kamati ya Utendaji ya Kanda.

(c) Kuchagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Mtunza Hazina wa Kanda.

(d) Kuthibitisha Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Kitaalam za Kanda kwa

kuzingatia sifa na vigezo vilivyowekwa baada ya kupokea mapendekezo ya Kamati ya Utendaji.

(e) Kusimamia na kuendesha kampeni wakati wa chaguzi za kiserikali.

7.6.5 Baraza la Uongozi la Kanda litakutana mara mbili ndani ya miaka mitano. Vikao maalumu au vya dharura vitafanyika kwa maombi maalumu kutoka Mikoani kwa maalekezo kutoka Taifa.

7.6.6 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kanda ni:-

(a) Mwenyekiti

(b) Makamu Mwenyekiti

(c) Wajumbe wote wa Sekretariet ya Kanda isipokuwa Maafisa wa Kanda na Makatibu wa Kamati za Kitaalam hawatakuwa na kura.

(d) Wenyeviti wa Mabaraza ngazi ya Kanda

(e) Mwenyekiti wa wabunge ndani ya Kanda

(f) Mwenyekiti Umoja wa Madiwani ndani ya Kanda

(g) Wenyeviti wa Kamati za kitaalamu zitakazoundwa kwa mahitaji maalum.

(h) Wenyeviti wa Mikoa ndani ya Kanda husika.

7.6.6 Kazi ya Kamati ya Utendaji ya Kanda ni-:

(a) Kuandaa mpango kazi wa Chama ndani ya Kanda

(b) Kusimamia utendaji kazi wa ngazi za chini za Kanda.

(c) Kusimamia nidhamu ya Makatibu wa Chama ndani ya Kanda.

(d) Kusimamia utekelezaji wa maelekezo kutoka ngazi ya Taifa.

(e) Kuteua maafisa wa ofisi ya Kanda

(f) Kuthibitisha uteuzi wa Makatibu wa Mikoa, Wilaya na Majimbo

(g) Kuteua wajumbe maalum wawili kuingia Kamati ya Utendaji ya Jimbo/ Wilaya.

(h) Kusimamia Sekretariat ya Kanda.

(i) Kuwa mamlaka ya nidhamu kwa madiwani ndani ya Kanda.

(j) Kushauri Kamati Kuu kuhusu uteuzi na nidhamu ya Wabunge, Mameya/ Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani ndani ya Kanda.

7.6.7 Kamati ya utendaji ya Kanda itakutana mara nne kwa mwaka. Vikao maalumu au vya dharura vinaweza kuitishwa muda wowote kadiri itakavyolazimu.

7.6.8 Wajumbe wa Sekretarieti ya Kanda ni:-

(a) Katibu wa Kanda atakuwa Mwenyekiti wa Sekretariat na atapendekezwa na Sekretariat ya Kamati Kuu kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Kanda husika kutoka miongoni mwa Wanachama wenye sifa na kuthibitishwa na Kamati Kuu.

(b) Makatibu wa Kamati zote za kudumu za Kanda

(c) Makatibu wa Mabaraza ngazi ya Kanda.

(d) Mtunza Hazina wa Kanda

(e) Katibu wa umoja wa Wabunge ndani ya Kanda

(f) Katibu wa umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda

(g) Maafisa wa kanda

7.6.9 Kazi za Sekretarieti ya Kanda zitakuwa ni kama ifuatavyo;

(a) Kuwa chombo cha Utendaji cha Kamati ya Utendaji ya Kanda

(b) Kuzisimamia, kuendesha na kuratibu shughuli za kila siku za Kanda

(c) Kutekeleza maagizo ya kila mara kutoka ngazi ya Taifa.

7.6.10 Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Kanda zitakazoundwa kama ifuatavyo-:

(a) Kamati ya Fedha na Rasilimali

(b) Kamati ya Mafunzo

(c) Kamati ya Uenezi

(d) Kamati ya Sheria na Haki za Binadamu

(e) Kamati ya CHADEMA ni Msingi

(f) Kamati ya Hamasa

(g) Kamati ya Sera, Ilani na Utafiti.

(h) Kamati ya Wagombea

(i) Kamati ya Maadili

(j) Kamati ya TEHAMA

7.6.10.1 Kila Kanda itakuwa na mamlaka ya Kuunda Kamati nyingine zaidi ya zile

zilizoainishwa baada ya kushauriana na Ofisi ya Katibu Mkuu.

7.6.10.2 Kila Kamati ya Kanda itapewa kazi/ hadidu za rejea na Ofisi ya Katibu Mkuu.

**7.7 Ngazi ya Taifa**

7.7.1 Ngazi hii itaundwa kwa eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7.7.2 Ngazi ya Taifa itaundwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Chama zilizotungwa na Baraza Kuu.

7.7.3 Viongozi Wakuu wa Ngazi ya Taifa watakuwa wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Taifa

(b) Makamu Mwenyekiti Bara

(c) Makamu Mwenyekiti Zanzibar

(d) Katibu Mkuu

(e) Naibu Katibu Mkuu Bara

(f) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

7.7.4 Kutakuwa na Kurugenzi za Utendaji Makao Makuu ya Chama zitakazoundwa na Kamati Kuu kutokana na mahitaji ya Chama.

7.7.5 Kutakuwa na kamati za hamasa ambazo utaratibu wa uundwaji wake na utendaji wa kazi utaelezwa kwenye Mwongozo utakaotungwa na Baraza Kuu.

7.7.6 Kamati Kuu inaweza kuongeza au kupunguza idadi ya Kurugenzi kadri ya mahitaji

7.7.7 Ngazi ya Taifa itakuwa na vikao kama ifuatavyo;

(a) Mkutano Mkuu wa Taifa

(b) Baraza Kuu

(c) Kamati Kuu

(d) Sekretarieti ya Kamati Kuu

7.7.8 Wajumbe wa Mkutano Mkuu watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Wajumbe wote wa Kamati Kuu

(b) Wajumbe wote wa Baraza Kuu

(c) Wenyeviti wa Wilaya/Majimbo

(d) Makatibu wote wa Majimbo/Wilaya

(e) Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wanaotokana na Chama

(f) Wajumbe ishirini watakaochaguliwa na Mikutano Mikuu ya kila Baraza la chama kuingia kwenye Mkutano Mkuu Taifa kwa kama ifuatavyo:-

(i) Wajumbe kumi na tano kutoka Tanzania Bara

(ii) Wajumbe watano kutoka Tanzania Zanzibar kwa kila baraza

(g) Mjumbe Mwakilishi wa kila Wilaya

(h) Viongozi wa Kitaifa wa Mabaraza ambao sio wajumbe wa Kamati Kuu.

7.7.9 Mkutano Mkuu Taifa utakutana mara moja katika kipindi cha miaka mitano. Mikutano Mikuu maalum / dharura inaweza kuitishwa wakati wowote ukiwepo ulazima kwa utaratibu utakaowekwa na Kanuni.

7.7.10 Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Kuchagua Mwenyekiti wa Chama Taifa na Makamu wake wawili

(b) Kujadili taarifa za Baraza Kuu na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji.

(c) Kuteua mgombea wa Urais na mgombea mwenza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mgombea Urais wa Zanzibar.

(d) Kujadili na kuridhia Itikadi, Falsafa na Sera za Chama na kuweka mikakati na miongozo ya utekelezaji.

(e) Kujadili na kuridhia programu ya Chama kwa kuzingatia mapendekezo ya Baraza Kuu.

(f) Kuzingatia na kutoa maamuzi juu ya rufaa na masuala ya kinidhamu yanayowakilishwa na Baraza kuu.

(g) Kupokea na kujadili taarifa ya Bodi ya wadhaminiwa Chama juu ya mali na rasilimali za Chama

(h) Kuidhinisha Ilani (Manifesto) ya Chama kwa uchaguzi mkuu.

(i) Kuthibitisha mapendekezo ya kuunda Tume maalum kama yalivyowalishwa na Baraza Kuu.

(j) Kujadili na kufanyia maamuzi agenda nyingine yeyote iliyoletwa kwake na Baraza Kuu.

(k) Kujadili na kuthibitisha mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba ya Chama.

7.7.11 Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Wajumbe wote wa Kamati Kuu

(b) Makamu Mwenyekiti wa Kanda

(c) Makatibu wa Kanda

(d) Watunza Hazina wa Kanda

(e) Wenyeviti wa Baraza la Uongozi, Mkoa.

(f) Makatibu wa Mkoa

(g) Wajumbe wateule wasiozidi sita watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa kwa kushauriana na Katibu Mkuu na kuidhinishwa na Baraza Kuu. Wajumbe wateule hawa watateuliwa kwa uwiano wa wajumbe wanne; wanaume na wanawake wawili.

(h) Wajumbe watano watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila Baraza la Chama, kwa uwiano wa wajumbe wanne toka Bara na mmoja toka Zanzibar kwa kila Baraza.

(i) Wenyeviti wa Wilaya za Chama

(j) Makatibu wa Wilaya za Chama

7.7.12 Kazi za Baraza Kuu:-

(a) Kupendekeza wagombea wa Urais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na kuwasilisha mapendekezo yake katika mkutano mkuu kwa uamuzi.

(b) Kupokea na kudhibitisha jina la Katibu Mkuu litakalowakilishwa na mwenyekiti taifa.

(c) Kupokea na kudhibitisha majina mawili ya manaibu Katibu Mkuu moja kutoka Tanzania Bara na moja kutoka Zanzibar yatakayowasilishwa na Mwenyekiti Taifa.

(d) Kuchagua wajumbe nane kuingia kwenye Kamati Kuu. Kwa uwiano ufuatao:-

i. Wanaume watatu na wanawake watatu kutoka Tanzania Bara na angalau mmoja awe mlemavu.

ii. Mwanaume na Mwanamke mmoja kutoka Tanzania Zanzibar.

(e) Kudhibitisha wajumbe walioteuliwa na Mwenyekiti Taifa kwa mujibu wa kifungu cha 7.7.14(q).

(f) Kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya rufaa za uchaguzi na za kinidhamu kutoka ngazi za chini.

(g) Kujadili mikakati ya uendeshaji wa shughuli za Chama kwa kipindi kati ya Mkutano Mkuu na Mkutano Mkuu na kuifanyia maamuzi.

(h) Kuthibitisha mikakati na rasilimali za kuendesha kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za Serikali hususani uchaguzi Mkuu na uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(i) Kuandaa ratiba na maelekezo ya uchaguzi wa kichama kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama

(j) Kutunga na kuzifanyia marekebisho Kanuni za Chama pamoja na miongozo mbalimbali ndani ya Chama.

(k) Kujadili taarifa za Kamati Kuu na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji.

(l) Kusimamia utendaji kazi wa Kamati Kuu.

(m) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu masuala yote ya Katiba ya Chama na mabadiliko yake.

(n) Kujadili rasimu ya Ilani (Manifesto) ya uchaguzi Mkuu na kuwasilisha mapendekezo yake kwa Mkutano Mkuu kwa maamuzi.

(o) Kuteua Wajumbe wa Bodi ya wadhamini ya Chama.

(p) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.

(q) Kuthibitisha kanuni za uendeshaji Chama na miongozo ya Mabaraza ya Vijana, Wanawake naWazee.

(r) Kupokea na kuthibitisha wajumbe wateule wa Kamati Kuu wasiozidi sita watakaoteuliwa na Mwenyekiti Taifa kwa kushauriana na Katibu Mkuu.

(s) Kuthibitisha Kanda za Chama.

7.7.13 Baraza Kuu la Taifa litakutana angalau mara moja kila mwaka. Vikao maalum/ dharura vinaweza kuitishwa kadiri itakavyolazimu kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

7.7.14 Wajumbe wa Kamati Kuu watakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti wa Taifa

(b) Makamu Mwenyekiti Bara.

(c) Makamu Mwenyekiti Zanzibar

(d) Katibu Mkuu

(e) Naibu Katibu Mkuu Bara

(f) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

(g) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayetokana na Chama

(h) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayetokana na Chama

(i) Rais wa Zanzibar anayetokana na Chama

(j) Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar anayetokana na Chama

(k) Spika wa Bunge na Spika wa Baraza la Wawakilishi watokanao na Chama.

(l) Wawakilishi watano wa Wabunge wa Bunge la Muungano.

(m) Wajumbe watatu toka Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(n) Wajumbe nane waliochaguliwa na Baraza Kuu kuingia Kamati Kuu kwa uwiano wa nusu kwa nusu wanaume na wanawake na mjumbe mmoja kutoka kila kundi atoke Zanzibar.

(o) Wawakilishi watano wa madiwani wawili wakiwa madiwani wa kawaida ambao Wenyeviti na Katibu wa umoja wa Madiwani ngazi ya Taifa na watatu watokane na Mwenyekiti, Katibu na Mnadhimu wa Umoja wa Mameya/ Wenyeviti wa Halmashauri.

(p) Wenyeviti wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee ngazi ya Taifa.

(q) Wajumbe wateule wasiozidi sita watakao teuliwa na Mwenyekiti Taifa kwa kushauriana na Katibu Mkuu na kuthibitishwa na Baraza Kuu miongoni mwao ni Mwanasheria Mkuu wa Chama, mmoja kutoka Zanzibar na angalau wawili wawe wanawake.

(r) Wenyeviti Wastaafu wa Chama ngazi ya Taifa .

(s) Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni au Waziri Mkuu atokanaye na Chama.

(t) Kiongozi wa Kambi ya Upinzani au Makamu wa Pili wa Rais kwenye Baraza la Wawakilishi atokanaye na Chama.

(u) Wenyeviti wa Kanda

(v) Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini atakuwa mjumbe asiye na kura.

(w) Wakurugenzi wa Kurugenzi za Chama watakuwa wajumbe wasio na kura.

(x) Makatibu wa Mabaraza ya Chama ngazi ya Taifa watakuwa wajumbe wasio na kura

(y) Wajumbe waliotajwa katika ibara ya 7.7.17(e) na (f) watakuwa wajumbe wasio na kura.

7.7.15 Kamati Kuu itakutana mara nne (4) kwa mwaka. Vikao maalum/dharura vinaweza kuitishwa kadri itakavyolazimu kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

7.7.16 Kazi za Kamati Kuu zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kufanya utafiti wa wagombea wa Urais na Mgombea Mwenza na kuwasilisha ripoti zake kwa Baraza Kuu

(b) Kuteua Wakurugenzi wa Makao Makuu ya Chama.

(c) Kuthibitisha Makatibu wa Kanda watakaopendekezwa na Sekretariat.

(d) Kutoa mapendekezo kwa Baraza Kuu juu ya rufaa za Uchaguzi na kinidhamu.

(e) Kuandaa na kutoa Mapendekezo kwa Baraza Kuu, Mikakati ya kuendesha

shughuli za Chama kwa kila mwaka na kwa kipindi cha miaka mitano.

(f) Kuandaa na kutoa mapendekezo kwa Baraza Kuu, Mikakati ya kupata mahitaji ya rasilimali za kuendesha kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali.

(g) Kuandaa na kutoa mapendekezo kwa Baraza kuu ratiba na maelekezo ya uchaguzi wa kichama.

(h) Kupitia na kutoa kwa Baraza Kuu mapendekezo ya haja ya kuzifanyia marekebisho au maboresho Kanuni za Chama ama Katiba ya Chama.

(i) Kujadili taarifa za Sekretarieti ya Kamati Kuu na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji.

(j) Kusimamia utendaji kazi wa Sekretarieti ya Kamati Kuu.

(k) Kufanya mapitio ya Sera za Chama na kutoa mapendekezo kwa Baraza Kuu.

(l) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Baraza Kuu na Mkutano Mkuu.

(m) Kuwa kiungo na kudumisha mahusiano mema kati ya Chama na vyama vingine vya siasa nchini, Afrika Mashariki na nchi nyingine.

(n) Kupendekeza kwa Baraza Kuu majina ya Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini.

(o) Kuteua kamati au tume za kushughulikia masuala maalum ya kichama kwa muda maalumu.

(p) Kuteua wakaguzi wa mahesabu ya Chama kwa kila mwaka

(q) Kuthibitisha uteuzi wa wagombea Uspika, Ubunge na Baraza la wawakilishi Zanzibar

(r) Kuteua wagombea wa Ubunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mabunge mengine ya kikanda.

(s) Kuteua wagombea wa Uenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Mtunza Hazina wa Kanda.

(t) Kuteua wagombea wa ujumbe wa Kamati Kuu wanaotokana na Wabunge, Mameya/Wenyeviti wa Halmashauri na umoja wa madiwani kwa mujibu wa Kanuni.

(u) Kuandaa agenda za Baraza Kuu na Mapendekezo ya agenda za Mkutano Mkuu.

(v) Kufanya uamuzi juu ya mapendekezo ya kufukuza Mwanachama.

(w) Kuandaa hoja za kupelekwa Bungeni na Wabunge wa Chama

(x) Kumwachisha ujumbe wa Kamati Kuu mjumbe mteule ambaye ataenda kinyume na Katiba, Kanuni na maadili au kushindwa kukidhi matakwa ya kuteuliwa kwake.

(y) Kusimamia utendaji kazi wa Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee.

(z) Kufanya uteuzi wa mwisho wa Madiwani wa Viti Maalum kutokana na orodha iliyopendekezwa na Baraza la Wanawake Taifa.

(aa) Kuthibitisha mapendekezo ya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti/ Makamu Mwenyekiti na Mameya/ Manaibu Meya wa Halmashauri.

(bb) Kupendekeza kwa Baraza Kuu Uundwaji wa Kanda za Chama.

7.7.17 Wajumbe wa Sekretariet ya Kamati Kuu watakuwa kama ifuatavyo;

(a) Katibu Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Sekretariat

(b) Naibu Katibu Mkuu Bara

(c) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

(d) Wakurugenzi wa Kurugenzi zote za Makao Makuu

(e) Wajumbe watano wataalam watakaoteuliwa na Mwenyekiti kwa kushauriana na Katibu Mkuu.

(f) Katibu wa Sekretariat atakaeteuliwa na Katibu Mkuu.

(g) Makatibu wa Mabaraza yote ya Chama Taifa

7.7.18 Kazi za Sekretarieti ya Kamati Kuu itakuwa kama ifuatavyo;

(a) Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji shughuli za Chama

(b) Utekelezaji wa maamuzi na maelekezoya Kamati Kuu

(c) Uandaaji wa agenda na nyaraka kwa ajili ya vikao vya Kamati Kuu, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu.

7.7.19 Kutakuwa na Kamati Maalum ya Zanzibar;

7.7.20 Wajumbe wa Kamati Maalum Zanzibar watakuwa:-

(a) Makamu Mwenyeki Zanzibar ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(b) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

(c) Wajumbe wa Kamati Kuu watokao Zanzibar.

(d) Makamu Wenyeviti wa Mabaraza Taifa kutoka Zanzibar

(e) Wenyeviti wa Kanda Zanzibar

(f) Wajumbe wa Sekretariat ya Zanzibar watakuwa wajumbe wasio na kura.

7.7.21 Kazi za Kamati Maalum Zanzibar zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Kuwasilisha mapendekezo ya masuala yote ya Zanzibar kwa Kamati Kuu kupitia kwa Sekretariat.

(b) Kupendekeza mambo ya kisera yahusuyo Zanzibar

(c) Kuteua Wakuu wa idara wa ofisi ya Makao Makuu Zanzibar.

7.7.22 Kamati Maalumu ya Zanzibar itakutana mara nne kwa mwaka. Vikao Maalumu au vya Dharura vinaweza kuitishwa kadiri itakavyolazimu kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

7.7.23 Kwa shughuli za kiutendaji Zanzibar, patakuwa na Sekretarieti ya Ofisi ya Makao Makuu yenye wajumbe wafuatao-:

(a) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar ndiye Mwenyekiti wa sekretariat ya kamati maalum Zanzibar.

(b) Wakuu wa idara zilizopo Zanzibar

(c) Katibu/Naibu katibu wa mabaraza ya chama Zanzibar.

7.7.24 Kazi za Sekretariat ya Ofisi ya Makao Makuu ya Zanzibar zitakuwa kama ifuatavyo;

(a) Utekelezaji wa kazi za kila siku za chama Zanzibar

(b) Utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Kamati Kuu yanayohusu Zanzibar

(c) Uandaaji wa agenda na nyaraka kwa ajili ya vikao vya kamati maalum Zanzibar.

## 7.8 Mabaraza ya Chama

7.8.1 Chama kitakuwa na Mabaraza ya aina tatu kuanzia kwenye ngazi ya msingi hadi Taifa. Kila Baraza litajitengenezea mwongozo wake wa utendaji na mwongozo huo utathibitishwa na Baraza Kuu la Chama kwa mujibu wa Katiba ya Chama

7.8.2 Mabaraza haya ni kama yafuatayo:-

(a) Baraza la Vijana litajumuisha vijana wote wa kike na wa kiume ambao ni wanachama wenye umri wa miaka 18 ya kuzaliwa na usiozidi miaka 35.

(b) Baraza la Wanawake linajumuisha wanachama wanawake wenye umri wa kuanzia miaka 18 ya kuzaliwa na kuendelea.

(c) Baraza la Wazee linajumuisha wana chama wenye umri usiopungua miaka 50 ya kuzaliwa.

7.8.3 Mabaraza ya Chama yataundwa kwenye ngazi zote saba za uongozi wa Chama kuanzia ngazi ya Msingi

# SURA YA NANE

Mapato ya Chama

## 8.0 MAPATO, MALI NA WADHAMINI WA CHAMA

**8.1 Mapato ya Chama yatatokana na vyanzo vifuatavyo;**

(a) Ada na viingilio vya wanachama.

(b) Michango ya hiari ya wanachama na wafuasi wa Chama

(c) Michango ya hiari ya watu au taasisi za ndani na nje ya nchi wanaounga mkono Chama. (d) Misaada na ruzuku toka ndani na nje ya nchi.

(e) Mapato yanayotokana na hisa na miradi halali ya Chama.

(f) Mapato au makusanyo ya rasilimali yatakayotokana na mifumo ya TEHAMA.

**8.2 Mali za Chama ni pamoja na**

(a) Mali zozote zenye kuondosheka na zisizo ondosheka

(b) Hisa za Chama katika miradi ya kiuchumi.

(c) Mali za Mabaraza ya Vijana, Wanawake na Wazee.

## 8.3 Wadhamini wa Chama

(a) Kutakuwa na bodi ya wadhamini wa Chama yenye wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi tisa itakayoteuliwa na Baraza Kuu.

(b) Mali zote za kudumu, vitega uchumi na dhamana zote zitawekwa chini ya jina lililosajiliwa la bodi ya wadhamini.

(c) Wajumbe wa bodi ya wadhamini watateuliwa na kuhudumu kwa kipindi cha miaka mitano tangu siku ya uteuzi.

(d) Kanuni za Chama zitabainisha taratibu za mikutano ya bodi ya wadhamini.

(e) Mwenyekiti wa bodi ya wadhamini atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe walioteuliwa na Baraza Kuu.

(f) Mkurugenzi wa Fedha na Uchumi wa Chama ndiye atakuwa Katibu wa Bodi ya Wadhamini na atalazimika kuwasilisha taarifa ya Bodi ya wadhamini kwa Katibu Mkuu.

(g) Wajumbe wa Kamati Kuu hawatateuliwa katika Bodi ya Wadhamini, isipokuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini anayeingia kwa mujibu wa ibara 7.7.14 (v) ya Katiba.

(h) Kutakuwa na Kanuni za Bodi ya wadhamini zitakazopitishwa na Kamati Kuu.

# SURA YA TISA

## 9.0 MAMBO YA JUMLA KUHUSU KATIBA NA CHAMA

Mambo ya Jumla

### 9.1 Marekebisho ya Katiba

9.1.1 Mapendekezo ya mabadiliko yoyote ya Katiba yatafanywa na Baraza Kuu la Taifa kabla ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

9.1.2 Mapendekezo yoyote ya mabadiliko ya Katiba yatafikishwa na kujadiliwa na Kamati ya Utendaji za Majimbo/Wilaya kabala ya Baraza Kuu kuandaa rasimu ya mapendekezo kwa Mkutano Mkuu.

9.1.3 Mkutano Mkuu ndiyo wenye mamlaka ya kubadili Katiba ya Chama.

9.1.4 Mapendekezo ya marekebisho ya Katiba yatafikishwa kwa Kamati za Wilaya sio chini ya siku 30 kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu unaohusika kujadili mabadiliko. Kamati za Wilaya zitatakiwa kurejesha maoni yake katika siku 21 tangu tarehe ya mapendekezo kutumwa.

## 9.2 Kanuni na Maadili ya Chama

9.2.1 Baraza kuu litatunga Kanuni za kufafanua na kuimarisha utekelezaji wa Katiba.

9.2.2 Kanuni za Chama zitatungwa kwa kuzingatia na kuhusiana na sura za Katiba ya Chama.

9.2.3 Kukitokea migongano kati ya kipengele cha Katiba na kile cha Kanuni, kipengele cha Katiba kitatawala.

9.2.4 Baraza Kuu litakuwa na uhuru wa kuzifanyia marekebisho Kanuni za Chama ili kwenda na mahitaji ya wakati.

9.2.5 Kamati Kuu itatunga maadili ya kuongoza nidhamu, utii na uwajibikaji na dhamira ya watendaji na viongozi wa Chama na wanachama kwa ujumla. Hii ni pamoja na Maadili ya Mwenendo katika vikao vya Chama.

## 9.3 Chama kuingia Mseto na Vyama Vingine

9.3.1 Chama kinaweza kuunda mseto na chama au vyama vingine vyenye madhumuni na malengo yanayofanana na Chama ili kuimarisha uwezo wa kushinda uchaguzi mkuu au wa Serikali ya mtaa kwa lengo la kuunda utawala wa pamoja.

9.3.2 Chama kinaweza kuunda ubia na vyama vingine katika kuendesha miradi ya kiuchumi ama huduma.

9.3.3 Chama kinaweza kuungana na chama ama vyama vingine kuunda Chama kipya.

9.3.4 Uamuzi kuhusu ibara ndogo ya 9.3.1 utafanywa na Kamati Kuu na ibara ndogo ya 9.3.2 utafanywa na Baraza Kuu la Taifa na kuhusu ibara ndogo ya 9.3.3 na Mkutano Mkuu.

## 9.4 Kuvunjwa kwa Chama

9.4.1 Chama kitavunjwa rasmi endapo robo tatu (3/4) ya wajumbe wote watakaohudhuria Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa ulioitishwa kwa madhumuni ya kuvunjwa kwa Chama watapitisha hoja hiyo. Mkutano huo utatangaza rasmi kuvunjwa kwa Chama na kusimamishwa kwa shughuli zote za Chama.

9.4.2 Katika tukio la kuvunjwa kwa Chama, bodi ya wadhamini wa Chama itahodhi mali hiyo kulipia madeni yote ya Chama. Endapo kutakuwa na salio lolote la mali ya Chama baada ya kulipa madeni yote, salio hilo litawasilishwa au kukabidhiwa kwa Taasisi yoyote inayoshughulikia wasiojiweza ama Chama chochote cha wasiojiweza Tanzania kwa jinsi itakavyoamuliwa na bodi ya wadhamini.

9.4.3 Katika tukio la kuvunjwa kwa Chama kwa nia ya kuungana na Chama kingine cha siasa bodi ya wadhamini wa Chama itahodhi mali yote ya Chama na kuitumia mali hiyo kulipia madeni yote ya Chama. Endapo

kutakuwa na salio lolote la mali ya Chama baada ya kulipa madeni ya Chama salio hilo litatumika kufuatana na azimio la kuvunja Chama ili kuungana na Chama kingine.

**9.5 Umoja/Kamati za Wawakilishi wa Chama Katika Vyombo vya Utawala vya Uwakilishi wa Kisiasa**

9.5.1 Kutakuwa na Kamati za Wawakilishi wa Chama katika vyombo vya uwakilishi. Vyombo hivi ni Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Jiji, Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

9.5.2 Kila Kamati itakuwa na Mwenyekiti, Katibu na Mnidhamu ambao watachaguliwa na wawakilishi wote katika chombo husika.

9.5.3 Kamati za wawakilishi zitawajibika kwa Kamati za Utendaji za ngazi husika, katika utendaji kazi wake na zitafanya kazi kwa mujibu wa Kanuni za Chama zinazozihusu.

9.5.4 Kutakuwa na vikao maalum vya Wenyeviti na Mameya wote wa Halmashauri za Serikali za Mitaa wanaotokana na Chama. Vikao hivi vitaitishwa kwa shughuli maalum na kwa maelekezo ya Kamati Kuu.

9.5.5 Kutakuwa na umoja wa wenyeviti wa Serikali za Vijiji kwa Vijijini na wenyeviti wa Mitaa kwa mijini na katika Shehiya, wanaotokana na Chama. Vikao hivi vitaitishwa kwa shughuli maalum na kwa maelekezo ya Kamati za Utendaji za

Majimbo/Wilaya.9.5.6 Kutakuwa na Umoja wa Madiwani wa CHADEMA nchini ambao utakuwa na uongozi, vikao na kuendeshwa kwa mujibu wa Kanuni zitakazotungwa na Baraza Kuu la Chama.

**9.6 Kukasimu Madaraka ya Shughuli za Utendaji**

9.6.1 Kamati ya Utendaji ya Wilaya au Kamati Kuu Taifa zinaweza kukasimia baadhi ya madaraka kwa Secretariat yake kwa azimio la wingi wa kura za wajumbe wa kikao.

9.6.2 Baraza Kuu linaweza kukasimia baadhi ya madaraka yake kwa Kamati Kuu kwa azimio la uwingi wa kura za wajumbe.

9.6.3 Mkutano Mkuu unaweza kukasimu kwa Baraza Kuu baadhi ya madaraka yake, lakini kwa azimio maalum.

9.6.4 Kila ngazi ya uongozi katika muundo wa chama inaweza kuwa na mamlaka na uhuru wa kukasimu madaraka yake isipokuwa tu, kwa majukumu yaliyozuiliwa kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

**9.7 Kuanza Kutumika kwa Katiba Hii**

9.7.1 Katiba hii itaanza kutumika baada ya kupitishwa na Mkutano Mkuu Maalum.

**Imepitishwa na:Mkutano**
**Mkuu Maalum wa tarehe**
**13 Agosti 2006.**

# KANUNI ZA CHAMA

# KANUNI ZA CHAMA

## A. UTANGULIZI

Uendeshaji wa Chama chochote cha siasa, kimsingi huongozwa na Katiba ya Chama. Lakini, Katiba hutoa tu misingi mikuu na ya jumla ya utekelezaji wa kazi za Chama. Katika kutekeleza baadhi ya vipengele vya Katiba kunahitajika Kanuni mahususi za kufuatwa ili kutekeleza na kufikia malengo ya ibara, ibara ndogo na aya za Katiba.

## B. FASILI NA UFAFANUZI

Katika Kanuni hizi maneno yafuatayo yatakuwa na maana kama ifuatavyo:-

**BARAZA KUU**
Kikao cha ngazi ya Taifa cha Utendaji cha Mkutano Mkuu Taifa.

**FALSAFA YA CHAMA**
Ina maana ya imani na mtizamo wa Chama kama ilivyoainishwa kwenye Katiba.

**ITIKADI**
Ina maana ya mwelekeo wa chama kisiasa, kiuchumi na kijamii.

**KANDA**
Ina maana ya muunganiko wa Mikoa kuunda ngazi ya Chama kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu.

**JIMBO**
Ni Jimbo la chaguzi za kiserikali kwa mujibu wa sheria za nchi.

**KAMATI KUU**
Ni kikao cha ngazi ya Taifa cha utendaji cha Baraza Kuu.

**KAMATI YA UTENDAJI**
Ina maana ya kikao cha kusimamia utendaji wa shughuli za Chama katika ngazi husika.

**KANUNI**
Ni taratibu za uendeshaji wa Chama kwa msingi wa Katiba ya Chama.

**KATIBU MKUU**
Ni Mtendaji Mkuu wa Chama.

**KURUGENZI**
Ina maana ya muundo wa utendaji zitakazoundwa na Kamati Kuu kwa kuzingatia na mahitaji ya Chama.

**MABARAZA**
Ina maana ya muundo wa makundi ya jamii kiumri na kijinsia ndani ya Chama.

**MKUTANO MKUU**
Ina maana ya kikao cha juu kuliko vyote kwenye ngazi ya chama husika.

**MWENYEKITI**
Ni kiongozi mkuu wa Chama ngazi husika.

**SEKRETARIAT**
Ni kikao cha utendaji wa shughuli za kila siku kwa ngazi husika.

**TEHAMA**
Ni teknolojia ya habari na mawasiliano.

# SURA YA KWANZA

Nembo za Chama

**1.0 Jina, Nembo, Bendera na Makao Makuu ya Chama**

1.1 Mabadiliko yoyote ya Jina, Nembo au Bendera ya Chama yatafanywa na Mkutano Mkuu wa Chama kwa kuzingatia mapendekezo ya Baraza kuu kwa mujibu wa ibara ya 9.1 ya Katiba.

1.2 Nembo ya sasa ni picha ya vidole viwili wima na vitatu vimekunjwa kuunda ishara ya herufi ‘V’ – alama ya Vema na Ushindi

1.3 Bendera ya Chama

**MUUNDO WA BENDERA:**
Bendera ya CHADEMA ina rangi nne: Nyeusi, Bluu isiyokoza (light blue), nyeupe na nyekundu.

Bendera ya CHADEMA ina nembo ya kiganja cha mkono kilichonyoosha vidole viwili katika mfumo wa V kama ishara ya USHINDI. CHADEMA ni chama kinacholenga kushinda kidemokrasia na hatimaye kuleta ushindi kwa maendeleo ya Taifa.Rangi ya BLUU ISIYOKOZA iko juu ya rangi NYEKUNDU kama ishara kwamba kama Taifa tumevushwa na mashujaa kuelekea katika jamii yenye haki, na

wakati wote CHADEMA imevuka hatua kama chama cha siasa na sasa inasimamia haki.

Rangi nyeupe iko mbele ya rangi zote kama ishara kwamba Chama kinatanguliza UKWELI NA UWAZI katika Nyanja zote. Pia rangi nyeupe imebeba nembo ya chama kwa kuwa UKWELI NA UWAZI ni misingi muhimu sana kwa chama. Nembo ya chama iko mbele kama ishara ya CHADEMA kuwa chama kiongozi katika kuchochea misingi muhimu katika kuleta mabadiliko na maendeleo katika Taifa.

Rangi zingine zinatenganishwa na ufito mweusi ambao una umbo la “T” ikiwasilisha kifupi cha jina la Taifa laTanzania.

**RANGI ZA BENDERA:**

**NYEUSI;**

Rangi hii inawakilisha WATU WA TANZANIA. Hii ni rangi ya wazawa asili wa nchi yetu. Ni rangi ambayo inabeba pia falsafa ya NGUVU YA UMMA.

**BLUU ISIYOKOZA (LIGHT BLUE)**

Hii ni rangi ya asili ya CHADEMA. Ni rangi ambayo inawakilisha HAKI. Lakini pia rangi hiyo inawakilisha BAHARI kama ishara ya maliasili/rasilimali na Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar.

**NYEUPE**

Rangi nyeupe inawakilisha UKWELI, UWAZI na AMANI. Huu ni msingi muhimu wa CHADEMA. CHADEMA ni chama ambacho kinasimamia uadilifu kwa njia ya demokrasia.

**NYEKUNDU**
Rangi nyekundu **inawakilisha** MASHUJAA **NA UKOMBOZI.** CHADEMA inathamini historia ya nchi yetu ambayo inawakilisha kumbukumbu ya mashujaa waliotupitisha katika michakato mbalimbali ya demokrasia na maendeleo ikiwemo harakati za kuondoa ukoloni. Rangi ni chimbuko la uzalendo wetu.

1.4 Kauli mbiu inayotumika sasa ni:-

| KIONGOZI | WAITIKIAJI |
|---|---|
| **Chadema** | VEMA |
| **Chadema** | Mabadiliko ya Kweli,<br>Uhuru wa Kweli |
| **People's** | POWER |

# SURA YA PILI

## 2.0 Katiba, Kanuni na Maadili

Katiba

2.1 Kanuni za Chama zinaweza kufanyiwa marekebisho na Baraza Kuu kwa kuzingatia Ibara 9.2.4 ya Katiba ya Chama.

2.2 Maadili ya Chama yanaweza kufanyiwa marekebisho na Kamati Kuu, kwa kuzingatia ibara ya 9.2.5 inayoipa Kamati Kuu mamlaka ya kuyatunga.

2.3 Kwa mujibu wa Ibara 2.2 ya Katiba Mabaraza ya Wazee, Vijana na Wanawake yatakuwa na miongozo na miongozo hiyo itakuwa chini ya Kanuni za Chama.

# SURA YA TATU

**3.0 Itikadi na Falsafa ya Chama**

Falsafa na Itikadi

3.1 Uongozi wa Chama katika ngazi zote una wajibu wa kushirikisha umma kama mtu mmoja mmoja ama vikundi au asasi zao za kijamii katika shughuli zote za Chama zinazolenga kujenga ujasiri wa kudai haki zao kwa mshikamano wa kijamii utakaowezesha hatimaye kujenga nguvu ya mamlaka ya umma.

3.2 Mbali na kueneza sera za Chama, ni wajibu wa kila ngazi ya uongozi wa Chama kuelimisha umma juu ya elimu ya uraia ili kuwawezesha wanajamii kuwa na uelewa na ufahamu wa kutosha kuhusu haki zao za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

3.3 Ni wajibu wa wawakilishi wa Chama katika vyombo vya utawala kama vile Serikali za Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata, Halmashauri za Serikali za Mitaa, Bunge na Baraza la Wawakilishi, kushirikisha jamii wanazoziwakilisha katika mambo yote muhimu yanayofanyiwa maamuzi na vyombo hivyo ili kupata maoni yao kabla ya maamuzi kufanyika ama kuwajulisha misingi iliyotumika kufikia maamuzi na athari za utekelezaji wa maamuzi hayo.

# SURA YA NNE

**4.0 Madhumuni ya Chama.** Madhu muni

4.1 Madhumuni ya Chama ndiyo dira na misingi ya kazi ya Chama kikishika utawala wa nchi. Lakini ndiyo pia vigezo vya ushawishi wa Chama kwa watawala waliopo kwa kupitia wawakilishi wa Chama walio katika vyombo vya utawala vinavyohusika na utungaji sera na usimamiaji wa utoaji huduma kwa jamii na kwa kupitia asasi za kijamii zinazojihusisha na maendeleo ya jamii.

4.2 Madhumuni ya Chama ndiyo pia yatakuwa dira na msingi wa kuandaa Ilani za Chama kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Bunge/Baraza la Wawakilishi na wa Serikali za Mitaa.

4.3 Kwa kuzingatia ibara ya 4.1 na 4.2, Madhumuni yaliyoainishwa katika Katiba ya Chama yatakuwa yanafanyiwa mapitio ya mara kwa mara kwa kuzingatia mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayotokea nchini na nje ya nchi.

4.4 Baraza Kuu ndilo lenye jukumu la kufanya mabadiliko ya madhumuni ya Chama kwa kushirikisha uongozi wa Chama ngazi ya Wilaya na Mkoa na kwa

kuzingatia maoni ya umma kupitia asasi zao za kijamii.

4.5 Ni jukumu la kila ngazi ya Chama kuwa na programu ya shughuli za chama zinazohusu jamii husika sanjari na mikakati ya utekelezaji wake. Programu hizi zilenge kutekeleza Ilani za Uchaguzi za ngazi husika pamoja na Itikadi, Falsafa, na Madhumuni ya Chama.

4.6 Kuweka utaratibu juu ya matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa shughuli za Chama kwa mujibu wa mwongozo utakaotungwa na Baraza Kuu.”

# SURA YA TANO

**5 Uanachama**

Masharti ya Uanachama

5.0 Mtu yeyote anaweza kuomba uanachama na kusajiliwa kwa kutumia mfumo wa kawaida au wa TEHAMA kwa mujibu wa Katiba ya Chama

5.1 Katika kila ngazi ya msingi na tawi kutakuwa rejista yenye orodha ya kawaida na/ au ya kidigitali ya Wanachama.

Orodha hiyo ioneshe:-

(a) Jina kamili la mwanachama

(b) Namba ya kadi yake ya uanachama na ilipotolewa

(c) Namba ya ngazi yake ya msingi

(d) Umri na jinsia yake

(e) Kiwango cha elimu ya mwanachama

(f) Shughuli zake za mapato

(g) Kituo na namba yake ya upigaji kura

(h) Namba kitambulisho cha utaifa wake

(i) Namba ya nyumba/mahali anapoishi.

(j) Namba ya simu ya mwanachama.

(k) Taarifa nyingine yoyote ya utambulisho itakayoonekana inafaa.

5.2 Mwanachama atatakiwa kuwa na kadi yake au utambulisho mwingine wa kielektroniki wakati wote atakaposhiriki kwenye vikao vya Chama vinavyomhusu kwaajili ya kuhakiki uhalali wa uanachama wake na kuwawezesha uongozi kuzikagua.

5.3 Mwanachama anayehama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine, atatakiwa kutoa taarifa kwa Katibu wa msingi anaotoka na kwa katibu wa msingi anaokwenda ili aendelee kushiriki shughuli za Chama.

5.4 Mwanachama aliyepoteza kadi ama kadi yake kuchakaa sana atapewa kadi mpya. Kadi iliyochakaa itarudishwa kwa Katibu wa ngazi yake. Mwanachama huyu atalazimika kulipia kadi mpya.

5.5 Katibu wa Tawi atatoa taarifa ya idadi ya wanachama kwa Katibu wa Kata kila baada ya miezi miwili. Naye katibu wa Kata atatoa taarifa ya idadi ya wanachama kikata kwa Katibu wa Jimbo kila baada ya miezi miwili. Katibu wa Jimbo atatoa idadi ya wanachama kiwilaya kwa Katibu wa Kanda wa Chama kila baada ya miezi sita. Tawi litatoa taarifa ya kwanza Januari ya kila mwaka kwa ngazi za Kata, Jimbo litatoa taarifa yake kila robo ya mwaka na Katibu wa Kanda atatoa taarifa kwa Katibu Mkuu kila tarehe 15 ya

mwezi Juni na Desemba ya kila mwaka.

5.6 Kila tawi litaweka kumbukumbu/orodha ya wanachama wanaokoma kuwa wanachama wa Tawi.Kumbukumbu itaonesha jina kamili la mwanachama katika rejista ya kidijitali na/ au ile ya kawaida ya Wanachama na tarehe aliyokoma kuwa Mwanachama wa Tawi.

5.7 Kiingilio cha uanachama kitalipwa na mwanachama mpya kwa kiwango kitakachokuwa kimewekwa na Kamati Kuu.

5.8 Ada ya kila mwaka italipwa na mwanachama kwa kukatwa moja kwa moja (Direct Debit) na watoa huduma (Service Providers) kwa njia ya kielektroniki au mfumo mwingine kama itakavyoamuliwa na Kamati Kuu.

5.9 Kila kadi ya mwanachama itastahili kuambatanishwa na stempu ya malipo ya mwisho au uthibitisho mwingine wowote wa malipo.

5.10 Ada ya mwaka itaishia tarehe 30 Juni bila ya kujali imelipwa lini.

5.11 Ada ya mwaka italipwa katika kipindi chote cha mwaka, yaani hakuna tarehe maalum ya ada katika mwaka.

5.12 Mgawo na mapato yatokanayo na ada na mapato mengine yatagawanywa kwa vipaumbele kama yatakavyoamuliwa na Baraza Kuu.

***Mgawo wa mapato mengine yoyote utategemea vipaumbele vyetu kama itakavyoamuliwa na Baraza kuu la chama***.

5.13 Mwanachama ambaye hajalipia kadi yake kwa muda wa mwaka mmoja hatakuwa na sifa ya kugombea uongozi; asiyelipia kwa miaka miwili atapoteza haki yake ya kupiga kura kwenye vikao vya Chama.

5.14 Matakwa ya kifungu 5.12 cha Kanuni hizi yataiwezesha Kamati Kuu kuchukua hatua za kinidhamu chini ya Ibara 5.4.4 ya Katiba

# SURA YA SITA

**6.0 Muundo, Vikao na Mawasiliano ndani ya Chama.**

Uongozi na Vikao

6.1 Pale ambapo kuna Kamati ya muda ya kuratibu shughuli za Chama kwa mujibu wa Ibara 6.1.3 ya Katiba, Kamati Kuu/Kamati ya Utendaji ngazi ya juu husika, itaweka taratibu za utendaji wa kamati hizo.

6.2 Iwapo kiongozi aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa ngazi husika hawezi kuhudhuria kikao kinachomhusu hataweza kuwakilishwa na mjumbe mwingine.

6.3 Majukumu ya kifedha ya waweka hazina yatafanywa na makatibu wa ngazi husika endapo ngazi hiyo haina nafasi ya Mweka Hazina. Mfano ngazi ya msingi hadi Kata.

6.4 Nafasi yoyote itakapokuwa wazi lazima taarifa itolewe mara moja kwa ngazi ya juu ili taratibu za uchaguzi wa kuziba pengo zifanyike kwa mujibu wa Katiba.

6.5 Taratibu zifuatazo lazima zizingatiwe katika kuchukua hatua za kinidhamu:-

6.5.1 Kwa mujibu wa Ibara 5.4.3 na 5.4.4 ya Katiba, mwanachama yeyote hatachukuliwa hatua za kinidhamu ama kuonywa ama

kuachishwa ama kufukuzwa uanachama bila kwanza:

(a) Kujulishwa makosa yake kwa maandishi na kutakiwa kutoa majibu katika muda usiopungua wiki mbili.

(b) Kupewa nafasi ya kujitetea mbele ya kikao kinachohusika.

(c) Mwanachama atajulishwa kwa maandishi uamuzi wa kikao ndani ya wiki mbili baada ya kusikilizwa.

(d) Kamati Kuu inaweza kuchukua hatua za dharura bila kuzingatia utaratibu wa kifungu (a) na (b) hapo juu kama itaona maslahi ya Chama kwa ujumla yanaweza kuathiriwa isipokuwa mwachama au kiongozi anayelalamikiwa atalazimika kuitwa kwenye kikao husika.

6.5.2 Mtu yeyote aliyepoteza uanachama wake kwa mujibu wa Ibara ya 5.4 ya Katiba atapoteza haki zake zote za uanachama na hatarudishiwa ada, zawadi au ruzuku yeyote aliyokwishaitoa kabla ya kupoteza uanachama wake.

6.5.3 Mwanachama aliyepewa adhabu na kikao kimoja cha kikatiba atakuwa na haki ya kukata rufani kwa kikao cha ngazi ya juu ya kile kilichompa adhabu.

6.5.4 Mwanachama aliyewahi kuachishwa ama kufukuzwa uanachama anaweza kuomba

kurejea kwa maandishi kupitia ngazi iliyomfukuza akieleza sababu za kutaka kurejea. Maombi yake yatachunguzwa kwenye ngazi hiyo na kutolewa maamuzi na vikao vya ngazi moja ya juu inayofuata. Aliyesimamishwa au kufukuzwa na Kamati Kuu ataweza tu kurejeshwa na Baraza Kuu. Watakaofukuzwa na Mkutano Mkuu hawatakuwa na chombo kingine chochote kitakachotengua uamuzi huo.

6.5.5 Kiongozi yeyote hatachukuliwa hatua za kinidhamu bila kwanza kupewa mashitaka kwa maandishi na mamlaka husika na kupewa nafasi ya kujibu mashitaka kwa maandishi.

6.5.6 Kiongozi mhusika, zaidi ya utetezi wa maandishi, atapewa nafasi ya kujieleza bayana mbele ya kikao cha mamlaka ya nidhamu.

6.5.7 Kiongozi aliyeadhibiwa atapewa taarifa ya misingi ya maamuzi ya mamlaka ya nidhamu ili kumwezesha kuamua kukata rufani au la.

6.5.8 Mwadhibiwa atakayeamua kukata rufani atatakiwa kufanya hivyo katika muda wa siku thelathini baada ya kuarifiwa uamuzi wa adhabu.

6.5.9 Baada ya kutoa uamuzi kikao husika kinalazimika kuandaa taarifa kamili ya mwenendo wa shauri na kuwasilisha ngazi

ya juu. Taarifa hiyo lazima ifike katika muda wa siku kumi na nne baada ya kikao cha maamuzi.

## 6.6. Ngazi za Chama

6.6.1 Ngazi zote za uongozi kuanzia msingi hadi Taifa zitaundwa kwenye maeneo yaliyoelezwa ndani ya Ibara za Katiba zifuatazo

(a) Ibara 7.1.1 – maeneo ya ngazi ya Msingi

(b) Ibara 7.2.1 – maeneo ya ngazi ya Tawi

(c) Ibara 7.3.1 – maeneo ngazi ya Kata/ Shehiya

(d) Ibara 7.4.1 – (a) ni maeneo ya ngazi ya Jimbo/Wilaya

(e) Ibara 7.4.1 – (b) ni maeneo ya ngazi ya Wilaya yenye Majimbo mengi ya uchaguzi.

(f) Ibara 7.5.1 maeneo ngazi ya Mkoa

(g) Ibara ya 7.6.1 Ngazi ya Kanda

(h) Ibara 7.7.1 maeneo ngazi ya Taifa

6.6.2 Ngazi zote za uongozi zitaendelea kuwepo pale ambapo:-

(a) Kuna wanachama hai.

(b) Kuna uongozi halali wa kikatiba

(c) Kanuni za uendeshaji ngazi husika zinazingatiwa na kufuatwa

# SURA YA SABA

**7.0 Majukumu ya Vikao na Uongozi wa Ngazi za Chama.**

Vikao na Majukumu ya Uongozi

7.1 Vikao na Mihutasari yake.

7.1.1 Kila ngazi itawasilisha katika muda wa mwezi mmoja baada ya kukaa mihutasari ya vikao vyake kwa ngazi ya juu yake, yaani Msingi kwa Tawi, Tawi kwa Kata, Kata kwa Wilaya, Wilaya kwa Mkoa, Mkoa kwa Kanda na Kanda kwa Taifa. Mihutasari inayohusika ni ile ya Secretarieti, Kamati za Utendaji, Kamati Kuu, Baraza Kuu. Kila ngazi itawasilisha ripoti zake kwa kufuata utaratibu wa vikao vyao. Kama kuna tatizo lolote, basi angalau muhtasari wa maazimio/maamuzi ya kikao vipelekwe katika muda huo kwa ngazi ya juu kwa hatua za haraka.

7.1.2 Endapo ngazi husika itashindwa kufanya kikao chochote cha kikatiba, ni lazima kwa Katibu wa ngazi hiyo kupeleka taarifa ya sababu za kutofanyika kwa kikao hicho kwa ngazi ya juu inayohusika. Baada ya kupokea taarifa hiyo ngazi ya juu lazima ichukue hatuazinazostahili ikiwa ni pamoja na kukaripia ama kutoa ushauri.

7.1.3 Barua za kuitisha vikao ziambatane na ajenda za kikao. Muhtasari wa maazimio na maamuzi ya kikao kilichopita/kilichotangulia pamoja na taarifa ya utekelezaji wa maamuzi hayo itawasilishwa wakati wa kikao.Taarifa za utekelezaji zipelekwe pia ngazi za juu zinazohusika.

7.1.4 Ngazi za juu zinapopokea mihutasari ya vikao vya ngazi za chini pamoja na taarifa za utekelezaji wa maazimio ya vikao hivyo zina wajibu wa kutoa maoni na ushauri kwa ngazi husika. Vinginevyo hapatakuwa na maana yeyote ngazi za chini kupeleka mihutasari hiyo ngazi za juu.

7.1.5 Mihutasari ya maazimio na maamuzi ya vikao vya juu pamoja na maelekezo mahususi ya utekelezaji wa maazimio ya vikao hivyo, ipelekwe ngazi za chini katika muda wa majuma mawili toka kumalizika kwa kikao husika.

## 7.2 Taratibu za Uteuzi wa Wagombea Uchaguzi wa nafasi za Uongozi wa Chama.

7.2.1 Baraza Kuu la Chama ndilo litaidhinisha ratiba ya Uchaguzi Mkuu ndani ya Chama. Ratiba itaonyesha pia tarehe za kuwasilisha na kutolewa uamuzi wa rufani toka ngazi moja kwenda nyingine.7.2.2 Ratiba ya Uchaguzi Mkuu ndani ya Chama itatolewa siyo chini ya miezi sita kabla ya uhai wa uongozi wa Kitaifa uliopo kumalizika.

7.2.3 Wagombea watajaza fomu za maombi ambazo zitatayarishwa na Kamati Kuu. Fomu hizi zitalenga kupata taarifa kamili ya mwombaji ili kuviwezesha vikao vya uteuzi kumwelewa na kumtathimini.

7.2.4 Uchaguzi wa kila ngazi moja ya chini utafanyika angalau mwezi mmoja kabla ya uchaguzi wa ngazi inayofuata isipokuwa kwa ngazi ya Msingi na Tawi itakuwa wiki moja, ngazi ya Kata hadi Wilaya itakuwa wiki mbili. Hii ni kutoa nafasi ya kusikiliza rufani na kuzitolea uamuzi kabla ya uchaguzi wa ngazi inayofuata kufanyika.

7.2.5 Kamati Kuu itaweka utaratibu wa kusaidia vikao vya uchambuzi kutoa mapendekezo kwa kuzingatia vigezo vya sifa za uongozi na hatimaye kuteua wagombea kwa mujibu wa kutimiza masharti na sifa za uongozi.

7.2.6 Vikao vya kuchuja na kuteua wagombea vitakuwa ni vile vya Kamati za Utendaji za ngazi zinazohusika pamoja na Kamati Kuu na Baraza Kuu kwa uongozi wa Kanda, Kitaifa na Mabaraza ya Chama.

7.2.7 Waombaji wote wataitwa mbele ya vikao vya uchujaji kuhojiwa na ama kutakiwa kufafanua taarifa walizozijaza katika fomu zao za maombi.

7.2.8 Vikao vya uteuzi vitatakiwa kuwafahamisha wale wote ambao hawatapendekezwa na kufahamishwa sababu za kutopendekezwa kwao.

7.2.9 Kamati ya uchujaji itawasilisha taarifa kamili ya mapendekezo kwa ngazi ya uteuzi ikionyesha maoni yao kwa kila mgombea na maelezo mengine ya msingi yaliyofanya kikao kufikia mapendekezo hayo.

7.2.10 Uteuzi wa mwisho utafanywa na Kamati ya Utendaji ya ngazi ya juu ya ile iliyofanya uchambuzi. Rufani zote lazima ziwasilishwe na kuamuliwa kabla au wakati wa uteuzi wa mwisho, ili kwenda na ratiba ya uchaguzi.

7.2.11 Majina ya walioteuliwa tu ndiyo yatawasilishwa mbele ya kikao cha uchaguzi yaani Mkutano Mkuu wa ngazi inayohusika. Kama mgombea ni mmoja tu, basi apigiwe kura za "ndio" au "hapana".

7.2.12 Idadi ya wagombea kwa kila nafasi itaongozwa tu na idadi ya waombaji waliotimiza masharti na sifa za uongozi kwa nafasi husika.

7.2.13 Wajumbe wa kikao cha uchujaji ambao ni wagombea wa ngazi husika hawatashiriki katika kujadili wagombea wenzao wa nafasihizo hizo, lakini watashiriki katika kujadili wagombea wa nafasi zingine.

7.2.14 Kikao cha ngazi ya juu kinaweza kutuma msikilizaji katika kikao cha kuchuja. Huyu atachukua kumbukumbu zozote za matukio ambazo zitasaidia kikao cha uteuzi wa mwisho katika kutekeleza majukumu yake. Pia ataruhusiwa kutumia uzoefu na

ujuzi wake kufafanua masuala ya Katiba na Kanuni ili kukiwezesha kikao husika kufanya kazi zake kwa ufanisi na kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

7.2.15 Mwanachama yeyote hataruhusiwa kugombea zaidi ya nafasi moja katika ngazi moja ya uongozi wa Chama.

7.2.16 Wanaopendekezwa kwenye nafasi za Ukurugenzi watapaswa kujaza fomu maalum zitakazotayarishwa na Makao Makuu na zote zitawasilishwa kwa Kamati Kuu itakayofanya uteuzi kwa taratibu zitakazokubaliwa na kikao.

## 7.3 Taratibu za Kusimamia Uchaguzi na Kupiga Kura.

7.3.1 Vikao vya uchaguzi vitasimamiwa na viongozi toka ngazi ya juu ya ile inayofanya uchaguzi. Kwa hiyo Tawi litasimamia Msingi, Kata itasimamia Tawi, Wilaya itasimamia Kata na Mkoa utasimamia Wilaya, Kandaitasimamia Mkoa na Taifa litasimamia Kanda. Mikutano ya Kitaifa itasimamiwa na Kamati ya wazee wastaafu wa Chama itakayoteuliwa na Kamati Kuu.

7.3.2 Katika vikao vya uchaguzi ni wajumbe halali wa kikatiba tu ndiyo wataruhusiwa kupiga kura. Wawakilishi wa wajumbe wa kikatiba kama watakuwepo, watatakiwa kutoka nje ya ukumbi wakati wa kupiga kura.

7.3.3 Upigaji kura utakuwa wa siri na karatasi maalum zitatumika kwa shughuli hiyo.

7.3.4 Uchaguzi utaanza kwa nafasi nyingine na kumalizia na nafasi ya Mwenyekiti kwa kila ngazi.

7.3.5 Msimamizi wa uchaguzi atateua watu watatu toka miongoni mwa wajumbe kuhesabu kura kwa kila nafasi inayogombewa. Kila mgombea atakuwa na haki ya kuwa na wakala wa kusimamia uhesabuji kura.

7.3.6 Kura za wagombea nafasi moja zikilingana Mwenyekiti wa kikao atakuwa na kura ya turufu ili mradi yeye asiwe mgombea.

7.3.7 Matokeo yatatangazwa baada ya uchaguzi wote kukamilika. Msimamizi ataanza na wagombea wa kura za chini na kumalizia na mshindi kwa kila nafasi. Aidha matokeo ya Mwenyekiti yatakuwa ya mwisho kutangazwa.

7.3.8 Ni mgombea tu asiyeridhika na matokeo ya uchaguzi atakayeruhusiwa kuwasilisha ngazi ya juu malalamiko ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa nafasi aliyogombea. Atatakiwa kuwa na ushahidi wa wazi unaodhihirisha kuwepo kwa vitendo vya rushwa ama ukiukwaji wa Katiba.

## 7.4 Taratibu za Uteuzi wa Wagombea Uwakilishi katika Vyombo vya Utawala.

7.4.1 Kanuni 7.2.3 na 7.2.5 za uteuzi wa wagombea nafasi za uongozi ndani ya Chama zitatumika pia katika uteuzi wa wagombea uwakilishi katika vyombo vya utawala.

7.4.2 Utaratibu wa kanuni 7.2.3, 7.2.5, 7.2.6, 7.2.7, 7.2.8 na 7.2.9 utafuatwa katika kuwachuja waombaji wa uenyekiti wa Kitongoji, Mtaa na Kijiji na wajumbe wa Kamati ya Kitongoji, Mtaa na Halmashauri ya Kijiji; waombaji wa udiwani; na waombaji wa ubunge ama ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

7.4.3 Uteuzi wa mwisho utafanywa na vikao vifuatavyo:-

(i) Wagombea uenyekiti wa Vitongoji – Kamati ya Utendaji ya Tawi.

(ii) Wagombea uenyekiti na ujumbe katika Halmashauri ya Kijiji/ Mtaa-Mkutano Mkuu wa Tawi.

(iii Wagombea Udiwani – Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

(iv) Wagombea Ubunge na Ujumbe wa Baraza laWawakilishi – Kamati Kuu.

(v) Wagombea Udiwani Viti Maalum – utafanywa na Kamati Kuu.

(vi) Kamati Kuu itatayarisha taratibu za wazi na vigezo maalum vya jinsi ya kuwapata wagombea

Viti Maalum.

7.4.5 Kamati Kuu litatoa ratiba ya uteuzi. Ratiba hiyo itatoa muda wa rufaa kusikilizwa na kuamuliwa kabla ya tarehe ya kuchukua fomu za uteuzi wa kiserikali za kugombea uchaguzi.

**7.5 Sifa za kuzingatiwa katika Kuteua Wagombea katika Uongozi wa Chama na Uwakilishi katika Vyombo vya Utawala –** Licha ya mgombea kuwa na sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi, Chama kitazingatia, sifa zifuatazo:

7.5.1 Uzoefu katika uongozi wa kisiasa: Mwombaji anahitajika kuwa na historia nzuri ya uongozi wa kisiasa katika Chama ama vyama vingine vya siasa na anatakiwa kuwa mwenye mahusiano mazuri na viongozi wengine na jamii kwa ujumla.

7.5.2 Uadilifu wa mwombaji katika uongozi wa nyuma kisiasa na katika uongozi wa asasi za kijamii ama utumishi na uongozi wa kiutawala serikalini aliowahi kuwa nao.

7.5.3 Uwezo na ujuzi wa kumwezesha kuwa na ubunifu katika kutekeleza na kusimamia shughuli za uongozi/wadhifa wa ngazi anayoomba.

7.5.4 Uwezo wa kushirikisha na kushirikiana na wengine katika kutekeleza majukumu yake, ili kufanikisha eneo lake la uongozi kwa ufanisi wa hali ya juu.

7.5.5 Ufahamu na uelewa wake kuhusu Madhumuni, Itikadi na Falsafa ya Chama.

7.5.6 Uelewa na ufahamu wake kuhusu maadili na sifa za uongozi kama zilivyoainishwa na Chama.

7.5.7 Muombaji yeyote anatakiwa awe ni mwanachama wa msingi au tawi la chama katika eneo anamoishi au anakotoka.

7.5.8 Muombaji yeyote ni lazima ajue kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza.

**7.6 Majukumu ya Viongozi Wakuu wa Chama**

7.6.1 Wenyeviti

(i) Kuongoza vikao vya Mikutano Mikuu, Mabaraza ya Mashauriano na Uongozi, Kamati za Utendaji/Kamati Kuu na Baraza Kuu kwa ngazi husika.

(ii) Kuhakikisha mihutasari ya vikao na maamuzi muhimu ya vikao hivyo inaandikwa na kusambazwa kwa eneo husika katika muda usiozidi siku kumi na nne baada ya vikao na kuwa yeye binafsi anapata nakala yake.

(iii) Kuwa msemaji mkuu wa masuala ya Chama kwa ngazi yake baada ya kushauriana na Katibu Mkuu/Katibu, Kamati ya Utendaji/Kamati Kuu ama Sekretarieti ya ngazi husika.

(iv) Kuwakilisha Chama katika shughuli za kiserikali katika eneo lake kwa kadri Chama kinavyohusishwa.

(v) Kusimamia na kuratibu utendaji kazi za Chama katika eneo lake

(vi) Kueneza sera na misimamo ya Chama ndani ya jamii ya eneo lake kwa njia ya mikutano ya hadhara kwa kushirikisha viongozi wengine wa ngazi yake ama ngazi za chini au juu.

7.6.2 Makamu Wenyeviti

(i) Ni wasaidizi wakuu wa wenyeviti wa ngazi zao.

(ii) Kumwakilisha Mwenyekiti Katika shughuliza kiserilkali kwa maagizo ya Mwenyekiti au Mwenyekiti anapokuwa na udhuru nje ya eneo lake.

(iii) Ni Wenyeviti wa Kamati za Maadili kwa ngazi ya Kanda na Taifa.

(iii) Na majukumu mengine kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na Miongozo ya Chama.

7.6.3 Makatibu wa Chama kwa ngazi zao:-

(i) Ni wasimamizi wakuu wa rasilimali, utawala na uendeshaji wa Chama.

(ii) Ni wenyeviti wa Sekretarieti za ngazi zao.

(iii) Ni wawajibikaji wakuu wa utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya vikao vya ngazi zao na vikao vya Juu

(iv) Ni wasimamizi na wawajibikaji wakuu wa uandikaji wa mihutasari ya vikao na taarifa za mwaka na za utendaji/ shughuli za Chama katika ngazi zao.

(v) Ni waratibu na wafuatiliaji wakuu wa utendaji kazi wa makatibu wa ngazi za chini yao.

(vi) Wanawajibika kwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa ngazi zao katika utendaji kazi wao wa kila siku. Hivyo wanatakiwa kuwa na Mashauriano ya karibu na Wenyeviti wao.

7.6.4 Manaibu Katibu Mkuu

(i) Ni wasaidizi wakuu wa Katibu Mkuu

(ii) Ni waandishi wa kumbukumbu za vikao vya ngazi ya Taifa.

(iii) Kwa upande wa Naibu Katibu Mkuu Zanzibar majukumu yake ni kama yalivyoainishwa kwenye ibara ya 7.7.23 ya Katiba.

7.6.5 Makatibu Waenezi

(i) Ni watendaji na wahamasishaji wakuu wa Chama katika shughuli za uenezi wa sera za Chama na ilani za uchaguzi.

(ii) Ni waagizaji wasimamiaji wa uchapishaji na usambazaji wa vifaa vya uenezi wa Chama na uchaguzi. Hii ni pamoja na kadi, sera, ilani, bendera na machapisho mengine ya uenezi na uchaguzi.

(iii) Kubuni mikakati ya uhamasishaji jamii kwa kushirikiana na waratibu wa vijana na wanawake.

(iv) Ni watoaji wa habari na maoni ya Chama kwa vyombo vya habari na kwa jamii. Hii ni pamoja na maamuzi maalum ya vikao vikuu vya Chama kwa kila ngazi husika kwa maelekezo ya Wenyeviti na Makatibu.

(v) Ni wasimamiaji wa mikutano na vyama vingine vya siasa kwa kuzingatia msimamo na maelekezo ya vikao vikuu vya Chama ngazi inayohusika.

(vi) Kubuni na kuratibu mafunzo ya shughuli za uenezi wa Chama kwa makatibu wenezi, waratibu wa vijana na wanawake wa ngazi ya chini.

(vii) Kusimamia na kuratibu kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za serikali kwa eneo la ngazi yake.

(viii) Kubuni na kuchapisha mabango na makala zingine za uenezi wa Chama au kwa ajili ya kampeni za uchaguzi wa kiserikali.

7.6.6 Waweka Hazina

Kusimamia mali na fedha za Chama kwa kuzingatia kanuni za fedha na maamuzi ya vikao.

(i) Kubuni mikakati ya kukiwezesha Chama kupata rasilimali za kuendesha kazi zake kwa ufanisi.

(ii) Kubuni miradi ya kushirikisha vikundi vya vijana na vya wanawake wa

Chama kujipatia mapato ya kuchangia Chama.

(iii) Kuandaa taarifa za kila mwaka za mali na mahesabu ya mapato na matumizi na kuzituma ngazi husika kwa kuzingatia kanuni za fedha za Chama.

7.6.7 Majukumu ya viongozi wa Mabaraza ya Chama.

7.6.8 Wenyeviti wa Mabaraza ya Chama:-

(a) Kuongoza vikao vya Baraza la chama husika

(b) Kuhakikisha mihutasari ya vikao na maamuzi muhimu ya vikao hivyo inaandikwa na kusambazwa kwa eneo husika katika muda usiozidi siku kumi na nne baada ya vikao na kuwa yeye binafsi anapata nakala yake.

(c) Kuwa msemaji mkuu wa masuala ya Baraza husika kwenye ngazi yake.

(d) Kuwakilisha Baraza husika kwa kadri inavyohitajika

(e) Kuhamasisha jamii inayohusu Baraza lake katika maeneo yake kukipenda, kukienzi na kujiunga na Chama

(f) Kuhamasisha jamii inayohusu Baraza lake kushiriki kugombea uongozi wa chaguzi za chama na za kiserikali

7.6.9 Makatibu wa Mabaraza ya Chama:-

(a) Watakuwa watendaji wakuu wa shughuli za Baraza husika

(b) Kuwa Mwenyekiti wa Sekretariet ya Baraza katika ngazi yake.

(c) Watatakiwa kubuni na kutekeleza mikakati ya kujenga vikundi vya kiuchumi/kitamaduni n.k. kwenye tabaka la jamii linalowahusu.

(d) Kuunda, kukuza na kusimamia vikundi vya jamii husika kufanikisha chaguzi za Chama na za kiserekali ili Chama kipate uongozi imara.

(e) Kubuni mbinu mbalimbali za kuunda timu za uhamasishaji na uenezi wa sera za chama kwa kundi la jamii husika.

(f) Kutunza kumbukumbu na nyaraka za Baraza.

7.6.10 Kwa madhumuni ya utekelezaji wa Ibara ya 6.3.4 (c) ya Katiba, Kiongozi yeyote wa Chama atahesabika kuwa ameshindwa kutimiza wajibu wake ikiwa atashindwa kutekeleza mambo yafuatayo-:

a) Kushindwa kuitisha vikao vya kikatiba, kwenye ngazi husika.

b) Kushindwa kusimamia mapato na matumizi katika ngazi husika.

c) Kushindwa kutoa taarifa zitakazohitajika na ngazi ya juu.

d) Kushindwa kuhudhuria vikao vya kikatiba bila sababu mahususi.

e) Kuwa chanzo cha mgogoro ndani ya Chama.

f) Kutoa taarifa zisizokuwa za kweli kuhusu Chama.

g) Kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Kanuni za 7.6.1, 7.6.2, 7.6.3, 7.6.7, 7.6.5, 7.6.6, 7.6.7, 7.6.8 na 7.6.9.

7.6.11 Hatua za kinidhamu kama zilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 6.5.2 ya Kanuni hizi zitafuatwa wakati wa utekelezaji wa Kanuni ya 7.6.10.

## 7.7 Uendeshaji wa Ofisi

7.7.1 Kuwepo na Ofisi na Ulipaji wa Pango.

7.7.1.1 Ofisi ni kielelezo cha msingi cha uhai wa Chama. Kwa hiyo kila ngazi ya Chama inatakiwa kuwa na Ofisi ya Chama iliyojengwa na kumilikiwa na Chama au ya kukodi.

7.7.1.2 Viongozi kwa kushirikiana na wanachama wanao wajibu wa kutafuta rasilimali au kuchangia vifaa vya ujenzi wa ofisi za Chama.

7.7.1.3 Ngazi zote za Chama zina wajibu wa kutafuta viwanja na kuanza ujenzi wa ofisi za Chama.

7.7.1.4 Wajibu wa kulipia pango la ofisi kwa ngazi zote litakuwa la ngazi husika.

7.7.2 Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka Kila ofisi itatakiwa kuwa na majalada maalumu ya kutunza kumbukumbu na nyaraka.

7.7.2.1 Makao Makuu ya Chama

(a) Majalada tofauti kwa ajili ya mikutano mikuu, vikao vya Baraza Kuu, vikao vya Kamati Kuu na vikao vya Sekretariati.

(b) Majalada kwa kila Mkoa kwa ajili ya kuhifadhi mihutasari ya mikutano mikuu na vikao vya Kamati za Utendaji za Mkoa na mawasiliano mengine.

(c) Jalada moja kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Bunge na Baraza la Wawakilishi.

(d) Jalada moja kuhusu Uchaguzi wa Madiwani na ngazi za chini.

(e) Jalada moja kuhusu uchaguzi ndani ya Chama.

(f) Jalada moja kwa ajili ya mawasiliano na Msajili wa Vyama vya Siasa.

(g) Jalada moja la mawasiliano na vyama vingine vya siasa.

(h) Jalada moja la mawasiliano na Serikali na Wizara au Idara zake.

(i) Jalada moja la mawasiliano na Taasisi mbalimbali za ndani ya nchi.

(j) Jalada moja la mawasiliano na wahisani wa ndani na nje.

(k) Jalada moja la Bodi ya Wadhamini.

(l) Jalada moja la Kamati ya Wabunge wa Chama.

(m) Jalada moja la Umoja wa Madiwani.

(n) Jalada moja kuhusu masuala ya kinidhamu

(o) Jalada kwa kila Kurugenzi ya Chama.

(p) Jalada moja kuhusu masuala ya Baraza la vijana

(q) Jalada moja kuhusu masuala ya Baraza la Wanawake.

(r) Jalada moja kuhusu masuala ya Baraza la wazee.

(s) Jalada moja kwa kila Kanda

(t) Majalada ya nyaraka za siri za Chama kama itakavyoamuliwa na Katibu Mkuu baada ya kushauriana na Sektetarieti.

7.7.2.2 Ofisi za Kanda

(a) Majalada tofauti kwa ajili ya mikutano ya Mabaraza ya Uongozi, Kamati ya Utendaji na Sekretariat.

(b) Jalada la Umoja wa Madiwani

(c) Jalada la Wabunge wanaotoka katika Kanda husika

(d) Jalada la Ofisi ya Katibu Mkuu

(e) Jalada moja kwa kila Kamati za Kanda

(f) Jalada moja la masuala ya nidhamu

(g) Majalada mengine kadri itakavyo elekezwa na Katibu Mkuu.

7.7.2.3 Ofisi za Mikoa/Wilaya

(a) Majalada tofauti kwa ajili ya mikutano mikuu, Kamati ya Utendaji na Sekretariat ngazi ya Wilaya na Baraza la Uongozi la Mkoa.

(b) Majalada kwa kila Kata na Matawi yake na Wilaya na Kata zake.

(c) Majalada ya mawasiliano na Makao Makuu.

(d) Jalada kuhusu uchaguzi mkuu wa Rais na Bunge.

(e) Jalada kuhusu uchaguzi ndani ya Chama.

(f) Jalada kuhusu uchaguzi wa Madiwani.

(g) Jalada kuhusu uchaguzi wa Vitongoji, Mitaa na Vijiji.

(h) Jalada kuhusu mawasiliano na vyama vingine vya siasa Wilayani au Mkoani.

(i) Jalada kuhusu mawasiliano na serikali Wilayani na Serikali Wilayani (ofisi ya Mkuu wa Wilaya) na Halmashauri au na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

(j) Jalada la mawasiliano na Taasisi za kijamii ndani na nje ya Wilaya au Mkoa.

(k) Jalada la Kamati za Madiwani na Wabunge/Wawakilishi.

(l) Jalada la masuala ya Baraza la Vijana.

(m) Jalada la masuala ya Baraza la Wanawake.

(n) Jalada la masuala ya uchumi na miradi.

(o) Jalada la masuala ya jumla.

(p) Jalada la masuala ya Baraza la Wazee

7.7.2.4 Ofisi za Kata

(a) Jalada moja kwa kila vikao vya Mkutan Mkuu na vyama Kamati ya Utendaji.

(b) Jalada moja la mawasiliano ya jumla na Wilaya.

(c) Jalada moja la mawasiliano na Matawi.

(d) Jalada moja la masuala ya Wanawake.

(e) Jalada moja la uchaguzi wa Rais, Bunge na Udiwani.

(f) Jalada moja la uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa.

(g) Jalada moja la mawasiliano ya kiserikali ngazi ya Kata.

(h) Jalada moja la mawasiliano na vyama vingine kwenye Kata.

(i) Jalada moja kuhusu shughuli za uchaguzi ndani ya Chama.

(j) Jalada moja la masuala ya Baraza la Vijana.

(k) Jalada moja kuhusu masuala ya Baraza la Wanawake.

(l) Jalada moja kuhusu masuala ya Baraza la Wazee.

7.7.2.5 Ofisi za Matawi

(a) Jalada moja kwa kila vikao vya mikutano mikuu na vya Kamati za Utendaji.

(b) Jalada moja la Mawasiliano na Kata na Wilaya.

(c) Jalada moja la mawasiliano na Misingi.

(d) Jalada moja la masuala ya Baraza la Vijana.

(e) Jalada moja la masuala ya Baraza la Wanawake.

(f) Jalada moja kuhusu shughuli za uchaguzi wa kiserikali.

(g) Jalada moja kuhusu shughuli za uchaguzi ndani ya Chama.

(h) Jalada moja la mawasiliano na vyama vingine.

(i) Jalada moja kwa masuala ya baraza la Wazee.

7.7.3 Utendaji Maofisini

Kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Chama haitawezekana kuwa na watendaji wa ngazi zote kuanzia msingi hadi mkoa,ama kuwa na viongozi watendaji wa kulipwa kwa kila ngazi na kila kada ya watumishi na utendaji.

Kwa hiyo:

7.7.3.1 Viongozi wa kila ngazi wapangiane zamu za kuwa ofisini na kuwe na ratiba za kila juma au mwezi.

7.7.3.2 Bila ya kuathiri 7.7.3.1 ya kanuni hizi, ngazi za Wilaya na Mkoa ziwe angalau na mtu mmoja wa kudumu wa kufungua na Kufunga ofisi akiwa ndio karani wa ofisi.

7.7.3.3 Vikao vya kikatiba viwe na ratiba ambazo kila mjumbe mhusika anapewa.

7.7.34 Mawasiliano yoyote kwenda nje ya ofisi yawe na nambari ya kumbukumbu ya jalada husika na kubaki na nakala katika jalada husika.

7.7.3.5 Barua au nyaraka zote zinazopokelewa ziingizwe mara moja katika jalada husika baada ya kugongwa muhuri wa ofisi kuandikwa tarehe ya kupokelewa. Barua/ waraka upelekwe kwa kiongozi mhusika katika jalada.

# SURA YA NANE

## 8.0 Mapato, Mali na Wadhamini wa Chama

Mali za Chama

8.1 Ni jukumu la Bodi ya Wadhamini kupitia kwa Katibu Mkuu kusimamia masuala yote ya mapato na matumizi ya fedha za Chama, pamoja na mali zote za Chama kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Chama na kuwa kanuni hizo zitatumika kikamilifu.

8.2 Mwaka wa fedha wa Chama utakuwa tarehe 01 Julai hadi tarehe 30 Juni mwaka unaofuata.

8.3 Ni wajibu wa msingi wa Kamati za Utendaji za Matawi kusimamia ulipaji wa ada za kila mwaka na hiki kitakuwa ni moja ya vipimo vya utendaji kazi kwa kamati hizo.

8.4 Ni wajibu wa msingi wa Kamati za Utendaji za Kata na Wilaya kufuatilia na kuhakikisha kuwa mgawanyo wa makusanyo ya ada na viingilio unazingatiwa.

8.5 Michango yoyote ya hiari kutoka kwa wanachama itapangwa na kuidhinishwa na Kamati za Utendajiza kila ngazi kwa mahitaji ya kila ngazi na Katibu mkuu kwa shughuli za Kitaifa.8.6 Michango yoyote ya wapenzi na wahisani wa Chama itakusanywa na viongozi walioteuliwa mahsusi kwa kazi hiyo.

8.7 Stakabadhi ya malipo juu ya michango yote ya kikanuni ya Wabunge na Madiwani katika ngazi ya Jimbo/Wilaya na Taifa itatolewa baada ya kupokelewa.

**8.8 VIKAO VYA BODI YA WADHAMINI**

8.8.1 Bodi ya wadhamini itakutana mara nne (4) kwa mwaka

8.8.2 Akidi ya kikao cha bodi ya wadhamini itakuwa nusu ya wajumbe walioteuliwa na mamlaka husika.

8.8.3 Ikiwa Mwenyekiti hayupo, wajumbe wa kikao watamchagua Mwenyekiti wa Kikao miongoni mwao.

8.8.4 Katibu wa Kikao atakuwa ni Mkurugenzi anayehusika na masuala ya Fedha na Utawala wa Chama

8.8.5 Bodi ya Wadhamini inaweza kukutana kwa dharura wakati wowote inapohitajika.

# SURA YA TISA

**9.0 Mambo ya Jumla Kuhusu Katiba na Chama.**

Mambo ya Jumla

9.1 Chama kuingia mseto/ushirika kwa ajili ya uchaguzi na Chama ama vyama vingine kutaweza kutekelezwa kitaifa ama katika eneo moja la kiutawala kama vile Kijiji, Kata, Wilaya au mamlaka moja ya serikali za Mitaa.

9.2 Kwa madhumuni ya utekelezaji wa Kanuni 9.1 katika ngazi ya Wilaya uamuzi wa kufanya hivyo utafanywa na Kamati ya Utendaji ya Wilaya. Kwa uchaguzi wa Mbunge, uamuzi wa mwisho utafanywa na Makao Makuu kutokana na mapendekezo ya Wilaya.

9.3 Ushirika na vyama vingine wa kuendesha shughuli za kiuchumi utafanywa kwa uhuru na kila ngazi ya uongozi wa Chama na Kamati Kuu au Kamati ya Utendaji ya kila ngazi ndiyo itatoa maamuzi. Kwa shughuli za kiuchumi, neno Chama ni pamoja na vyama huru vya kijamii.

9.4 Katika hatua ya kuvunja Chama kwa sababu yoyote ile Baraza Kuu litahitaji kujulisha sababu na kupata maoni ya Kamati zote za Utendaji za Wilaya na Mikoa kabla ya kuandaa rasimu ya kupeleka katika Mkutano Mkuu wa Taifa.9.5 Vikao vya Kamati za

wawakilishi wa Chama katika vyombo vya utawala, kama vilivyoainishwa katika Ibara ya 9.5 ya Sura ya Tisa ya Katiba, vinalenga kuwajengea wawakilishi hao uelewa, ufahamu na mitazamo ya aina moja ya kichama katika uwakilishi wa wananchi katika vyombo vya ngazi moja.

9.6 Vikao vya Kamati za Wawakilishi hawa wa Chama vitajitungia Kanuni zake ambazo zitahitaji kuthibitishwa na Kamati za Utendaji za Wilaya kwa wawakilishi katika serikali za Mitaa na Kamati Kuu kwa Wabunge/Wawakilishi kabla ya kuanza kutumika. Kamati hizi zitafanya kazi kama Kamati Ndogo za Kamati za Utendaji/Kamati Kuu za ngazi husika.

9.7 Katika kuandaa Ilani ya Uchaguzi, Ilani ya masuala ya Kitaifa itaandaliwa na Baraza Kuu na kupitishwa na Mkutano Mkuu na Ilani zinazolenga mambo mahsusi ya kila Jimbo la uchaguzi au eneo la mamlaka moja ya Serikali za Mitaa ambamo Chama kitakuwa na wagombea itaandaliwa na Kamati ya Utendaji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa ngazi husika.

# SURA YA KUMI

## 10.0 Maadili ya Viongozi, Sifa Mahususi za Viongozi na Maadili ya Wanachama

Maadili ndani ya Chama

## 10.1 Maadili ya Viongozi

(i) Kila kiongozi anatakiwa kuwa na tabia ambayo ni mfano wa kuigwa na wanachama na jamii kwa ujumla.

(ii) Kila kiongozi anategemewa kutimiza wajibu wa ngazi yake ya uongozi kama inavyoelezwa kwenye Kanuni za Chama. Ili aweze kufanya hivyo atawajibika kujiendeleza na kujielemisha kisiasa na kijamii kwa kiwango kitakachomwezesha kutimiza wajibu huo kwa umahiri na ufanisi.

(iii) Kila kiongozi anatakiwa kulinda siri zote za Chama.

(iv) Kiongozi yeyote asijihusishe na vikundi vyenye misingi ya ukabila, udini, au ukanda ambavyo vina makusudi ya kubaguana ndani ya Chama au miongoni mwa jamii kisiasa au kijamii.

(v) Kiongozi asitumie wadhifa wake kwa kujinufaisha ama kwa kuajiri, kutoa tuzo au kandarasi kwa misingi ya upendeleo.Hii ni pamoja na uteuzi wa wagombea wa uongozi ndani ya Chama au katika chaguzi za kiserikali.

(vi) Kiongozi anatarajiwa kujitosheleza yeye na familia yake kwa mapato halali na kuepukana

na tabia ya kukopa kwa kuzidi uwezo wake au kuwa ombaomba kwani tabia hiyo itadhoofisha uwezo wake wa kutoa maamuzi sahihi yasiyo na upendeleo au yanayoegemea kwa wanaompa fadhila. Hivyo ni wajibu na jukumu la kila kiongozi kuwa na shughuli halali mahsusi za kumwingizia pato la kujitosheleza kimaisha.

(vii) Kiongozi anatakiwa kulinda mali zote za Chama kwenye ngazi yake na kusimamia matumizi ya mali za Chama kwa faida ya Chama na wanachama wake. Ni mwiko kwa kiongozi yeyote kutumia mali za Chama kwa maslahi binafsi.

(viii) Kiongozi anatakiwa kuwa mkweli na muwazi wakati wote hususani katika vikao halali na aachane na vikundi vya majungu na wadanganyifu. Ni mwiko kwa kiongozi kujihusisha na upotoshaji wa maamuzi halali ya vikao vya Chama.

(ix) Kiongozi asijihusishe au kushiriki na vikundi au vitendo vya kuchonganisha au kuzua migogoro ndani ya uongozi wa Chama au wanachama wake.

(x) Kiongozi asitoe tuhuma zozote juu ya viongozi wenzake pasipo kupitia vikao halalina kuzingatia taratibu na ngazi zilizoelezwa kwenye kanuni za Chama.

(xi) Kiongozi anatakiwa kutii na kutimiza maagizo anayopewa na viongozi wa ngazi ya juu au vikao halali na kama hakubaliani na maagizo hayo aeleze hivyo kwa kupitia taratibu na ngazi zilizowekwa kwenye kanuni.

(xii) Itakuwa marufuku kwa kiongozi wa CHADEMA kukashifu Chama, kiongozi au mwanachama yeyote wa Chama au vyama vingine, au

viongozi wa kiserikali. Ni muhimu viongozi wa CHADEMA waelewe tofauti ya kashfa na ukosoaji wa kisiasa.

(xiii) Kiongozi asiwe na uhusiano na vikundi katika jamii vyenye tabia zitakazompunguzia heshima kiongozi ndani ya jamii. Kwa mfano; kijana kiongozi wa CHADEMA hategemewi kushiriki katika magenge ya watumiaji wa madawa ya kulevya, n.k.

(xiv) Kiongozi asihusishe masuala ya familia yake na taratibu za uongozi ndani ya Chama. Hivyo basi itakuwa marufuku kwa wenza wa viongozi (wake kwa waume) kushinikiza/ kuagiza/ kushiriki maamuzi ya vikao halali vya Chama labda tu pale watakapokuwa ni viongozi wa kuchaguliwa/kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na Miongozo ya Chama. Na kwa malengo ya kanuni hii neno "Kiongozi" lina maana ya kiongozi yeyote wa Chama.(xv) Viongozi wa kuchaguliwa wanaotokana na Chama kwa ngazi zote watatakiwa kuzingatia maadili ya viongozi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

**10.2 Sifa Mahsusi za kila Kiongozi wa Chama Pamoja na maadili ya jumla na sifa zilizoainishwa katika kanuni za Chama, kila kiongozi anatarajiwa:**

(i) Awe na historia ya uadilifu na kukubalika katika jamii. Hii inamaanisha kuwa amekuwa mwanachama kwa muda wa kutosha kujijengea historia hiyo au tayari anayo sifa hiyo ndani ya jamii.

(ii) Awe na uzoefu katika masuala ya uongozi wa jumuiya katika nyanja za kisiasa au kwenye utumishi wa umma au taasisi mbalimbali.

(iii) Aonyeshe kwa tabia na mwenendo uzalendo wa kupenda nchi yake na kutetea nchi yake. (iv) Adhihirishe mapenzi yake na imani yake kwa Chama na wanachama kwa juhudi na vitendo vyake vya kuendeleza na kukuza Chama na wanachama wake.

(v) Awe na msimamo wa kuaminika.

(vi) Awe na kipaji cha ubunifu, uwajibikaji na uadilifu kwani vyote hivi ni muhimu kwa kiongozi bora na mahiri.

(vii) Aonyeshe uzoefu wa kuwa tayari kushirikiana na viongozi wenzake na uzoefu wa kufanya kazi na vikundi mbalimbali ndani ya jamii.

(viii) Kuwa na njia halali za mapato yake ya kujitosheleza kwani uongozi wa Chama ni wa msingi wa kujitolea.

(ix) Adhihirishe kuwa ana nidhamu na utii kwa kutekeleza maagizo au maelekezo ya vikao vya Chama na viongozi wa Chama.

(x) Akubali kukosoa na kukosolewa au kuelekeza na kuelekezwa na awe tayari kujirekebisha.

(xi) Kila kiongozi mwenye wadhifa wa Mwenyekiti, Katibu na Katibu Mwenezi kuanzia ngazi ya Kata hadi Kanda na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Wabunge na Madiwani watatakiwa kuwa na Msingi hai wa Chama aliojisajili na anaoulea.

## 10.3 Maadili ya Wanachama

Pamoja na sifa, haki na wajibu wa mwanachama kwa mujibu wa sura ya Tano ya Katiba ya Chama, kila mwanachama anatakiwa awe na tabia ambayo ni mfano wa kuigwa na jamii na ya kukiwezesha

Chama kukubalika kwa jamii anamoishi huyo mwananchama. Kwa hiyo kila mwanachama anatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kuwa mkweli kuhusu uanachama wake kwa kutokuwa na uanachama wa Chama kingine cha siasa.

(ii) Kupiga kura za haki anaposhiriki katika kuchagua viongozi wa Chama ama kuteua wagombea wa chama kwa chaguzi za kiserikali.

(iii) Kuwa shupavu na mwanaharakati wa kweli katika kutetea maslahi ya Chama na jamii kwa ujumla kwa kuzingatia Madhumuni, Itikadi na Falsafa ya Chama.

(iv) Kujiepusha na upinzani dhidi ya Chama na wagombea wake na makundi ya majungu ya kugonganisha viongozi na wanachama hasa wakati wa chaguzi za kichama ama za kiserikali.

(v) Kuwa mstari wa mbele kuunga mkono wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali na kutafuta wapiga kura wa kuunga mkono mgombea huyo wa Chama.

(vi) Kusimamia kura za wagombea wa Chama wakati wa chaguzi za kiserikali.

(vii) Kuwa mwepesi wa kujitolea kufanya kazi za Chama bila ya malipo na katika kuchangia Chama kwa kulingana na uwezo wake wa kiuchumi.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## 11.0 MAMLAKA YA MAKAO MAKUU KUTOA MIONGOZO

Miongozo ya Makao Makuu

11.1 Kwa madhumuni ya kuboresha utendaji ndani ya Chama, Makao Makuu yatakuwa na mamlaka ya kutoa miongozo na ufafanuzi kwa ajili ya kufanikisha matumizi ya Kanuni hizi.

# SURA YA KUMI NA MBILI

Itifaki

## 12.0 ITIFAKI NDANI YA CHAMA

### 12.1. Umuhimu wa Itifaki:-

Itifaki (protocol) ya Chama ni utaratibu ambao ni sehemu ya Kanuni zilizokubalika na kutumika katika shughuli au sherehe zilizo rasmi za Chama katika ngazi zote. Itifaki inahusisha nani atafanya nini, wakati gani na kabla au baada ya nani, lugha inayokubalika kutumika, mtiririko wa vyeo na heshima ya kila cheo, mavazi yanayofaa kutumika na mengine mengi yanayoweza kuwekwa kwenye itifaki inayokubaliwa na Chama kwa matumizi ya kichama. Hali kadhalika, itifaki inajengeka kutokana na utamaduni unaokubalika na Chama. Kwa mantiki hii, itifaki ya Chama itatofautisha CHADEMA na vyama vingine, kwa kuwa ngazi zote za Chama, kuanzia Msingi hadi Mkutano Mkuu zitaendeshwa kwa itifaki moja iliyokubaliwa na Chama.

### 12.2 Itifaki na Ngazi za Uongozi

Itifaki ni lazima ifuatane na wajibu na majukumu waliyonayo viongozi wa ngazi mbalimbali. Ngazi mbalimbali za uongozi zinapishana kwa ukubwa na vyeo, vile vile vinapishana kwa ukubwa kutokanana

ngazi za uongozi huo. Mwenyekiti wa Mkoa hawezi kuwa sawa na Mwenyekiti wa Wilaya (aliye chini yake) au Mwenyekiti Taifa (aliye ngazi ya juu yake). Hivyo basi, itifaki imepangwa kufuatana na ngazi mbalimbali za uongozi ndani ya Chama. Kutokana na hii patakuwa na wakuu wa itifaki ndani ya CHADEMA.

**12.3 Kitaifa**

Katika ngazi ya kitaifa, vikao vyote vya Taifa ambavyo ni Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati Kuu; Mkuu wa Itifaki atakuwa Naibu Katibu Mkuu (Bara) ambaye kwa asili yake anakaa Makao Makuu ya Chama. Mkurugenzi wa Uenezi na Habari atakuwa Naibu wake. Wakati wa mikutano ya hadhara ambayo viongozi wa kitaifa wanashiriki na wakuu wa itifaki wa kitaifa hawapo, mikutano hiyo itasimamiwa na wakuu wa itifaki wa ngazi inayofuata.

**12.4 Kanda**

Katika ngazi ya Kanda mkuu wa Itifaki atakuwa Katibu wa Kanda.

**12.5 Mkoa**

Katika ngazi ya Mkoa, mkuu wa itifaki atakuwa ni Katibu wa Mkoa.

**12.6 Jimbo/Wilaya**

Katika ngazi ya Jimbo/Wilaya, Katibu Mwenezi wa Wilaya atakuwa ndiye mkuu wa itifaki wa Wilaya. Katibu wa Vijana atakuwa msaidizi wake.

## 12.7 Kata

Katika ngazi ya Kata Katibu Mwenezi wa Kata ndiye atakuwa mkuu wa itifaki katika Kata. Katibu wa Vijana atakuwa msaidizi wake.

## 12.8 Tawi

Katika ngazi ya Tawi Katibu Mwenezi wa Tawi atakuwa ndiye mkuu wa itifaki katika Tawi. Katibu wa Vijana atakuwa Msaidizi wake.

## 12.9 Msingi

Katika ngazi ya msingi Katibu wa Msingi atakuwa ndiye mkuu wa itifaki wa Msingi.

## 12.10 Majukumu ya Wakuu wa Itifaki kila Ngazi

Majukumu ya wakuu wa itifaki katika kila ngazi itakuwa:-

(i) Kuhakikisha kuwa utaratibu wa mkutano, kikao au sherehe za chama unaandaliwa na unafahamika na uongozi na hatimaye unafuatwa kwa mfano wajumbe wote wanafika kwenye shughuli maalumu ya chama kabla ya Mwenyekiti wa ngazi husika.

(ii) Kuhakikisha kuwa Mwenyekiti wa ngazi husika ndiye anafungua na kufunga shughuli yeyote ya kichama.

(iii) Kuhakikisha kuwa viongozi wanapewa nafasi ya kutambulishwa, kusema au kuhutubia mkutano kutokana na itifaki zao kiuongozi bila kuathiri muda wa kusema wa mgeni rasmi kwa mujibu wa itifaki.(iv) Mkuu wa Itifaki katika kila ngazi ndiye anayeongoza ratiba ya mkutano, kikao au

semina katika ngazi husika; isipokuwa atafanya kazi kwa mujibu wa Katiba, Kanuni, Taratibu, Tamaduni na Desturi za Chama.

**12.11 Itifaki katika Ngazi za Chama**

Kila ngazi ya Chama inawajibika kwa ngazi ya juu yake kiutendaji kuanzia ngazi ya Msingi, Tawi, Kata, Wilaya, Mkoa, Kanda hadi Taifa (Kamati Kuu, Baraza Kuu hadi Mkutano Mkuu). Kwa itifaki ya Chama Mkutano Mkuu ndio wenye maamuzi ya mwisho juu ya mambo yote ya Chama. Kila ngazi ina wajibu wa kutimiza maagizo na maelekezo ya Chama kutoka ngazi ya juu yake kama inavyoelekezwa kwenye Katiba ya Chama.

**12.12 Itifaki kwa Viongozi wa Chama (Wenyeviti, Makamu Wenyeviti, Makatibu na Makatibu waenezi)**

12.12.1 Wenyeviti watakuwa wasemaji wakuu wa Chama katika ngazi husika.

12.12.2 Makamu wenyeviti watakuwa wasaidizi wakuu wa Wenyeviti wa ngazi zao na kukaimu wakati ambao Wenyeviti hawapo. Makamu Wenyeviti wa Taifa na Kanda watakuwa Wenyeviti wa Kamati za Maadili za Chama.

12.12.3 Makatibu wa Chama kila ngazi watakuwa ni watendaji wakuu na waendeshaji wa shughuli zote za kiofisi kwenye ngazi zao.

12.12.4 Makatibu waenezi watakuwa ni wahamasishaji na waenezaji wa sera za Chama na ilani ya uchaguzi katika kila ngazi za Chama.

**12.13 Lugha**

Lugha rasmi ndani ya Chama itakuwa ni Kiswahili isipokuwa kama kuna mahitaji maalum utaratibu utafanyika ili kupata mkalimani.

**12.14 Mavazi**

Mavazi ni sehemu ya utamaduni wa jamii yoyote duniani. Mavazi yatakayotumika kwenye shughuli za Chama yawe ni mavazi masafi, yenye kuleta heshima mbele ya jamii na yenye alama za Chama.

**12.15 Mapokezi**

Mapokezi katika kila ngazi yatafanywa na viongozi wakuu kama ifuatavyo-:

(i) Mgeni wa kitaifa anayetoka nje au ndani ya nchi atapokelewa na kukaribishwa na kiongozi wa ngazi inayofanana na mgeni husika. Mgeni ambaye anatoka kwenye taasisi ambayo kimuundo haifanani na CHADEMA mgeni atapokelewa na Mwenyekiti wa CHADEMA au mtu yeyote atakayeteuliwa na Mwenyekiti kufanya hivyo.

(ii) Mgeni kutoka ngazi ya juu ya Chama kwenda ngazi ya chini atapokelewa, kukaribishwa na kuagwa na Mwenyekiti wa Chama katika ngazi husika au mtu yeyote atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa ngazi hiyo kufanya hivyo.

# MIONGOZO MBALIMBALI YA CHAMA

## MIONGOZO YA KUSIMAMIA WABUNGE, HALMASHAURI, MADIWANI NA VIONGOZI WA VITONGOJI, VIJIJI NA MITAA INAYOONGOZWA NA CHADEMA

## SEHEMU A
## MWONGOZO WA KUSIMAMIA SHUGHULI, MWENENDO NA MAADILI YA WABUNGE WA CHADEMA

### 1. UTANGULIZI

Kwa lengo la kuhakikisha kuwa viongozi wa Chama na Wabunge wanafanya kazi kwa mwelekeo mmoja na kwa manufaa ya Chama, ni muhimu kuweka utaratibu madhubuti unaoelekeza namna ya kusimamia utendaji, mwenendo na maadili ya Wabunge.

Kanuni

### 2. MWONGOZO WA WABUNGE WA CHADEMA

Bila kuathiri kanuni na taratibu za Bunge na maadili ya viongozi na wanachama wa CHADEMA kama ilivyo katika Katiba ya Chama, Wabunge kwa tiketi ya CHADEMA wanapaswa wazingatie masharti ya Mwongozo huu kama ifuatavyo:-

(a) Mbunge anatakiwa kutii na kutimiza maagizo anayopewa na Chama kupitia vikao halali na kama hakubaliani na maagizo hayo aeleze hivyo kupitia taratibu na ngazi zilizowekwa kwenye Katiba ya Chama.

(b) Itakuwa ni mwiko kwa Mbunge kukashifu Chama au kiongozi wa CHADEMA ndani au nje ya Bunge.

(c) Mbunge ni mwakilishi wa Chama, kwa hiyo katika michango yao Bungeni ni lazima wazingatie na kusisitiza sera, mwelekeo na msimamo wa Chama kwa jambo husika.

(d) Mbunge anawajibika kutumia hadhi, uwezo, wadhifa na nafasi aliyonayo kama Mbunge kukijenga Chama ndani na nje ya Bunge.

(e) Mbunge anatakiwa kuwa na tabia ambayo ni mfano wa kuigwa katika jamii.

(f) Ni wajibu wa Wabunge kutoa taarifa za utendaji kazi katika Majimbo yao kwenye vikao vya Chama.

(g) Ni wajibu wa Mbunge kuchangia Chama na kushiriki katika shughuli za uenezi wa Chama kama itakavyoelekezwa na vikao halali.

(h) Mbunge wa viti maalumu atafanya kazi zake kwa kuzingatia utaratibu kama ifuatavyo;

   i. Atafanya kazi zake za uwakilishi ndani ya Mkoa wake alikochaguliwa na hivyo kazi zake zitakuwa ndani ya Mkoa husika pamoja na Wilaya/Majimbo yake.

   ii. Atalazimika kutoa taarifa yake ya utendaji ya kiserikali na kichama kwa Katibu Mkuu kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka na nakala ya taarifa hiyo itawasilishwa kwa Katibu wa Mkoa na Kanda.

   iii. Chama kinaweza kumpangia maeneo mengine ya kufanya kazi nje na eneo lake pale itakapoonekana inafaa au kulingana na mahitaji maalumu.

**NIDHAMU:**

Utaratibu wa Nidhamu

Bila kuathiri maadili na taratibu za kinidhamu zilizopo katika Katiba ya Chama, makosa yafuatayo yatahesabiwa kuwa ni makosa ya kinidhamu na yatastahili adhabu:-

(a) Mbunge kukaidi maagizo halali ya Chama

(b) Mbunge kukashifu Chama ndani au nje ya Bunge.

(c) Mbunge kulaumu au kulalamikia maamuzi ya vikao vya Chama nje ya vikao.

(d) Mbunge kuacha kujihusisha na shughuli za Chama bila sababu

(e) Mbunge kukataa kuchangia Chama.

(f) Mbunge kuchochea mgawanyiko ndani ya Chama.

Mbunge atakayefanya makosa yaliyoainishwa katika sehemu hii atakuwa ameonesha mwenendo usioendana na Itikadi, Falsafa, Madhumuni, Kanuni na Maadili ya Chama. Kwa mujibu wa Katiba ya Chama Ibara ya 5.4.3 Mbunge huyo atastahili adhabu.

**4. UTOAJI WA TAARIFA ZA UTENDAJI**

Taarifa za Utendaji

Kwa lengo la kukiwezesha Chama kujua changamoto zinazolikabili Jimbo la Mbunge na kuona namna Sera na Ilani ya Chama zinavyotumika na kuwezesha Chama kushauri au kusaidia upatikanaji wa ufumbuzi wa matatizo yaliyopo, Wabunge kwa kupitia umoja wao kwa mujibu wa Katiba ya Chama na kila mmoja kwa eneo lake watatakiwa kutoa taarifa zao za utendaji.

(a) Mbunge mmoja mmoja:-

i. Kila Mbunge atatakiwa kuwasilisha kwa Katibu Mkuu mikakati na mpango wa kazi wa mwaka kwa ajili ya Jimbo lake kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka.

ii. Kila Mbunge atatakiwa kutoa taarifa ya utendaji kazi za kiserikali na kichama kwa Katibu Mkuu kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka na nakala ya taarifa hiyo itawasilishwa kwa Katibu wa Kanda na Mkoa.

iii. Bila kuathiri ibara ya 2.0 (h) Wabunge wa Viti Maalum Jimbo lao ni Chama. Kama anavyowajibika Mbunge wa Jimbo, ndivyo hivyo Wabunge wa Viti Maalum watakavyowajibika kwa Chama.

(b) Katibu wa Kamati ya Wabunge:-

i. Katibu wa Kamati ya Wabunge kwa mujibu wa Katiba, atatakiwa kuwasilisha mpango wa jumla wa shughuli za Wabunge kwenye kikao cha kwanza cha Kamati Kuu cha mipango.

ii. Katibu wa Kamati ya Wabunge atatoa taarifa ya utendaji wa Wabunge katika Majimbo yao na ndani ya Chama kwenye kikao cha Kamati Kuu kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka.

## 5. WAJIBU WA CHAMA KWA WABUNGE

Wajibu wa Chama

Wajibu wa Chama kwa Wabunge utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kuwajengea uwezo Wabunge kuboresha utendaji wao.

(b) Kujenga na kuweka mtandao thabiti wa Chama katika Majimbo yao.

(c) Kuwapatia taarifa muhimu na sahihi zitakazowasaidia kutekeleza majukumu yao.

(d) Kuwathamini na kuwatambua kama Maafisa Waenezi wa Chama.

## 6. WAJIBU WA WABUNGE KWA CHAMA

Wajibu wa Wabunge

Pamoja na wajibu wa kikatiba walionao kama viongozi na wanachama, Wabunge watakuwa na wajibu ufuatao:

(a) Kuchangia Chama kifedha kutoka katika mapato yao ya Ubunge.

(b) Kushiriki moja kwa moja katika ziara za uenezi na ujenzi wa Chama kadiri zitakavyopangwa na Chama.

(c) Kuhakikisha Chama kinaimarika katika maeneo yao (d) Kwa kutumia fursa na hadhi waliyonayo katika jamii, kusaidia Chama kupanuka na kuimarika

(e) Kuwa maafisa Waenezi wa Chama

(f) Kuhakikisha kuwa wanatekeleza ilani na sera ya Chama katika maeneo yao

## 7. MICHANGO YA WABUNGE KWA CHAMA

Michango ya kifedha

### a) Wabunge wa Majimbo:

Mbunge wa Jimbo ana majukumu matatu kisiasa

i. Kuwatumikia wapiga kura wake.

ii. Kujenga na kuimarisha mtandao wa Chama katika Jimbo lake.

iii. Kusaidia Chama kukua na kuimarika nchi nzima.

iv. Kwa sababu ya majukumu hayo, Mbunge wa Jimbo atachangia Chama kila mwezi 10% ya posho za kibunge.

### b) Wabunge Viti Maalum:-

Jimbo la Wabunge hawa ni Chama, na jukumu lao la msingi ni kusaidia Chama ili kikue na kuimarika. Wabunge wa Viti Maalum watachangia Chama kila mwezi 30% ya posho za kibunge.

## SEHEMU B

## MWONGOZO WA KUSIMAMIA SHUGHULI, MWENENDO NA MAADILI YA HALMASHURI ZINAZOONGOZWA NA CHADEMA

### 1. UTANGULIZI

Wapiga kura huchagua Chama na mgombea kwa kuamini Sera na mikakati iliyoainishwa kuwa ndiyo njia bora ya kuwafikisha kwenye maendeleo. Kwa sababu hiyo, ni dhahiri kuwa Halmashauri zote zinazoongozwa na CHADEMA ni lazima ziongozwe kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA kwa maana ndiyo ilani iliyochaguliwa na wapigakura wa Halmashauri husika.

### 2. MWONGOZO WA HALMASHAURI ZINAZOONGOZWA NA CHADEMA

Halmashauri zinazoongozwa na CHADEMA

Bila kuathiri kanuni na taratibu zilizowekwa kisheria kusimamia Halmashauri, Halmashauri zote zinazoongozwa na CHADEMA zitaendeshwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

a) Halmashauri zote zinazoongozwa na CHADEMA zinatakiwa kuongozwa kwa mujibu wa Sera na Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA.

b) Halmashauri zinazoongozwa na CHADEMA zinatakiwa kutii na kutimiza maagizo yanayotolewa na Chama kupitia vikao vyake mbalimbali.

c) Madiwani wa CHADEMA katika Halmashauri inayongozwa na CHADEMA ni lazima wakutane na uongozi wa Chama ngazi ya

Wilaya husika angalau mara moja kila robo ya mwaka ili kupata miongozo mbalimbali. Vikao vya dharura kati ya Madiwani na Chama vinaweza kuitishwa kila inapohitajika.

d) Kila Mwenyekiti wa Halmashauri ya CHADEMA atatakiwa kuwasilisha mipango na mikakati ya maendeleo na huduma waliyojiwekea kwa mwaka husika kwa Katibu Mkuu kupitia ofisi ya Katibu wa Kanda kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka.

e) Kila Mwenyekiti wa Halmashauri inayoongozwa na CHADEMA atatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Halmashauri yake kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama kwa Katibu Mkuu kupitia ofisi ya Katibu wa Kanda.

f) Kila Halmashauri inayoongozwa na CHADEMA kwa kupitia Madiwani wake wana wajibu wa kuhakikisha kuwa Chama katika Halmashauri husika kinakua na kuimarika.

g) Halmashauri zinazoongozwa na CHADEMA lazima ziwe mfano wa kuigwa katika:-

i. Kushughulikia kero za wananchi.
ii. Matumizi mazuri ya fedha za umma.
iii. Kuwashirikisha wananchi katika kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali katika maendeleo yao.
iv. Kupambana na rushwa na kutetea haki za binadamu

v. Kubuni mbinu mbalimbali za kuwaletea wananchi maendeleo.

h) Na mambo mengine yote halali ambayo wananchi wanayategemea kutoka kwa Serikali yao; na Serikali itawajibika kuyatekeleza.

## 3. WAJIBU WA CHAMA KWA HALMASHAURI ZINAZOONGOZWA NA CHADEMA

Ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zetu zinafanya kazi ya kutafsiri Ilani ya Chama kwa vitendo katika utekelezaji wa majukumu yao kwa wananchi, Chama kitawajibika kufanya yafuatayo:-

a) Kutoa miongozo na maelekezo ya namna ya uendeshaji wa shughuli za Halmashauri kwa wakati.

b) Kuwajengea uwezo Wenyeviti wa Halmashauri zetu, viongozi wa Kamati mbalimbali za Halmashauri na Madiwani wetu ili kuwaongezea ufahamu na ufanisi katika utelezaji wa majukumu yao.

c) Kusimamia kwa karibu utendaji wa Halmashauri.

d) Kuzisaidia Halmashauri kuweka mipango na mikakati thabiti ya namna ya utekelezaji wa shughuli zao.

e) Kwa kushirikiana na Madiwani wa Halmashauri husika, kuimarisha mtandao wa Chama katika Halmashauri hiyo.

f) Kushauri na kuelekeza Halmashauri inayoongozwa na CHADEMA kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watakaokwamisha

utendaji wa kazi wa Halmashauri husika.g) Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya viongozi wa Halmashauri wanaotokana na Chama watakaokaidi maelekezo, maagizo au msimamo wa Chama juu ya jambo linalohusu Halmashauri yao.

h) Kusimamia kuundwa kwa Umoja wa Madiwani wa CHADEMA.

i) Pamoja na wajibu mwingine wowote ambao Chama kitaona kinatakiwa kutimiza kwa Halmashauri zake kulingana na wakati na matukio yaliyopo.

## 4. WAJIBU WA HALMASHAURI KWA CHAMA

a) Kutoa taarifa za utendaji kazi katika Halmashauri kwa Chama ngazi ya Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa.

b) Kuhakikisha Chama katika eneo la Halmashauri yao kinakua na kuimarika.

c) Kuhakikisha sera za Chama zinatafsiriwa kwa vitendo katika Halmashauri yao.

d) Na wajibu mwingine wowote ambao Halmashauri itaona unafaa kutekelezwa kwa maslahi ya Chama na Watanzania.

# SEHEMU C

## MWONGOZO WA MADIWANI WA CHADEMA

1. Kwa mujibu wa Mwongozo huu neno “Diwani” litakuwa na maana ya Diwani atokanaye na CHADEMA.

2. Bila kuathiri taratibu za kisheria za Halmashauri na maadili ya viongozi na wanachama kama ilivyo katika Katiba ya Chama, Madiwani kwa tiketi ya Chadema watatakiwa kuzingatia yafuatayo:-
   (a) Diwani anatakiwa kutii na kutimiza maagizo anayopewa na Chama kupitia vikao halali, kama hakubaliani na maagizo hayo aelezee hivyo kupitia taratibu na ngazi zilizowekwa kwenye Katiba ya Chama.
   (b) Itakuwa ni mwiko kwa Diwani kukashifu Chama au kiongozi wa Chama ndani au nje ya Halmashauri.
   (c) Diwani ni mwakilishi wa Chama, kwa hiyo katika michango yao kwenye vikao vya Halmashauri ni lazima wazingatie na kusisitiza Ilani, Sera, mwelekeo na msimamo wa Chama kwa jambo husika.
   (d) Diwani anawajibika kutumia hadhi, uwezo, wadhifa na nafasi aliyonayo kama Diwani kukijenga Chama ndani na nje ya Halmashauri.
   (e) Diwani anatakiwa kuwa na tabia ambayo ni mfano wa kuigwa katika jamii.

(f) Ni wajibu wa Madiwani kutoa taarifa za utendaji kazi katika Kata na Halmashauri zao kwenye vikao vya Chama.

(g) Ni wajibu wa Diwani kuchangia Chama na kushiriki katika shughuli za uenezi wa Chama kama itakavyoelekezwa na vikao halali vya Chama.

## 3. Michango ya Madiwani kwa Chama

Utaratibu wa Michango

Madiwani wote watalazimika kutoa 5% ya posho zao za vikao kwa Chama kila kikao cha Kawaida cha Baraza la Madiwani (Full Council).

## SEHEMU D

## MWONGOZO WA VIONGOZI WA VITONGOJI, VIJIJI NA MITAA

Mitaa/Vijiji na Vitongoji

Katika Mwongozo huu neno "Kiongozi", litakuwa na maana ya kiongozi wa Kitongoji, Kijiji au Mtaa anayetokana na CHADEMA.

Kiongozi wa Kitongoji, Kijiji au Mtaa atatakiwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Kiongozi anatakiwa kutii na kutimiza maagizo anayopewa na Chama kupitia vikao halali, kama hakubaliani na maagizo hayo aeleze hivyo kupitia taratibu na ngazi zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba.

(b) Itakuwa ni mwiko kwa kiongozi kukashifu Chama au viongozi wa Chama.

(c) Viongozi wa Vijiji/Mtaa na Vitongoji ni wawakilishi wa Chama, kwa hiyo katika utendaji wa kazi zao ni lazima wasisitize Sera na Ilani ya Chama na kutumia jukwaa hilo la uongozi kukijenga Chama.

(d) Kiongozi wa Kijiji, Mtaa au Kitongoji anawajibika kutumia hadhi, uwezo, wadhifa na nafasi aliyonayo kuhakikisha Chama kinaimarika katika eneo lake la uongozi.

(e) Kiongozi anatakiwa kuwa na tabia ambayo ni mfano wa kuigwa katika jamii.

(f) Ni wajibu wa viongozi wa Vijiji na Mitaa kutoa taarifa za utendaji wa kazi zao za kiserikali na ushiriki wao katika shughuli za Chama kwenye

vikao vya Chama ngazi za Kijiji/Mtaa na Kata ili kupata ushauri, maelekezo na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Chama juu ya utekelezaji wa majukumu yao.

(g) Ni wajibu wa viongozi wa Vijiji/Mitaa na Vitongoji kuchangia Chama kama ilivyo kwa wanachama wengine na kushiriki katika shughuli za uenezi wa Chama.

## SEHEMU E

## HATUA ZA KINIDHAMU KWA WABUNGE, MAMEYA/ WENYEVITI WA HALMASHAURI, MADIWANI, WENYEVITI WA VITONGOJI, VIJIJI NA MITAA

**1. UTANGULIZI**

Utaratibu wa Nidhamu

Utaratibu wa nidhamu kwa Wabunge, Mameya/ Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani, Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa utakuwa kama ifuatavyo:-

**2. WABUNGE, MAMEYA/MANAIBU MEYA WENYE VITI/MAKAMUWENYEVITIWAHALMASHAURI:-**

Ili hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Mbunge au Meya/Naibu Meya Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri taratibu zifuatazo zitatakiwa zifuatwe:-

(i) Malalamiko juu ya utovu wa nidhamu au jambo lolote linalolalamikiwa yafikishwe kwa Katibu Mkuu kwa maandishi ili yafikishwe kwenye Kamati ya Maadili ya Taifa.

(ii) Kamati ya Maadili ya Taifa itajadili mantiki ya malalamiko na kuona kama kuna hoja ya msingi katika malalamiko hayo.

(iii) Kamati ya maadili ikiridhika kuwa kuna hoja ya msingi ambayo inahitaji kushughulikiwa na Kamati Kuu, itawasilisha taarifa yake kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Kamati Kuu.

(iv) Kamati Kuu ikiridhika kuwa kuna hoja ya msingi itafanya uamuzi.

(v) Kamati ya Maadili ngazi ya Taifa katika uchunguzi wake italazimika kuwaita walalamikaji na mlalamikiwa na kuwahoji juu ya suala husika na kupata ushahidi wa pande zote.

(vi) Kamati ya Maadili ngazi ya Taifa haitakuwa na uamuzi wowote juu ya suala hilo bali itaandika taarifa ya uchunguzi na kutoa mapendekezo kwa Kamati Kuu.

(vii) Kamati Kuu baada ya kupokea mapendekezo hayo inaweza kuchukua hatua za dharura kama itaona inafaa juu ya suala hilo ili kunusuru Chama kama kuna hali ya kutishia hatima na uhai wa Chama.

(viii) Asiyeridhika na uamuzi wa Kamati Kuu atakuwa na haki ya kukata rufaa Baraza Kuu.

(ix) Baraza Kuu litatoa uamuzi juu ya suala hilo bila kulazimika kuita pande zinazohusika.

(x) CHADEMA itashughulikia matatizo ya viongozi na wanachama kwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba ya Chama, wala hata siku moja haitashughulikia mambo kama hayo Mahakamani. Mwanachama atakayeshindwa kufuata taratibu na ngazi za Chama hatavumiliwa na atakuwa amejifukuzisha uanachama.

(xi) Upande wowote unaohusika na mgogoro unaweza kuomba kuitwa na kikao chochote kinachoshughulikia suala hilo ili kutoa ufafanuzi zaidi.

1. **MADIWANI:**

Kwa Madiwani taratibu zote zilizoelezwa katika sehemu (a) (i–vi) zitafanywa na Kamati ya Maadili ya Kanda ambamo Kata au Diwani husika anatoka. Mapendekezo ya hatua za kuchukua yatapelekwa kwenye Kamati Kuu ya Chama Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

Rufaa ya Diwani itakatwa kwa Baraza Kuu na litakuwa na uamuzi wa mwisho.

2. **VIONGOZI WA VIJIJI/MITAA NA VITONGOJI**

Taratibu za (a) (i – vi) zitafanywa na Kamati ya Maadili ya Kanda na uamuzi utatolewa na Kamati ya Utendaji ya Kanda na rufaa yake itakuwa kwenye Kamati Kuu. Na Kamati Kuu itakuwa na uamuzi wa mwisho.

# MWONGOZO WA KUTANGAZA KUSUDIO LA KUWANIA NAFASI ZA UONGOZI KWENYE VYOMBO VYA UWAKILISHI SERIKALINI

## 1. UTARATIBU WA KUTANGAZA KUSUDIO LA KUGOMBEA

Utalatibu

Wanachama wenye kusudio/nia ya kugombea nafasi mbalimbali kwenye vyombo vya uwakilishi kwenye serikali (kama vile Uenyekiti wa Serikali ya Kijiji/Mtaa, Udiwani, Ubunge/Uwakilishi na Urais) wanatakiwa kuzingatia utaratibu ufuatao;

(a) Kuwasilisha kusudio lake la kugombea nafasi ya uongozi serikalini kwa Katibu wa Chama wa ngazi yake ya uongozi kwa mujibu wa Katiba isipokuwa nafasi ya Ubunge ambayo itaratibiwa na Katibu Mkuu kupitia ofisi za Kanda.

(b) Kuwasilisha wasifu wake pamoja na nakala za vyeti vya elimu kwa Katibu wa ngazi yake.

(c) Ofisi ya Katibu Mkuu itaweka utaratibu wa namna ya kuwatangaza waliowasilisha kusudio/nia ya kutaka kugombea nafasi mbalimbali baada ya taarifa zao kujadiliwa na vikao vya Chama katika ngazi husika. Na Katibu Mkuu atatangaza katika vyombo vya habari wale waliotangaza nia.

(d) Ni marufuku kuwa na makundi au mitandao ya kuwania uongozi ndani ya Chama au serikalini kwa nia kujihakikishia ushindi.

(e) Bila kuathiri Mwongozo wa Kuendesha Kampeni ya Uchaguzi ndani ya Chama

pamoja na marekebisho yake, mwanachama hataruhusiwa kuwachafua wenzake kwa njia yoyote waliowasilisha kusudio/nia ya kutaka kugombea nafasi mbalimbali za uwakilishi serikalini.

(f) Bila kuathiri Mwongozo dhidi ya Rushwa wa mwaka 2012 kiongozi/mwanachama asijihusishe na rushwa kabla na baada ya kuwasilisha kusudio/nia ya kutaka kugombea.

(g) Kwa nafasi ya Uongozi wa Kitaifa ndani ya Chama na Urais taarifa za walio na kusudio la kugombea nafasi hizo zitawasilishwa kwa Katibu Mkuu na kujadiliwa na Kamati Kuu na kutolewa uamuzi kwa hatua zinazofuata.

## 2.0 ADHABU

2.1 Atakayekiuka Utaratibu kama ulivyoainishwa katika kifungu 1.0 (d) (e) (f) cha Mwongozo huu, adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa;

(a) Kupewa onyo

(b) Kupewa onyo kali na kuwekwa katika uangalizi wa kipindi maalum.

(c) Kuzuiwa kugombea nafasi aliyokusudia ndani ya Chama na Serikali kwa tiketi ya CHADEMA.

(d) Kufukuzwa uanachama

(e) Kuripotiwa kwenye vyombo vya dola hasa kwa makosa ya jinai kama vile rushwa.

2.2 Adhabu zilizoainishwa katika kifungu cha 2.1 (a), (b), (c), (d), (e) cha Mwongozo huu hazitatolewa bila kuzingatia utaratibu wa Kanuni ya 6.5.2 ya Kanuni za Chama.

a) Kwa nafasi ya kitongoji mamlaka ya nidhamu itakuwa ni Tawi,

b) Kwa nafasi ya Mtaa/Kijiji mamlaka ya nidhamu ni Kata

c) Kwa nafasi ya Kata mamlaka ya nidhamu ni Jimbo/Wilaya

d) kwa nafasi ya Ubunge, Uenyekiti na Umakamu Uenyekiti, Umeya na Unaibu Umeya wa Halmashauri mamlaka ya nidhamu ni ngazi ya Kanda.

e) Na Nafasi ya Urais, Uspika na Unaibu Spika, Kiongozi na Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni au Baraza la Uwakilishi mamlaka ya nidhamu itakuwa Kamati Kuu.

## 3. MAMBO YA JUMLA

(a) Kutowasilisha taarifa ya kusudio la kugombea nafasi za uongozi hakutamuondolea mwanachama sifa ya kugombea.

(b) Kwa majimbo ya uchaguzi yaliyo chini ya Wabunge wa CHADEMA utaratibu wa kutangaza kusudio/nia utaruhusiwa katika mwaka wa uchaguzi kwa utaratibu utakaotolewa na ngazi ya Taifa.

(c) Mwongozo huu usomwe pamoja na mwongozo wa Chama dhidi ya Rushwa.

(d) Mwongozo huu usomwe pamoja na Mwongozo wa Taratibu za kuendesha Kampeni za Uchaguzi ndani ya Chama na maboresho yake.

# MWONGOZO WA TARATIBU ZA KUENDESHA KAMPENI ZA CHAGUZI ZA NDANI YA CHAMA TOLEO LA 2012

## 1.0 UTANGULIZI:

Kwa kuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo ni Chama kinachoamini katika demokrasia, usawa na maadili ya kweli;

Na kwa kuwa maadili ya Chama ndiyo yanaainisha sifa za uongozi wa Chama ambazo ni pamoja na nidhamu, utii, uwajibikaji na dhamira ya wanachama, viongozi wa Chama katika ngazi mbalimbali za muundo wa chama na jinsi ya kuwapata na kuwapima viongozi hao;

Hivyo basi, Mwongozo huu una lengo la kuhakikisha kuwa kampeni zinafanyika kwa uwazi, haki na kufuata misingi ya kidemokrasia.

## 2.0 TARATIBU ZA KUENDESHA KAMPENI NDANI YA CHAMA

Kampeni za uchaguzi ndani ya Chama zitatakiwa kufuata utaratibu ufuatao:-

(i) Mgombea au Wakala wake hataruhusiwa kufanya kampeni kabla ya muda wa kampeni kutangazwa na mamlaka husika ndani ya chama.

(ii) Mgombea au Wakala wake hataruhusiwa kufanya kampeni chafu kwa kumkashifu mgombea mwenzake kwa kusambaza nyaraka,

vipeperushi au kusambaza taarifakwa njia ya mitandao ya kijamii zisizohusiana na wasifu wake.

(iii) Itakuwa ni marufuku kusambaza taarifa kwa njia yoyote ile zenye lengo la kukashifu mgombea au kiongozi wa Chama.

(iv) Itakuwa ni marufuku kwa Mgombea au wakala wake kufanya kampeni kwa kuhusisha ukanda, udini, ukabila au ubaguzi wa aina yeyote ile.

(v) Mgombea au wakala wake anatakiwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika mwongozo dhidi ya rushwa.

(vi) Mgombea au wakala wake atatakiwa kuwa na sifa mahususi kama zilivyoainishwa na Katiba na Kanuni za Chama.

(vii) Mgombea au mwakilishi wake hataruhusiwa kufanya kampeni kwa kujinasibu na kiongozi yeyote wa kiTaifa, wilaya au kiongozi yeyote wa kuchaguliwa iwe kwa mazuri au mabaya.

## 3.0 ADHABU:

Ukiukwaji wa Taratibu na adhabu

Mgombea yeyote atakayekiuka taratibu na kanuni hizi atachukuliwa hatua zifuatazo;

(i) Kupewa onyo

(ii) Kupewa onyo kali

(iii) Kuondolewa katika mchakato wa uchaguzi iwapo itathibitika kuwa mgombea amekiuka utaratibu wa kampeni kwa mujibu wa Mwongozo huu.

(iv) Kufungiwa kugombea nafasi yeyote ya uongozi ndani ya chama kwa muda utakaoamuliwa na mamlaka husika isipokuwa muda hautazidi miaka mitano.

(v) Hatua zote zitazingatia utaratibu wa mamlaka za kinidhamu kama zilivyoainishwa katika ibara ya 6.3.6 ya Katiba.

## 4.0 MAMBO YA JUMLA KUHUSU KANUNI HIZI

Mambo ya Jumla

(i) Bila kuathiri taratibu za kuchukua hatua za kinidhamu na ukomo wa muda kama ulivyoainishwa katika kanuni ya 6.5.2 ya Kanuni Kuu za Chama, taratibu za kutumia Mwongozo huu utazingatia muda wa kampeni na tarehe ya uchaguzi na si vinginevyo.

(ii) Mwongozo huu ni sehemu ya Katiba na Kanuni za Chama, hivyo basi ikitokea mgongano wowote Katiba na Kanuni za za Chama zitatamalaki.

## MWONGOZO WA CHAMA DHIDI YA RUSHWA
## TOLEO – 2012

### 1. RUSHWA KWENYE UCHAGUZI NDANI YA CHAMA

Katazo la Rushwa ndani ya Chama

Ni marufuku kwa mwanachama au kiongozi kujihusisha na mambo yafuatayo wakati wa uchaguzi ndani ya Chama.

i. Kutoa fedha kwa njia yoyote ile, vyakula, vinywaji au zawadi nyinginezo kwa wajumbe / wapiga kura kwa lengo la kujipatia kura.
ii. Kuwasafirisha wajumbe / wapiga kura kuhudhuria Mkutano/kituo cha kupigia kura kwa ngazi husika kwa ajili ya uchaguzi kwa lengo la kujipatia kura.
iii. Kutoa ahadi zenye lengo la kuwalipa fadhila wajumbe au wapiga kura baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika.
iv. Kuandaa kikao chochote cha wapiga kura kwa lengo la kuwapa fedha, chakula au zawadi zingine bila kuzingatia taratibu za kampeni zilivyoainishwa.
v. Kutoa, kushinikiza, kupokea, au kushawishi rushwa ya ngono.
vi. Kutumia mamlaka ya kiongozi kwenye Chama kupendelea upande mmoja wa mgombea.
vii. Kutumia dhamana ya uongozi ili kujinufaisha yeye binafsi kisiasa au kimali wakati wa uchaguzi.

### 2. RUSHWA NJE YA MFUMO WA CHAMA

Ushiriki katika rushwa nje ya mfumo wa Chama

Bila kuathiri Kanuni ya kumi ya Kanuni za Chama, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya

kiongozi au mwanachama atakayebainika kujihusisha na rushwa katika shughuli zake za kila siku.

Masharti ya Mwongozo

## 3. MASHARTI YA MWONGOZO DHIDI YA RUSHWA

Itakuwa ni marufuku kwa kiongozi au mwanachama yeyote wa CHADEMA kujihusisha na rushwa ndani na nje ya Chama. Ikiwa itadhibitika kuwa kiongozi au mwanachama amejihusisha na rushwa hatua zifuatazo zitachukuliwa;

(i) Atapewa taarifa ya tuhuma zinazomkabili kwa maandishi na kutakiwa kuzijibu tuhuma hizo ndani ya siku saba baada ya kupata barua husika au muda mwingine wowote kama utakavyotajwa katika barua husika.

(ii) Baada ya kujibu tuhuma hizo kikao cha nidhamu cha mamlaka ya maamuzi kwa mujibu wa Katiba kitaitishwa na kutoa maamuzi husika haraka iwezekanavyo.

(iii) Kikao cha kinidhamu kinaweza kutoa adhabu zifuatazo baada ya kuridhika na tuhuma dhidi ya mlalamikaji;

- (a) Onyo kali.
- (b) Kuwa katika kipindi cha uangalizi maalumu.
- (c) Kuvuliwa nyadhifa za uongozi ndani ya Chama.
- (d) Kuvuliwa uanachama
- (e) Kuripotiwa kwa mamlaka za kisheria kwa ajili ya hatua za kisheria.

(f) Kutoruhusiwa kugombea nafasi yoyote ndani ya Chama kwa muda kwa muda utakaoamuliwa isipokuwa muda huo hautazidi miaka mitano.

(iv) Itakuwa ni marufuku kwa mwanachama / kiongozi kutoa tuhuma za rushwa bila uthibitisho dhidi ya kiongozi au mwanachama.

## 4. MAMBO YA JUMLA KUHUSU MWONGOZO HUU.

Mambo ya Jumla

(i) Kwa kuwa mwongozo huu ni sehemu ya Katiba na Kanuni za Chama. Hivyo basi endapo kipengele cha Mwongozo huu kitabainika kukinzana na Katiba au Kanuni, masharti ya Katiba na Kanuni yatatamalaki.

## MWONGOZO WA UMOJA WA MADIWANI WA CHADEMA

**1. LENGO LA KUANZISHA UMOJA WA MADIWANI** Lengo

Lengo la kutungwa kwa Mwongozo huu ni kuwaunganisha Madiwani wanaotokana na Chama ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi.

**2. MUUNDO WA UMOJA WA MADIWANI** Muundo

Muundo wa Umoja wa Madiwani utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Madiwani ngazi ya Wilaya / Halmashauri.

(b) Baraza la Madiwani ngazi ya Mkoa.

(c) Baraza la Madiwani ngazi ya Kanda.

(d) Baraza la Madiwani ngazi ya Taifa.

Vikao

**3. VIKAO VYA UMOJA WA MADIWANI**

Umoja wa Madiwani utakuwa na vikao viwili vya kusimamia na utendaji katika kila ngazi. Vikao hivyo ni kama ifuatavyo;

(a) Mkutano Mkuu wa madiwani wa ngazi husika

(b) Kamati ya Uongozi ya ngazi husika

Ngazi ya Wilaya

**4. UMOJA WA MADIWANI NGAZI YA WILAYA/ HALMASHAURI**

Umoja wa Madiwani ngazi ya Wilaya utakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano Mkuu

Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni Madiwani wote wanaotokana na Chama ndani ya Wilaya husika

(b) Kamati ya Uongozi

Wajumbe Kamati ya Uongozi ni:-

(i) Mwenyekiti wa Umoja wa Madiwani

(ii) Katibu wa Umoja wa Madiwani

(iii) Mnadhimu wa Madiwani

(iv) Mratibu wa mahusiano na mawasiliano

(v) Mtunza Hazina wa Madiwani

(vi) Mwenyekiti/ Meya wa Halmashauri husika.

(c) Endapo itatokea idadi ya Madiwani ni wachache kuliko nafasi za uongozi zilizopo katika ngazi ya Wilaya, itatakiwa angalau kuwe na Mwenyekiti na Katibu wa madiwani.

(d) Endapo idadi ya Madiwani ni chini ya watatu, atachaguliwa Diwani mmoja kuwakilisha Wilaya katika ngazi ya Mkoa na hakutakuwa na uongozi wa Umoja wa Madiwani.

(e) Kamati ya Uongozi itafanyika angalau mara nne kwa mwaka na vikao vya dharura vinaweza kuitishwa kadiri ya mahitaji.

(f) Mkutano Mkuu wa Wilaya utafanyika mara moja kwa mwaka.

## 5. UMOJA WA MADIWANI NGAZI YA MKOA

Ngazi ya Mkoa

(1) Umoja wa Madiwani Ngazi ya Mkoa utakuwa na vikao vifutavyo,

(a) Mkutano Mkuu

Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni:-

(i) Wajumbe wote wa Kamati za Uongozi ngazi ya Wilaya zilizopo ndani ya Mkoa husika.

(ii) Wawakilishi wa wilaya kutoka kwenye wilaya zenye madiwani wachache.

(iii) Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya Mkoa

(b) Kamati ya Uongozi

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ni:-

(i) Mwenyekiti wa Umoja wa Madiwani wa Mkoa.

(ii) Katibu wa Umoja wa Madiwani wa Mkoa.

(iii) Mnadhimu wa Umoja wa Madiwani Mkoa.

(iv) Mratibu wa mahusino na mawasiliano wa Umoja wa Madiwani wa Mkoa.

(v) Mtunza Hazina wa Mkoa.

(vi) Wenyeviti /Mameya wa Halmashauri ndani ya Mkoa.

(2) Kamati ya Uongozi ya Mkoa itakutana mara mbili kwa mwaka.

(3) Mkutano Mkuu utakutana mara moja kila baada ya miaka miwili na nusu

Ngazi ya Kanda

## 6. UMOJA WA MADIWANI NGAZI YA KANDA

(1) Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda utakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano mkuu wa Kanda.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda ni:

(i) Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya Kanda.

(ii) Kamati za Uongozi za Mikoa ndani ya Kanda.

(iii) Makamu Wenyeviti/Manaibu Meya watokao na Chama ndani ya Kanda husika.

(iv) Mameya / Wenyeviti wa Halmashauri ndani ya Kanda.

(b) Kamati ya Uongozi ya Kanda.

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ni:-

(i) Mwenyekiti wa Umoja wa Madiwani wa Kanda.
(ii) Katibu wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda.
(iii) Mnadhimu wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda
(iv) Mratibu wa mahusiano na mawasiliano wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda.
(v) Mtunza Hazina wa Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda.
(vi) Wawakilishi wawili wa Mameya/ Wenyeviti wa Halmashauri ndani ya Kanda watakaochaguliwa na Mameya/ Wenyeviti wote ndani ya Kanda.

(2) Kamati ya Uongozi ya Kanda itakutana mara mbili kwa mwaka

(3) Mkutano Mkuu wa Kanda utakuna mara moja kila baada ya miaka miwili na nusu.

**7. UMOJA WA MADIWANI NGAZI YA TAIFA**

Ngazi ya Taifa

Ngazi ya Taifa itakuwa na Vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano mkuu

Wajumbe wa Mkutano mkuu ni:-

(i) Kamati ya Uongozi ya Taifa.

(ii) Kamati zote za Uongozi za Kanda.(iii) Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Uongozi za Mikoa.

(iv) Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri za CHADEMA.

(b) Kamati ya Uongozi Taifa.

Kamati ya Uongozi ya Madiwani ngazi ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Umoja wa Madiwani Taifa,
(ii) Katibu wa Umoja wa Madiwani.
(iii) Mnadhimu wa Madiwani
(iv) Mratibu wa mahusiano na mawasiliano.
(v) Mtunza Hazina
(vi) Wenyeviti wa madiwani wa Kanda.

## 8. KAZI ZA MIKUTANO MIKUU YA UMOJA WA MADIWANI

Kazi za Uongoozi Mkuu

(1) Mikutano mikuu ya Umoja wa Madiwani itakuwa na kazi zifuatazo;

(a) Kwa ngazi ya Taifa itakuwa na kazi ya kuchagua wawakilishi wa Madiwani kwenye Kamati Kuu kwa mujibu wa ibara ya 7.7.14(j) ya Katiba ya Chama.

(b) Kupitisha mpango kazi wa Umoja wa Madiwa wa miaka mitano na kusimamia utekelezaji wake.

(c) Kuweka taratibu za uendeshaji wa Umoja wa Madiwani.

(d) Kuchagua Kamati za Uongozi za ngazi zao.

(e) Kusimamia utendaji wa Kamati za Uongozi katika ngazi husika.

(f) Kusaidia mamlaka za Chama kusimamia nidhamu kwa Umoja wa Madiwani katika ngazi husika.

(2) Mkutano mkuu wa Taifa wa Umoja wa Madiwani utakutana mara moja kila baada ya miaka miwili na nusu kwa vikao vya kawaida, vikao vya dharura vitaitishwa kwa kadri itakavyoamuliwa na Chama ngazi ya Taifa.

Kazi za Kamati za Uongozi

## 9. KAZI ZA KAMATI ZA UONGOZI ZA UMOJA WA MADIWANI

(1) Kamati za Uongozi za Umoja wa Madiwani katika ngazi zao zitakuwa na kazi zifuatazo;

(a) Kutekeleza mipango ya Umoja wa Madiwani katika ngazi husika.

(b) Kusaidia mamlaka za Chama kusimamia utendaji wa Umoja wa Madiwani katika ngazi husika.

(c) Kuandaa mpango kazi wa Umoja wa Madiwani kwa ngazi husika na kuwasilisha kwenye mkutano mkuu.

(d) Kusimamia utendaji wa Madiwani katika ngazi yao na kupima viwango vya ufanisi.

(e) Kutoa elimu kwa Madiwani ili watambue na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(f) Kusaidiana na Chama kuhakikisha kila Diwani analipa michango yake ya kikanuni kwa Chama kwa wakati.

(g) Kwa kushirikiana na Chama kuhakikisha Chama kinajengwa katika ngazi yao.

(2) Kamati ya Uongozi ngazi ya Taifa itakutana mara moja kwa mwaka na vikao vya dharura vinaweza kuitishwa kadiri ya mahitaji.

## MWONGOZO WA UMOJA WA VIONGOZI WA SERIKALI ZA VIJIJI NA MITAA WA CHADEMA

**1. Utangulizi** Utangulizi

Viongozi wa Serikali za Vijiji na Mitaa wanaotokana na CHADEMA ni kundi muhimu katika harakati za kukieneza Chama katika jamii.

Lengo la kuundwa kwa umoja huu ni kuunganisha kundi hili muhimu kwa ujenzi na ustawi wa Chama kwa ajili ya kusimamia na kutoa huduma kwa wananchi.

**2. Muundo wa Uongozi**

Umoja wa Viongozi wa Vijiji na Mitaa utaundwa katika ngazi za Chama zifuatazo; Muundo

(a) Kijiji/ Mtaa
(b) Kata/ Wadi
(c) Jimbo
(d) Wilaya /Halmashauri/Manispaa au Jiji

**3. Vikao**

Kila ngazi ya muundo katika Umoja huu itakuwa na vikao vifuatavyo :- Vikao

(a) Kamati ya Uongozi
(b) Mkutano Mkuu.

**4. Ngazi ya Kijiji**

(1) Ngazi ya Kijiji itakuwa na vikao vifuatavyo:

(a) Kamati ya Uongozi. Kijiji

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Kijiji ni:

(i) Mwenyekiti wa umoja
(ii) Katibu wa Umoja

(iii) Mratibu wa Mahusiano
(iv) Mtunza Hazina.
(v) Wenyeviti wa Vitongoji.

Mwenyekiti wa Kijiji atokanaye na Chama ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi, isipokuwa kama Mwenyekiti wa Kijiji hatokani na Chama wajumbe watachagua Mwenyekiti wa Umoja huo kutoka miongoni mwa Wenyeviti wa Vitongoji au Wajumbe wa Serikali ya Kijiji.

(b) Mkutano Mkuu

Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni:-

(i) Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi.
(ii) Wajumbe wote wa Halmashauri ya Kijiji wanaotokana na Chama.

**5. Ngazi ya Mtaa** Mtaa

Ngazi ya Mtaa itakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Kamati ya Uongozi.

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Mtaa ni:-

(i) Mwenyekiti wa umoja
(ii) Katibu wa Umoja
(iii) Mtunza Hazina.

Mwenyekiti wa Mtaa atokanaye na Chama ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi, isipokuwa kama Mwenyekiti wa Mtaa hatokani na Chama wajumbe watachagua Mwenyekiti wa Umoja huo kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Serikali ya Mtaa.

(b) Mkutano Mkuu

Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni:-

(i) Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi.

(ii) Wajumbe wote wa serikali ya Mtaa wanaotokana na Chama.

## 6. Ngazi ya Kata

Kata

(1) Ngazi ya Kata itakuwa vikao vifuatavyo;

(a) Kamati ya Uongozi ya Kata.

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ni:-

(i) Mwenyekiti

(ii) Katibu

(iii) Mratibu wa mahusiano na mawasiliano

(iv) Mtunza hazina

(v) Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa yote ndani ya Kata.

(b) Mkutano Mkuu wa Kata

Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni :-

(i) Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Kata.

(ii) Wenyeviti wa vitongoji wote ndani ya Kata husika.

(iii) Wajumbe wote wa Serikali ya Mtaa watokanayo na Chama.

## 7. Ngazi ya Jimbo

Jimbo

Ngazi ya Jimbo itakuwa na vikao vifuatavyo;

(a) Kamati ya Uongozi,

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ni:-

(i) Mwenyekiti
(ii) Katibu
(iii) Mratibu wa uhusiano na mawasiliano
(iv) Mtunza Hazina.

(b) Mkutano Mkuu

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo ni:-

(i) Kamati ya Uongozi ya Jimbo.
(ii) Kamati za Uongozi za Kata.
(iii) Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa yote ndani ya Jimbo.

**8. Ngazi ya Wilaya / Halmashauri**

Wilaya

Ngazi ya Wilaya au Halmashauri itakuwa na vikao vifuatavyo;

(a) Kamati ya Uongozi

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ni:- Mwenyekiti wa wilaya

(i) Katibu
(ii) Mratibu wa uhusiano na mawasiliano
(iii) Mtunza hazina.
(iv) Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Uongozi za majimbo.

(b) Mkutano Mkuu wa Wilaya

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya watakuwa wafuatao;

(i) Kamati ya Uongozi
(ii) Kamati za Uongozi za majimbo.

(iii) Wenyeviti na makatibu wa kata ndani ya Jimbo.

**9. Kazi za Kamati ya Uongozi kila Ngazi**

Kazi za Kamati za Uongozi zitakuwa ni:-

(i) Kuratibu shughuli za Umoja kwenye ngazi husika
(ii) Kuandaa nyaraka za Mikutano Mikuu
(iii) Kuandaa ziara za uenezi wa Chama kwenye ngazi husika

**10. Muda wa Vikao**

Kamati za Uongozi kila ngazi zitafanyika mara nne kila mwaka na Mikutano Mikuu itafanyika mara moja kila mwaka.

**11. Kazi za Mikutano Mikuu kila Ngazi**

Kazi za Mikutano Mikuu zitakuwa ni:-

Uchaguzi

(i) Kuchagua viongozi wa Umoja kwenye ngazi husika
(ii) Kutoa maelekezo ya kiutendaji kwa Kamati za Uongozi ngazi husika
(iii) Kusimamia utendaji wa Kamati za Uongozi kwa ngazi husika

**12. Uchaguzi wa Viongozi**

Kamati za uongozi ngazi zote zitachaguliwa na Mikutano Mikuu ya ngazi husika.

13. Muda wa uchaguzi ni kipindi cha miaka mitano ambacho kitakuwa mwaka mmoja baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

## MWONGOZO WA KAMATI ZA MAADILI YA CHAMA

Kanuni ya 10 Maadili

### 1. UTANGULIZI

Kwa kuwa uadilifu wa viongozi ni nguzo muhimu katika ujenzi wa Chama katika jamii, ili kukiwezesha Chama kufikia lengo hilo na kutekeleza kikamilifu Kanuni ya 10 ya Kanuni za Chama;

Baraza Kuu limetunga Mwongozo wa kuundwa kwa Kamati za Maadili katika ngazi zote za Muundo wa Chama.

Ili kuwezesha Kamati hizo kufanya kazi kwa ufanisi katika kutafsiri Maadili ya Chama yaliyoainishwa katika Kanuni ya 10 ya Kanuni za Chama, Maadili yamefafanuliwa ili kutoa Mwongozo wa kiutendaji kwa kamati hizo.

Kamati zinaundwa kama chombo cha kusaidia Mamlaka za nidhamu ndani ya Chama kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa maana hiyo, Kamati za Maadili hazitachukua nafasi ya mamlaka yoyote ya usimamizi wa nidhamu ndani ya Chama, bali vitakuwa ni vyombo vya kuzijengea Mamlaka hizo uwezo wa kimfumo na kiutekelezaji.

### 2. LENGO

Lengo

Lengo la Kamati za Maadili ni kusaidia mamlaka za nidhamu ndani ya Chama kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi na kwa wakati. Kwa maana hiyo, vyombo hivi vitafanya kazi kama kamati za ufundi (technical committees) za mamlaka za nidhamu za ngazi husika.

## 3. KANUNI ZA MAADILI

Maadili

Kwa mujibu wa Maadili ya Chama kama yalivyoainishwa katika Kanuni ya 10 ya Kanuni za Chama, Katika kutafsiri makosa ya kimaadili ya viongozi na wanachama zifuatazo zitakuwa tafsiri juu ya makosa hayo;

### (a) Usaliti

Usaliti katika Chama litakuwa ndilo kosa kubwa kuliko yote kwa misingi ya kimaadili. Pamoja na mambo mengine, kosa la usaliti litajumuisha matendo yafuatayo:

(i) Kupanga njama za kuhujumu Chama.

(ii) Kutoa siri za Chama kwa washindani wetu wa kisiasa.

(iii) Kupinga misimamo ya Chama hadharani nanje ya vikao vya Chama.

(iv) Kupokea fedha au hongo yoyote kwa lengo la kusaidia washindani wetu kisiasa dhidi ya maslahi ya Chama (kujitoa au kufanya mgombea ajitoe katika uchaguzi).

(v) Kufanya au kushawishi mgomo ndani ya Chama.

(vi) Kuingilia na au kuharibu kwa makusudi mifumo ya Teknolojia na Habari ya Chama kwa lengo la kukihujumu Chama.

(vii) Kuhujumu Mipango au program za Chama kwa namna yoyote ile.

**(b) Mapinduzi**

Katiba ya Chama imeweka utaratibu wa namna ya kuwapata viongozi na/au kuwaondoa madarakani pale inapobidi. Kwa hiyo kitendo chochote cha kuondoa au kupanga kuondoa uongozi au kiongozi wa Chama bila kufuata Katiba na taratibu zilizowekwa itahesabiwa kuwa ni Mapinduzi.

Makosa ya kimapinduzi yatahusisha matendo yafuatayo:

(i) Kupanga na kushiriki njama za kuondoa uongozi au kiongozi madarakani kinyume cha Katiba na nje ya vikao vya Chama.

(ii) Kushawishi au kugharimia mipango ya namna hiyo.

(iii) Kufahamu uwepo wa mpango wa mapinduzi na kukaa kimya bila kutoa taarifa.

**(c) Utunzaji wa siri za chama**

Ni wajibu wa kila kiongozi na mwanachama wa CHADEMA kutunza siri za Chama.

Siri za Chama zitahusisha mambo yote yanayohusu Chama ambayo si kwa matumizi ya umma na /au hayajaruhusiwa kutolewa na mamlaka husika.

Kiongozi au mwanachama atahesabiwa kuwa ametoa siri za Chama nje kama atafanya mambo yafuatayo;

(i) Kupeleka nyaraka za siri za Chama nje ya Chama.

(ii) Kuzungumza mambo ya vikao nje ya kikao.
(iii) Kusema madhaifu ya Chama au kiongozi nje ya vikao.
(iv) Kurekodi na kurusha katika mitandao ya kijamii au kupeleka kwenye vyombo vya habari taarifa za kikao ambazo hajapewa mamlaka ya kuzitoa.
(v) Kuingilia mawasiliano ya viongozi wa Chama kwa nia ovu.

**(d) Rushwa**

Vitendo vya rushwa ndani na nje ya mfumo wa Chama vitashughulikiwa kwa mujibu wa Mwongozo wa rushwa.

**(e) Matumizi mabaya ya madaraka/upendeleo**

Wanachama wote wako sawa mbele ya Katiba ya Chama na wana haki ya kupata huduma, fursa au maslahi kwa usawa ndani ya Chama. Kiongozi hatatakiwa kutumia madaraka yake ndani ya Chama kufanya yafuatayo:

(i) Kutumia mali za Chama kwa manufaa yake binafsi.
(ii) Kujipatia huduma au manufaa binafsi kinyume na taratibu kwa kutumia cheo chake.
(iii) Kutumia nafasi yake kuzuia wanachama wengine kupata haki au fursa wanazostahili na wenye uwezo nazo.
(iv) Kutoa nafasi au fursa kwa upendeleo.

**(f) Matumizi ya lugha**

Kiongozi anatakiwa kutumia lugha ya staha katika vikao na katika mahusiano ya kawaida na umma. Lugha za matusi au zisizo na staha zitakuwa ni kosa.

**(g) Kujitegemea kiuchumi**

Kiongozi wa CHADEMA anatakiwa kuwa na shughuli halali inayompatia kipato cha kuendesha maisha yake.

Pamoja na haki ya mtu kupata misaada kwa jamii inayomzunguka, kiongozi wa CHADEMA hatakiwi kufanya yafuatayo:

(i) Kukopa kuzidi uwezo wake wa kurudisha.

(ii) Kuwa omba omba kwa jamii inayomzunguka.

**(h) Usafi**

Kiongozi anatakiwa kuwa msafi yeye na mavazi yake.

**(i) Makundi ya kuchangamana nayo**

Pamoja na kwamba kazi ya siasa inahitaji kujichanganya na jamii, kiongozi hatatakiwa kuwa na mchangamano wa karibu na wa mara kwa mara na makundi yasiyoaminika katika jamii kulingana na mila na desturi ya jamii husika.

**(j) Kushiriki mambo ya kijamii**

Kiongozi anatarajiwa kuwa karibu na jamii anayoishi, kwa sababu hiyo kiongozi wa CHADEMA atatakiwa kushiriki kwa kadri awezavyo katika matukio ya kijamii katika eneo lake.

## 4. MAJUKUMU YA KAMATI ZA MAADILI

Majukumu ya Kamati

Kamati za Maadili zitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kupokea taarifa za ukiukwaji wa maadili kutoka Kamati Kuu au Mabaraza ya uongozi ya Mkoa au Kamati za Utendaji za Kanda.

(b) Kuchambua na kufanya uchunguzi wa taarifa husika.

(c) Kuhoji na kusikiliza maelezo ya watuhumiwa.

(d) Kupendekeza hatua za kuchukua kwa Mamlaka ya nidhamu ya ngazi husika.

(e) Kusimamia Maadili ndani ya Chama

## 5. MUUNDO WA KAMATI

Muundo

Kamati hizi zitaundwa katika ngazi ya Taifa na Kanda na ngazi zingine kadri itakavyoelekezwa. Muundo utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kamati ya Maadili ngazi ya Taifa.

(b) Kamati za Maadili ngazi za Kanda

## 6. KAMATI YA MAADILI YA TAIFA

Kamati hii itakuwa na wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi saba. Wajumbe wa Kamati watakuwa kama ifutavyo:

(i) Makamu Mwenyekiti Bara – Mwenyekiti wa Kamati.

(ii) Mkurugenzi wa Sheria – Katibu wa Kamati.

(iii) Mwenyekiti wa BAWACHA Taifa – Mjumbe.

(iv) Mwenyekiti wa Wazee Taifa – Mjumbe.

(v) Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa – Mjumbe.

(vi) Wajumbe wasiozidi wawili watakaoteuliwana Mwenyekiti Taifa na mmoja katiyawajumbe hao atatoka Zanzibar

## 7. KAMATI ZA MAADILI ZA KANDA

Kutakuwa na Kamati za Maadili za Kanda. Wajumbe

wa Kamati za Maadili za Kanda watakuwa kama ifuatavyo :

(a) Makamu Mwenyekiti wa Kanda – Mwenyekiti wa Kamati.

(b) Afisa wa sheria wa Kanda – Katibu wa Kamati.

(c) Wenyeviti wa Mikoa katika Kanda husika.

(d) Wajumbe wasiozidi wawili, mmoja mwanamke watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Kanda na kuidhinishiwa na Kamati ya Utendaji ya Kanda.

## 8. MAMLAKA YA KILA KAMATI

Mamlaka

Ili kuleta tija na kuondoa migongano baina ya kamati, kila kamati itafanya kazi zake katika eneo mahususi kwa mujibu wa ngazi yake.

## (a) KAMATI YA MAADILI YA TAIFA

Pamoja na mamlaka ya kuweza kushughulikia suala la maadili kwa ngazi yoyote ikionekana limeshindikana kwa kamati ya ngazi husika, kamati hii itashughulikia masuala ya kimaadili ya viongozi wafuatao;

(i) Viongozi wakuu wa chama isipokuwa Mwenyekiti Taifa.

(ii) Wajumbe wa Kamati Kuu.

(iii) Wenyeviti wa Kanda.

(iv) Wabunge

(v) Mameya/Manaibu Meya na Wenyeviti/ Makamu Wenyeviti wa Halmashauri za Chama.

(vi) Viongozi wengine katika ngazi yoyote ya Chama

## (b) KAMATI ZA MAADILI ZA KANDA

Kamati za Maadili za Kanda zitashughulikia masuala ya kimaadili kwa viongozi wafuatao:-

(i) Viongozi wote wa Kanda isipokuwa Mwenyekiti wa Kanda.

(ii) Viongozi wa Mikoa inayounda Kanda husika.

(iii) Viongozi wa Majimbo/Wilaya, Kata, Matawi na Misingi.

(iv) Na wanachama watakaokiuka maadili.

## 9. KAMATI YA MAADILI YA ZANZIBAR

Zanzibar

Wajumbe wa kamati hii watakuwa kama ifuatavyo:

(a) Makamu Mwenyekiti Zanzibar– Mwenyekiti

(b) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar – Katibu

(c) Viongozi wa Mabaraza wa kitaifa watokao Zanzibar.

(d) Wajumbe wasiozidi wawili kwa uwiano wa kijinsia watakaoteuliwa na Makamu Mwenyekiti Zanzibar na kuthibtishwa na Kamati Maalum ya Zanzibar.

Kamati hii itashughulikia mambo yote ya kimaadili kwa upande wa Zanzibar.

Masuala ya kimaadili yanayowahusu Makamu Mwenyekiti wa Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Wajumbe wa Kamati Kuu wanaotoka Zanzibar, yatashughulikiwa na Kamati ya Maadili ya Taifa.

## 10. MAMBO YA JUMLA

Mambo ya Jumla

Mambo yafuatayo yatazingatiwa katika utekelezaji wa Kazi za Kamati ya Maadili;

(a) Mashitaka/Malalamiko ya Kimaadili yanayomuhusu Mwenyekiti Taifa yatashughulikiwa na Kamati Kuu.

(b) Mjumbe wa Kamati ya Maadili akiwa anakabiliwa na tuhuma za kimaadili, hataruhusiwa kushiriki kikao ambacho jambo lake linajadiliwa.(c) Ikiwa mjumbe wa Kamati atatiwa hatiani na Kamati atakoma kuwa mjumbe wa Kamati ya Maadili.

(d) Kama Mwenyekiti wa Kamati ndiye anayetakiwa kuhojiwa na Kamati, Kamati itachagua Mwenyekiti miongoni mwao, isipokuwa Katibu wa Kamati hatachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati.

(e) Makosa ya kimaadili ni makosa yote yatakayotokana na kukiuka maadili ya Chama kama yalivyoainishwa katika Kanuni ya 10 ya Kanuni za Chama pamoja na masharti ya mwongozo huu

(f) Akidi ya vikao vya Kamati itakuwa ni asilimia 50%.

## MWONGOZO WA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO NDANI YA CHAMA

## (CHADEMA DIGITAL)

[Umetungwa kwa mujibu wa Ibara ya 6.3.7 (b) ya Katiba ya Chama]

**1. Utangulizi**

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA) ni njia ya kisasa ya upashanaji habari katika ulimwengu wa utandawazi. Nadharia kwamba dunia imekuwa kama Kijiji imetokana na kasi kubwa ya ukuaji wa mawasiliano na upashanaji habari inayotokana na maendeleo na mageuzi makubwa katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Duniani.

Kutokana na umuhimu wa mawasiliano katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa Chama kimeamua kutumia mfumo wa TEHAMA kwa dhumuni la kurahisisha mawasiliano na shughuli mbalimbali za kiutendaji na uendeshaji wa Chama.

Kwa kutambua umuhimu wa TEHAMA, Baraza Kuu la Chama limetunga Mwongozo huu, ili kuweka mfumo wa TEHAMA kuwa moja ya njia za mawasiliano rasmindani ya Chama, kuendesha vikao, utoaji wa taarifa, kukichangia Chama kirasilimali na kurahisisha ulipaji wa ada za uanachama.

**2. Kanzidata ya Wanachama**

Kutakuwa na kanzidata ambayo itatunza taarifa za wanachama nchi nzima. Kanzidata ya Chama itakuwa na taarifa zifuatazo;

2.1 Orodha ya wanachama

2.2 Maeneo wanayotoka wanachama ambayo ni; Kanda, Mkoa, Wilaya/Jimbo, Kata, Tawi na Msingi,

2.3 Jinsia

2.4 Nyadhifa ya kiuongozi ya mwanachama,

2.5 Mawasiliano kama namba za simu na baruapepe au taarifa zingine kadiri itakavyohitajika.

**3. Mawasiliano Ndani ya Chama**

Kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano ndani ya Chama, mfumo wa TEHAMA utakuwa ni moja ya njia zitakazotumika katika kurahisisha kufanya kazi hiyo.

Njia zitakazotumiwa katika mawasiliano hayo ni kama ifuatavyo;

3.1 Simu, runinga au kompyuta; vikao vitakavyotumia njia hii ni vile vya mashauriano ya kiofisi pale inapotokea wajumbe wengine kuwa nje ya ofisi.

3.2 Barua pepe au mfumo mwingine kwa kadiri itakavyoamuliwa utatambulika kama mfumo rasmi wa mawasiliano ndani ya Chama. Mtumiaji na mpokeaji wa barua pepe au mawasiliano yoyoteya kiofisi atalazimika kuyatunza mawasiliano hayo ili kuwa rejea pale yatakapohitajika.

3.3 Mitandao ya kijamii – mitandao ya kijamii itakayoanzishwa rasmi itatumika katika utoaji wa taarifa za kichama kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

## 4. Ukusanyaji wa Mapato Kwa Njia ya Tehama

Mwongozo huu unaruhusu na kutoa mamlaka kwa chama kukusanya fedha kwa kupitia mifumo ya kifedha na malipo ya kidigitali. Mapato yafuatayo yatakusanywa kwa mfumo wa kidigitali;

4.1. Kiingilio na ada ya uanachama

4.2. Michango ya hiari

4.3. Michango mingine kadiri itakavyoamuliwa na Kamati Kuu

**4.4. Ukusanyaji wa fedha kwa njia ya mtandao, utafanywa kwa masharti yafuatayo;**

1.1.1 Hakuna kiongozi wa ngazi yoyote atakayekuwa na mamlaka ya kukusanya fedha kwa shughuli yoyote ya chama isipokuwa kwa utaratibu uliowekwa au kutolewa na Katibu Mkuu.

1.1.2 Fedha zitakazokusanywa kwa njia ya mtandao kwa ajili ya shughuli za chama lazima ziingizwe kwenye akaunti ya benki ya Chama itakayotolewa kwa ajili hiyo.

1.1.3 Fedha zitakazokusanywa kwa mifumo ya TEHAMA itakavyowekwa hazitatumika kwa shughuli yoyote isipokuwa kwa idhini ya Ofisi ya Katibu Mkuu

1.1.4 Mwongozo huu hautahusu fedha zitakazochangwa na vikundi vya kusaidiana katika shughuli za kijamii mathalani ugonjwa,misiba, harusi au shughuli zingine kama hizo.

1.1.5 Itakuwa ni marufuku kwa kiongozi yeyote wa chama kutumia jina la chama kuomba misaada ya kifedha kwa njia za TEHAMA kwa malengo binafsi.

## 5. Hitimisho

Mwongozo huu utatumika sanjari na utaratibu ulioainishwa kwenye Katiba na Kanuni za Chama.

# MWONGOZO WA MABARAZA YA CHAMA

# MWONGOZO WA BARAZA LA WAZEE WA CHADEMA

## UTANGULIZI

Kwa kuwa, CHADEMA ni Chama kinachoheshimu na kuzingatia mifumo na misingi ya haki, uhuru, usawa na Demokrasia katika jamii kwa makundi yote;

Kwa kuwa, tunaamini kwamba Wazee ndiyo Hazina ya Hekima na Busara katika jamii yoyote duniani kutokana na uzoefu, ubunifu na hekima zao, hivyo basi kifungu cha 7.8 na 7.8.3 cha Katiba ya CHADEMA ya mwaka 2006 [toleo la 2016] kimetoa mamlaka ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Chama likiwemo Baraza la Wazee wa CHADEMA (BAZECHA);

Hivyo basi, sisi Wajumbe wa Baraza la Wazee tuliohudhuria Mkutano Mkuu wa Baraza la Wazee na kwa kuzingatia umuhimu wa uanzishwaji wa Baraza letu, tumekubaliana kukaa kama Mkutano Maalumu wa kuandaa rasimu ya Mwongozo wa uendeshaji wa shughuli za Baraza la Wazee wa CHADEMA na kupendekeza kwa Baraza Kuu la Chama ili upitishwe na kuwa Mwongozo rasmi, wa kuongoza wazee kuanzia ngazi ya msingi mpaka Taifa.

**FASILI NA UFAFANUZI** Ufafanuzi

Maneno yafuatayo yanatumika ndani ya mwongozo huu na yatakuwa na maana au fasili ya ufafanuzi kama inavyoelekezwa hapa chini:-

‘‘Baraza’’ ina maana ya Baraza la Wazee wa Chadema **[BAZECHA].**

**‘Caucus ya Wazee’ –** Kundi maalum la ushauri, usuluhishi na Upatanishi kwa viongozi wa Chama ngazi ya msingi hadi Taifa.

**“Mwanachama wa Baraza”** ina maana mwanachama hai wa CHADEMA aliyetimiza au kuzidi miaka 50 ya kuzaliwa.

Sekretariat – Ni kikao cha Utendaji wa shughuli za kila siku kwa ngazi husika.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 JINA

Jina

1.1 Jina la Baraza litakuwa **Baraza la Wazee**

## 1.2 MADHUMUNI YA BARAZA LA WAZEE

Madhu muni, Jukumu na Kaulimbiu ya Baraza

Madhumuni ya Baraza la Wazee ni kuwa chombo kikuu cha ushauri wa busara na hekima utakaokiwezesha Chama kufikia na kuendeleza madhumuni yake ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

## 1.3 MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE

Baraza litatimiza madhumuni yake, kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kuwa chombo cha ushauri ngazi zote za Chama.
(b) Kuwa chombo cha utatuzi na usuluhishi wa migogoro ndani ya Chama.
(c) Kuwa chombo cha kupatanisha na kuunganisha viongozi.
(d) Kuhamasisha wazee ndani ya jamii kukipenda kujiunga na kukienzi Chama.
(e) Kubuni mipango na mikakati ya kuwahusisha wazee ndani ya jamii kutambua, viongozi bora kwenye

chaguzi za ndani ya Chama na za kiserikali.

(f) Kubuni na kushauri sera bora zinazolengakuwaingiza wazee ndani ya Chama.

(g) Kuunda ‘Caucus ya Wazee’ itakayokuwa na jukumu la kushauri viongozi wa Chama kuanzia ngazi ya Msingi hadi Taifa.

(h) Kuhamasisha wazee ndani na nje ya Chama kuwa na maadili yanayoweza kuvutia na kuigwa na jamii.

(i) Kushauriana na kushirikiana na watu wengine ndani na nje ya Chama kutetea maslahi ya wazee wote nchini.

**1.4** KAULI MBIU YA BARAZA :-
**“WAZEE” – “HAZINA YA HEKIMA NA BUSARA”**

Makao Makuu

## 1.5 MAKAO MAKUU YA BARAZA

1.5.1 Makao Makuu ya Baraza yatakuwa Dar es Salaam

1.5.2 Kutakuwa na Ofisi ya Baraza Zanzibar.

# SURA YA PILI

## 2.0 UANACHAMA

Taratibu za Uana chama wa Baraza

2.1 Mwanachama wa CHADEMA ambaye ametimiza miaka 50 au zaidi ya kuzaliwa na anayekubaliana na masharti ya Mwongozo wa Baraza anaweza kuwa mwanachama wa ‘Baraza la Wazee’.

## 2.2 HAKI ZA MWANACHAMA

(a) Kila mwanachama ana haki ya kuchagua kiongozi au kuchaguliwa kuongoza kwa mujibu wa Mwongozo wa Baraza.

(b) Kila mwanachama ana haki ya kujitetea au kutoa maelezo mbele ya kikao cha Baraza kinachomhusu.

(c) Kila mwanachama ana haki ya kukata rufaa kwenye kikao cha juu, kama hakubaliani na uamuzi uliofikiwa katika kikao kilichotoa maamuzi.

(d) Kila mwanachama ana haki ya kunufaika na fursa zitokanazo na shughuli na michakato mbalimbali inayoendeshwa na Baraza kwa mujibu wa Mwongozo huu.

(e) Kila mwanachama ana haki ya kujielimisha juu ya haki na wajibu wake ndani ya Baraza.

## 2.3 ADA NA KIINGILIO

Kutakuwa na ada na kiingilio kwa kila mwanachama wa Baraza kwa viwango vitakavyowekwa na Baraza.

## 2.4 WAJIBU WA MWANACHAMA

(a) Kujua haki zake kwa kuielewa katiba ya Chama na Mwongozo wa Baraza.

(b) Kushiriki kikamilifu shughuli mbalimbali za Baraza.

(c) Kuhudhuria vikao vyote vya Baraza vinavyomhusu.

(d) Kutekeleza miongozo na maagizo mbalimbali ya Baraza.

(e) Kuendelea kujielimisha juu ya masuala mbalimbali yanayohusu siasa, uchumi na jamii, kutumia elimu yake kuendeleza Baraza na Chama.

(f) Kila mwanachama ana wajibu wa kulilinda, kulitangaza na kulitetea Baraza wakati wowote na popote inapofaa.

(g) Ni wajibu wa kila Mwanachama kulipa kiingilio na ada ya Mwaka na michango yote ya Baraza na ile ya Chama.

(h) Kutetea na kueneza Falsafa na Itikadi ya Chama.

(i) Kushirikiana na wanachama na viongozi wengine wote katika kutekeleza sera na mipango mbalimbali ya Baraza na Chama.

(j) Kuwa tayari kupambana na aina yoyote na namna yoyote dhidi ya uonevu, ukandamizaji na ubaguzi ndani ya Baraza, Chama na umma.

## 2.5 UKOMO WA UANACHAMA:-

Mwanachama atakoma kuwa mwanachama endapo yafuatayo yatatokea:-

(a) Kwa kujiuzulu mwenyewe kwa hiari yake.

(b) Kufariki

(c) Kuachishwa ama kufukuzwa uanachama ngazi yoyote husika kutokana na kukosa sifa za kuwa mwanachama wa Baraza au Chama.

(d) Hatakuwa amelipa ada ya uanachama kwa muda wa miezi 36 mfululizo bila sababu, inayokubaliwa na Chama.

(e) Endapo mwanachama ataonekana kuwa na mwenendo usioendana na Itikadi ya Chama.

## 2.6 MISINGI, MAADILI NA ITIFAKI YA VIONGOZI WA BARAZA

(a) Misingi, Maadili na itifaki ya Baraza la Wazee wa CHADEMA litaendeshwa kwa kufuata na kuzingatia Misingi ya Utu, Uzalendo, Uadilifu, Uwajibikaji, Umakini, Ubunifu, Haki, Usawa, Uwazi na Umoja kama ilivyoainishwa kwenye Katiba na Kanuni za Chama za Mwaka 2006 [toleo la 2016].

(b) Kiongozi atakayekwenda kinyume na maadili haya atahesabiwa kuwa amevunja maadili ya Baraza.

# SURA YA TATU

## 3.0 MUUNDO, VIKAO NA UONGOZI WA BARAZA

Muundo wa Vikao na Uongozi

### 3.1 MUUNDO WA BARAZA

Kutakuwa na ngazi saba za uongozi wa Baraza nazo ni:-

(a) Msingi
(b) Tawi
(c) Kata/ Wadi
(d) Wilaya
(e) Mkoa
(f) Kanda
(g) Taifa

3.2 Uundaji wa ngazi moja ya juu utafanyika baada ya kuwa na muundo wa uongozi ngazi ya chini kwa angalau 50% ya maeneo ya kiutawala yanayostahili kuwa na muundo wa uongozi wa kikatiba kwa ngazi hiyo.

3.3 Kwa kuzingatia kifungu cha 3.2 cha Mwongozo huu, ngazi ya juu ya Baraza itateua kamati ya muda itakayokuwa na wajibu wa kuratibu shughuli za Baraza kwa kuwaunganisha wanachama katika eneo lisilo na uongozi wa kikatiba hadi pale utakapopatikana.

## 3.4 VIKAO VYA UONGOZI WA BARAZA

**Kutakuwa na vikao vya aina mbili:-**

(a) Mkutano Mkuu wa Baraza

(b) Kamati ya Utendaji ya Baraza

## 3.5 UHALALI WA VIKAO KWA NGAZI ZOTE

Ili kikao kiwe halali akidi ya asilimia hamsini (50%) ya wajumbe halali wa kikao husika itahitajika.

## 3.6 UCHAGUZI WA VIONGOZI NA MUDA WA UONGOZI.

### 3.6.1 Uchaguzi wa Uongozi

Uchaguzi wa Uongozi utazingatia taratibu na sifa za uongozi kama zilivyoainishwa kwenye Kanuni za Chama.

### 3.6.2 Muda wa Uongozi

(a) Kila uongozi uliochaguliwa au kuteuliwa wakati wa uchaguzi mkuu wa Baraza utaongoza kwa kipindi cha miaka mitano.

(b) Kiongozi aliyechaguliwa au kuteuliwa baada ya uchaguzi atashika wadhifa wake hadi kipindi cha uchaguzi mkuu kinachofuata.

(c) Kiongozi aliyemaliza muda wa uongozi ana haki ya kugombea na kuchaguliwa tena mradi awe ametimiza masharti ya kuchaguliwa kuwa kiongozi.

(d) Muda wa uongozi unaweza kufupishwa kama mamlaka iliyochagua au kuteua itaamua hivyo.

## 3.8 KUKOMA KWA UONGOZI

(a) Kwa kiongozi kujiuzulu kwa hiari yake

(b) Kwa kiongozi kuachishwa uongozi au kufukuzwa uanachama.

(c) Kwa kiongozi kushindwa kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Kanuni au Maadili ya Chama.

(d) Kwa kiongozi kufariki.

(e) Kiongozi atakoma kushika Uongozi wa ngazi ya chini mara baada ya kuchaguliwa au kuteuliwa kushika uongozi wa ngazi ya juu ndani ya Baraza.

## 3.9 KUZIBA NAFASI WAZI ZA UONGOZI

Nafasi yoyote ya uongozi inayokuwa wazi itazibwa kwa kuzingatia taratibu zilizopo kwenye ibara 6.3.5 ya Katiba ya Chama.

## 3.10 MAMLAKA ZA NIDHAMU NA UWAJIBIKAJI.

Kiongozi aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu ataweza kusimamishwa uongozi kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 6.3.6 ya Katiba ya Chama.

# SURA YA NNE

## 4.0 NGAZI, UONGOZI NA MAJUKUMU YA VIKAO

## 4.1 NGAZI YA MSINGI

(a) Ngazi ya msingi itakuwa ngazi ya chini kabisa katika muundo wa Baraza.

(b) Ngazi ya msingi itaundwa kwenye maeneo kama yalivyoainishwa kwenye Ibara 7.1.1 ya Katiba ya Chama.

### 4.1.1 Viongozi wa Msingi

Ngazi hii itakuwa na viongozi wafuatao:-

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu
(d) Mweka Hazina

4.1.2 Viongozi hawa watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Msingi kwa kuzingatia taratibu zilizopo kwenye Kanuni za Chama.

4.1.3 Ngazi ya Msingi itakuwa na vikao vifuatavyo:

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji ya Baraza

4.1.4 Mkutano Mkuu ndio utakuwa kikao kikuu cha Baraza katika ngazi hii na utafanyika mara mbili kwa mwaka. Mikutano maalumu/ dharura inaweza kuitishwa wakati wowote kufuatana na mahitaji ya wakati husika.

4.1.5. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Msingi watakuwa ni wanachama wote wa Baraza katika Msingi husika

**4.1.6 Kazi za Mkutano Mkuu za Msingi**

(a) Kupitia na kupitisha mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Msingi.

(b) Kutoa mapendekezo kuhusu mwelekeo wa ujazaji nafasi za uongozi zilizo wazi.

(c) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati ya Utendaji.

(d) Kupokea ushauri, maelekezo na kutekeleza maagizo ya ngazi ya juu ya Baraza au Chama.

(e) Kumchagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina.

(f) Kuthibitisha majina ya wazee wasiopungua watatu na wasiozidi watano kuwa 'Caucus ya Wazee' wa ngazi hiyo kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Utendaji.

4.1.7 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Msingi watakuwa ni wajumbe waliotajwa kwenye kifungu cha 4.1.1 cha Mwongozo huu.

4.1.8 Kamati ya Utendaji ya Msingi itakutana mara kwa mara kutokana na mahitaji ya Baraza isipokuwa italazimika kukutana mara moja kwa mwezi.

**4.1.9 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Baraza ngazi ya Msingi ni:-**

(a) Kuratibu shughuli za kila siku za Baraza kwa ngazi yao.

(b) Kuandaa Mkutano Mkuu wa Msingi.

(c) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu wa Msingi majina ya wazee wanachama wa Baraza wasiopungua watatu na wasiozidi watano kuwa wajumbe kwenye 'Caucus ya Wazee' ngazi ya msingi.

(d) Wajumbe wa Caucus ya Wazee watatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) Uanachama wa Baraza

(ii) Wenye haiba yenye ushauri wa hekima na busara katika jamii

(iii) Waweze kupatikana kwa ushauri wakati wowote watakapohitajika.

(iv) Wanakubalika na kuheshimiwa na jamii.

(v) Wasiwe viongozi wa Kamati ya Utendaji.

(e) Kushiriki kampeni za wagombea wa Chama kwenye chaguzi za serikali katika maeneo yao.

(f) Kusimamia nidhamu ya wanachama wa Baraza na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(g) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya Baraza

(h) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu jina la Katibu wa Msingi

(i) kuweka kumbukumbu za wanachama katika eneo la msingi.

(j) Kushawishi wananchi kipindi cha uchaguzi wajiandikishe na kuwapigia kura wagombea CHADEMA.

## 4.2 NGAZI YA TAWI

(a) Uundwaji wa ngazi hii utafuata taratibu zilizowekwa na ibara 7.2.1 ya Katiba ya Chama

(b) Ngazi ya Tawi ya Baraza la Wazee itakuwa na

viongozi wafuatao:-

(i) Mwenyekiti
(ii) Makamu Mwenyekiti
(iii) Katibu
(iv) Mweka Hazina

4.2.1 Viongozi hawa watachaguliwa na Mkutano Mkuu ngazi ya Tawi kwa kuzingatia taratibu za uchaguzi zilizopo kwenye Kanuni za Chama.

4.2.2 Ngazi ya Tawi itakuwa na vikao vifuatavyo:

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji

4.2.3 Mkutano Mkuu wa Tawi ndio kikao kikuu cha Baraza ngazi hii na utahudhuriwa na wanachama wote wa Baraza kwenye Tawi.

4.2.4 Mkutano Mkuu ngazi ya Tawi utafanyika mara mbili kwa mwaka. Mikutano maalumu au ya dharura inaweza kuitishwa wakati wowote na Kamati ya Utendaji kadri itakavyolazimu.

**4.2.5 Kazi za Mkutano Mkuu wa Tawi:-**

(a) Kupitia na kupitisha mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Tawi.
(b) Kutoa mapendekezo kuhusu mwelekeo na ujazaji nafasi za uongozi zilizo wazi.
(c) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati ya Utendaji.
(d) Kupokea na kufanyia kazi maagizo toka ngazi za juu.
(e) Kumchagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka hazina wa Tawi.
(f) Kuchagua wajumbe wawili (kwa kuzingatia jinsia) wawakilishi wa Tawi kwenye Mkutano Mkuu wa Kata.
(g) Kuteua Katibu wa Tawi
(h) Kuthibitisha majina ya wajumbe wa 'causus ya Wazee' kwa kuzingatia masharti yaliyopo kwenye kifungu cha 4.1.9 (c) cha Mwongozo huu.

**Kamati ya Utendaji ya Baraza Ngazi ya Tawi**

4.2.6 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi watakuwa ni wale walioainishwa kwenye Kifungu 4.2 (b) cha Mwongozo huu.

4.2.7 Kamati ya Utendaji ya Tawi itakutana mara moja kwa mwezi lakini vikao maalum vinaweza kuitishwa kutokana na mahitaji.

**4.2.8 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Baraza ngazi ya Tawi ni:-**

(a) Kuendesha shughuli za kila siku za Baraza katika eneo lake

(b) Kuandaa Mkutano Mkuu wa ngazi ya Tawi

(c) Kushiriki kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali.

(d) Kusimamia nidhamu ya wanachama wa Baraza na kuchukua hatua kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(e) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na mtumizi ya Baraza.

(f) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.(g) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu wa Tawi majina ya wajumbe wa 'Caucus ya Wazee' kwa kuzingatia masharti yalipo kifungu 4.1.9 (c) cha Mwongozo huu.

## 4.3 Ngazi ya Kata/Wadi

4.3.1 Ngazi hii itaundwa kwa kuzingatia taratibu za ibara 7.3.1 ya Katiba ya Chama.

4.3.2 Viongozi wa Kata/Wadi watakuwa wafuatao:-

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu
(d) Naibu Katibu
(e) Mweka Hazina

4.3.3 Ngazi ya Kata/Wadi itakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji

4.3.4 Wajumbe wa Mkutano Mkuu Kata/Wadi:-

(a) Mwenyekiti na Makamu wake

(b) Katibu na Naibu wake

(c) Mweka Hazina

(d) Wawakilishi toka kila Tawi ndani ya Kata/Wadi

(e) Wenyeviti na Makatibu wa matawi ndani ya Kata

(f) Waweka Hazina wa kila Tawi

4.3.5 Mkutano Mkuu wa Kata utakutana mara mbili kila mwaka. Mikutano maalumu/dharura inaweza kuitishwa wakati wowote kwa kadri itakavyolazimu.

**4.3.6 Kazi za Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi**

(a) Kupitia na kupitisha mapendekezo ya Kamati ya Utendaji

(b) Kumchagua Mwenyekiti na Makamu wake.

(c) Kuchagua Katibu na Naibu Katibu.

(d) Kumchagua Mweka Hazina.

(e) Kuwachagua wajumbe wawakilishi wawili wa Kata kwenda Mkutano Mkuu wa Wilaya kwa kuzingatia jinsia.

(f) Kujaza nafasi za uongozi zilizo wazi. (g)

Kutoa maelekezo kwa Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi.

(h) Kusikiliza na kutolea maamuzi au mapendekezo kwa ngazi ya juu kuhusu masuala ya kinidhamu kwa wanachama na viongozi wa Baraza.

(i) Kuidhinisha Programu ya Baraza ngazi ya Kata.

(j) Kuthibitisha majina ya Wajumbe wa Caucus ya Wazee ngazi ya Kata/Wadi kwa kuzingatia masharti yaliyo kwenye kifungu cha 4.1.9(c) cha Mwongozo huu.

4.3.7 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata/ Wadi ni wale waliotajwa kwenye kifungu 4.3.2 cha Mwongozo huu.

**4.3.8 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Kata/Wadi ni kama ifuatavyo:-**

(a) Kuandaa Mkutano Mkuu wa Kata.

(b) Kuhamasisha wazee kujiunga na Chama kwa kueneza Itikadi, Falsafa na Sera za Chama.

(c) Kushiriki kampeni za Uchaguzi wa wagombea wa Chama katika chaguzi za Serikali.

(d) Kusimamia nidhamu ya wanachama wa Baraza katika ngazi yao na kuchukua hatua za kinidhamu zinazostahili.

(e) Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya ngazi yao.

(f) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama.

(g) Kupendekeza majina ya wazee wa 'Caucus ya Wazee' kwa mujibu wa kifungu 4.1.9 (c) cha Mwongozo huu.

## 4.4 Ngazi ya Wilaya

4.4.1 Ngazi ya Wilaya itakuwa na miundo miwili:

(a) Wilaya zenye Jimbo moja la uchaguzi.

(b) Wilaya zenye zaidi ya Jimbo moja la uchaguzi.

4.4.2 Ngazi ya Wilaya yenye Jimbo moja la uchaguzi itaundwa kwa kuzingatia masharti ya ibara 7.4.1 ya Katiba ya Chama.

4.4.3 Viongozi wa Wilaya yenye Jimbo moja la uchaguzi

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu na
(d) Naibu Katibu
(e) Mweka Hazina

4.4.4 Vikao vya Wilaya zenye Jimbo moja la uchaguzi

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji ya Baraza

4.4.5 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya yenye Jimbo moja

(a) Viongozi wa Jimbo / Wilaya waliotajwa kwenye ibara ya 4.4.3 ya mwongozo huu.
(b) Viongozi wa kila Kata katika Wilaya Sawa sawa na Ibara 4.3.2 ya mwongozo huu
(c) Wawakilishi wawili toka kila Kata ya Wilaya kwa uwiano wa mwanaume mmoja na mwanamke mmoja.

4.4.6 Mkutano Mkuu wa Wilaya utafanyika mara moja kila mwaka. Mikutano maalumu inaweza kuitishwa wakati wowote kutokana na mahitaji.

4.4.7 Kazi za Mkutano Mkuu wa Wilaya ni pamoja na:-

(a) Kupitia na kupitisha mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Baraza.
(b) Kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti
(c) Kuchagua Katibu na Naibu Katibu wa Wilaya.
(d) Kumchagua Mweka Hazina.
(e) Kujaza nafasi za uongozi zilizowazi kwenye Kamati ya Utendaji.
(f) Kutoa mwongozo/maelekezo kwa Kamati ya Utendaji.
(g) Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu masuala ya kinidhamu kwa wanachama na uongozi wa Baraza.
(h) Kuidhinisha Program ya Baraza ngazi ya Wilaya.
(i) Kuthibitisha majina ya wajumbe wa 'Caucus ya Wazee' Ngazi ya wilaya kwa kuzingatia masharti yaliyopo kwenye kifungu 4.1.9 (c) cha Mwongozo huu.

4.4.8 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Baraza Wilaya ni wajumbe walioainishwa kwenye kifungu 4.4.3 cha Mwongozo huu.

4.4.9 Kamati ya Utendaji ya Wilaya itakutana mara nne kwa mwaka. Mikutano maalumu inaweza kuitishwa pale itakapohitajika.

**4.4.10 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Baraza Wilaya ni:-**

(a) Kuandaa mikutano mikuu ya Wilaya.
(b) Kuhamasisha wazee kujiunga na chama kwa kuendeleza Falsafa, Itikadi na Sera za Chama.
(c) Kutoa mapendekezo ya mikakati ya uendeshaji Baraza ngazi ya Wilaya.
(d) Kusimamia utekelezaji wa program za Baraza.
(e) Kuendesha shughuli za kila siku za Baraza ngazi ya Wilaya.
(f) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wanaotoka kwenye Jimbo/ Wilaya husika

## 4.5 Wilaya Zenye Zaidi ya Jimbo Moja la Uchaguzi

4.5.1 Kutakuwa na Kamati ya Uratibu Wilaya

**4.5.2 Wajumbe wa Kamati ya Uratibu Wilaya watakuwa:-**

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu na Naibu Katibu
(d) Wenyeviti kutoka kila Jimbo la uchaguzi la Wilaya.

(e) Makatibu kutoka kila Jimbo la Uchaguzi la Wilaya.

### 4.5.3 Kazi za Kamati ya Uratibu Wilaya.

(a) Kuwa kiunganishi baina ya majimbo yote ndani ya wilaya.
(b) Kutoa ushauri wa kiutendaji kwa majimbo yote ndani ya Wilaya.
(c) Kuwa kiunganishi baina ya kila Jimbo ndani ya Wilaya na serikali kuu/serikali ya mitaa kuhusu masuala ya Wazee.
(d) Kushiriki shughuli za kampeni za wagombea Urais/Mwenza katika majimbo yote ya Wilaya.

(e) Kuratibu na kutoa taarifa kwa ngazi za juu za Baraza juu ya hali ya kisiasa, kijamii na kiutawala ngazi ya Wilaya husika.

## 4.6 Ngazi ya Mkoa

4.6.1 Ngazi ya Mkoa itaundwa katika eneo la Mkoa wa kiutawala wa serikali kwa mujibu wa ibara 7.5.1 ya Katiba ya Chama.

4.6.2 Ngazi ya Mkoa itakuwa na kikao kimoja tu cha Kamati ya Uratibu ya Mkoa

4.6.3 Wajumbe wa Kamati ya Uratibu ya Mkoani:
(a) Mwenyekiti
(b) Katibu

(c) Mweka Hazina
(d) Wenyeviti wote toka wilaya zote za mkoa husika
(e) Makatibu wote toka Majimbo/Wilaya katika Mkoa husika. Kwa Mkoa wa Dar Miongozo itatolewa.
(f) Wajumbe wa Baraza Kuu kutoka Jimbo/ Wilaya husika.

**4.6.4 Kazi za Kamati ya Uratibu ya mkoa ni:-**

(a) Kuwa kiunganishi baina ya Wilaya kichama.
(b) Kutoa ushauri wa kiutendaji kwa Wilaya zote ndani ya Mkoa.
(c) Kushiriki shughuli za kampeni za wagombea Ubunge, Rais / Mwenza katika Majimbo yote ya Mkoa.
(d) Kuratibu na kutoa taarifa kwa ngazi za juu za Baraza kuhusu hali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutawala ngazi ya Mkoa.
(e) Kuteua wajumbe wa 'Caucus ya Wazee' wa Mkoa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4.1.9 (c) cha Mwongozo huu. 'Caucus ya Wazee' ya Mkoa itashughulikia pia Wilaya ambazo zina Jimbo zaidi ya Moja.
(f) Kuchagua Viongozi walioanishwa katika kifungu cha 4.6.3 (a), (b), na (c).
(g) Kuchagua wawakilishi wawili wa Mkutano Mkuu Taifa wa Baraza kwa uwiano wa kijinsia.

## 4.7. Ngazi ya Kanda

Ngazi ya Kanda itaundwa katika eneo la Kanda za kiutawala ndani ya Chama. Ngazi hii itakuwa na Kamati ya Uratibu ya Kanda.

### 4.7.1 Viongozi wa Kamati ya Uratibu ya Kanda watakuwa;

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu
(d) Mweka Hazina

### 4.7.2 Wajumbe wa Kamati ya Uratibu ya Kanda:

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Wenyeviti wa Kamati za Uratibu za Mikoa ndani ya Kanda
(d) Mweka Hazina
(e) Makatibu wa Kamati za Uratibu za Mikoa ndani ya Kanda
(f) Wajumbe wa Kamati Kuu Wazee waliosajiliwa kwenye msingi ndani ya Kanda
(g) Wabunge/Wawakilishi Wazee ndani ya Kanda
(h) Madiwani Wazee wasiozidi watatu (03) watakaochaguliwa na Kamati ya Uratibu ya Kanda

**4.7.3 Kazi za Kamati ya Uratibu ya Kanda:**

Kazi za Kamati ya Uratibu ya Kanda ni;

(a) kuwa kiunganishi baina ya Mikoa ya Kichama ndani ya Kanda.

(b) Kuchagua Viongozi wa Baraza wa Kanda kama walivyotajwa kwenye kifungu cha 4.7.1

(c) Kutoa ushauri wa kiutendaji kwa mikoa yote ndani ya Kanda.

(d) Kushiriki shughuli za kampeni za Wagombea wa Kiserikali.

(e) Kuratibu na kutoa taarifa kwa ngazi za juu za Baraza.

## 4.8 Ngazi ya Taifa

4.8.1 Ngazi ya Taifa itaundwa katika eneo lote la Jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa mujibu wa ibara 7.7.1 ya Katiba ya Chama.

4.8.2 Viongozi wakuu ngazi ya Taifa watakuwa wafuataao:-

(a) Mwenyekiti

(b) Makamu Mwenyekiti (Bara)

(c) Makamu Mwenyekiti (Zanzibar)

(d) Katibu Taifa

(e) Naibu Katibu Taifa (Bara)

(f) Naibu Katibu Taifa (Zanzibar)

(g) Mweka Hazina

**4.8.3 Ngazi ya Taifa itakuwa na vikao vifuatavyo-:**

(a) Mkutano Mkuu

(b) Kamati ya Utendaji

(c) Kutakuwa na kikao cha Sekretarieti.

**4.8.4 Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni:-**

(a) Mwenyekiti

(b) Makamu Mwenyekiti (Bara)

(c) Makamu Mwenyekiti (Zanzibar)

(d) Katibu Taifa

(e) Naibu Katibu Taifa (Bara)

(f) Naibu Katibu Taifa (Zanzibar)

(g) Wenyeviti wa Mikoa

(h) Makatibu wa Mkoa

(i) Viongozi wa Chama Taifa ambao ni wazee na Viongozi wastaafu wa Baraza ngazi ya Taifa.

(j) Wabunge ambao ni Wazee

(k) Wawakilishi wawili wazee kutoka kila mkoa kwa uwiano wa jinsia.

(l) Mweka hazina.

(m) Kutakuwa na kikao cha Sekretarieti.

(n) Wajumbe wawakilishi wa Wzee kwenye Baraza Kuu na Mkutano Mkuu.

4.8.5 Mkutano Mkuu utafanyika mara moja kwa miaka mitano. Mikutano maalum inaweza kuitishwa wakati wowote pale inapohitajika.

### 4.8.6 Kazi za Mkutano Mkuu wa Baraza Taif ni:

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa Baraza Taifa

(b) Kuchagua Makamu Wenyeviti (Bara na Zanzibar)

(c) Kumchagua Katibu Mkuu(d) Kuchagua Manaibu Katibu Wakuu wa Baraza.

(e) Kuwachagua wajumbe watano kuwakilisha Baraza Kuu kwa uwiano wanne

(4) toka Bara na mmoja (1) toka Zanzibar.

(f) Kuwachagua wajumbe ishirini (20) kwa uwiano wa wajumbe kumi (15) Bara na watano (5) Zanzibar, kuwakilisha wazee kwenye Mkutano Mkuu wa Chama kwa kuzingatia uwiano wa Kanda.

(g) Kujadili na kupitia taarifa za Kamati ya Utendaji

(h) Kujadili na kupitisha Mpango wa muda mrefu wa Baraza

(i) Kujadili na kuthibitisha mapendekezo ya maboresho ya Mwongozo wa Baraza na kuwasilisha kwenye Baraza Kuu la Chama.

### 4.8.7 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa ni;

(a) Mwenyekiti

(b) Makamu Mwenyekiti Taifa (Bara na Zanzibar)

(c) Wajumbe wote wa Sekretarieti

(d) Viongozi Wakuu Wazee wa Chama Ngazi ya Taifa

(e) Viongozi wazee wa Serikali Ngazi ya Taifa.

(f) Wenyeviti wa Kanda Wataalam watatu watakaoteuliwa na Mwenyekiti baada ya kushauriana na Katibu Mkuu.

4.8.8 Kamati ya Utendaji ya Baraza itakutana mara moja kwa mwaka na vikao maalum vinaweza kuitishwa kila inapohitajika.

**4.8.9 Kazi za Kamati ya Utendaji ni:-**

(a) Kutoa ushauri kwa Viongozi Wakuu wa Chama pale inapohitajika

(b) Kusimamia shughuli za Baraza za kila siku.

(c) Kuteua Mweka Hazina

(d) Kuandaa Mikutano Mikuu ya Baraza Taifa.

(e) Uandaaji wa taarifa mbalimbali kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Baraza.

**4.8.10 Wajumbe wa Sekretarieti Taifa:**

(a) Katibu Taifa ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti.

(b) Naibu Katibu Mkuu Bara

(c) Naibu Katibu mkuu Zanzibar

(d) Mtunza Hazina

(e) Wataalamu watatu Wazee watakaoteuliwa na Mwenyekiti baada ya kushahuriana na Katibu taifa, na angalau mmoja awe Mwanamke.

**4.8.11 Kazi za sekretarieti:**

(a) (a) Kuwa chombo cha utendaji wa shughuli za kila siku za Baraza

(b) Kuteua wataalam kwa ajili ya shughuli za kila siku za Baraza.

(c) Kuandaa mikakati mbalimbali ya uendeshaji wa Baraza na kuwasilisha kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(d) Kuandaa program mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi

(e) Kutoa mapendekezo ya uteuzi mbalimbali zinazofanywa na kamati ya Utendaji

(f) Kutekeleza maamuzi na maelekezo ya kamati ya utendaji na uongozi.

(g) Kuandaa ajenda na Nyaraka kwa ajili ya vikao vya kamati ya utendaji

# SURA YA TANO

## 5.0 MAJUKUMU YA VIONGOZI

### 5.1 Wenyeviti

(a) Kuongoza vikao vya Baraza.
(b) Kuwa msemaji mkuu wa Baraza.
(c) Kuwakilisha Baraza kwa kadri inavyohitajika.
(d) Kuhamasisha wazee katika maeneo yake kukipenda, kukienzi na kujiunga na Chama.
(e) Kuhamasisha wazee kugombea uongozi waChama na serikali.

#### 5.1.2 Makamu Wenyeviti

(a) Ni wasaidizi wakuu wa wenyeviti
(b) Kuongoza vikao kama mwenyekiti hayupo
(c) Kumwakilisha mwenyekiti kila inapobidi

### 5.3 Makatibu

(a) Watakuwa watendaji wakuu wa shughuli za Baraza.
(b) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kujenga vikundi vya kiuchumi na kitamaduni.
(c) Kuweka kumbukumbu ya maamuzi ya Baraza na kuhakikisha yanafikishwa ngazi husika.

(d) Kuunda na kusimamia vikundi vya Wazee ili kufanikisha chaguzi za serikali ili Chama
kipate viongozi imara wanaokubalika katika jamii.

(e) Kubuni mbinu mbalimbali za kuunda timu za uhamasishaji na uenezi wa Sera na Falsafa ya Chama katika jamii.

**5.4 Waweka Hazina**

(a) Kusimamia mali na fedha za Baraza kwa mujibu wa taratibu zinazowekwa na Chama.

(b) Kubuni mikakati ya kuongeza mapato ya Baraza.

(c) Kuhakikisha wanachama wa Baraza wanalipa ada na viingilio.

(d) Kusimamia ukaguzi wa fedha za Baraza ngazi husika.

(e) Kuanda taarifa za mapato na matumizi ya mwaka.

**5.5 Caucus ya Wazee**

(a) Kuwa chombo cha ushauri ngazi husika.

(b) Kutoa ushauri wa awali ili kuzuia migogoro baina ya viongozi ndani ya Baraza na Chama.

(c) Kuwa chombo cha usuluhishi na upatanishi ndani ya Chama katika ngazi husika.

(d) Kuwa chombo cha ushauri kuhusu sifa muhimu zinazotakiwa na jamii kwa wagombea katika chaguzi za Chama na serikali.

# MWONGOZO WA BARAZA LA WANAWAKE WA CHADEMA (BAWACHA)

Utangulizi na Fasili na Ufafanuzi

## UTANGULIZI

Kwa kuwa, CHADEMA ni Chama kinachozingatia haki, uhuru na demokrasia katika jamii;
Kwa kuwa, tunaamini kwamba wanawake ndiyo chimbuko la maendeleo katika Taifa lolote lile duniani kutokana na nguvu, ubunifu na wingi wao, hivyo basi kifungu cha 7.8 na 7.8.3 cha Katiba ya Chadema ya mwaka 2006 kimetoa mamlaka ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Chama likiwemo Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA);
Hivyo basi, sisi wajumbe wanawake tuliohudhuria Mkutano Mkuu wa Chama na kwa kuzingatia umuhimu wa uanzishwaji wa Baraza letu, tumekubaliana kukaa kama Mkutano Maalumu wa kuandaa rasimu ya Mwongozo wa uendeshaji wa shughuli za wanawake wa CHADEMA na kupendekeza kwa Baraza Kuu la Chama ili upitishwe na kuwa mwongozo rasmi, wa kuongoza wanawake kuanzia ngazi ya msingi mpaka Taifa.

## FASILI NA UFAFANUZI

Maneno yafuatayo yanatumika ndani ya mwongozo huu yatakuwa na maana au fasili ya ufafanuzi kama inavyoelekezwa hapa chini:-

**“Baraza”** ina maana ya Baraza la Wanawake waCHADEMA (BAWACHA).

**“Mwanachama wa Baraza”** ina maana ya mwanachama hai wa CHADEMA ambaye amejiunga na Baraza la Wanawake kwa kutimiza masharti ya Katiba ya Chama na Mwongozo huu.
**“Viongozi wa Serikali”** ina maana ya viongozi wa Serikali wanaotokana na Chama.

# SURA YA KWANZA

Jina na Makao Makuu

1.0 **JINA**

1.1 Jina la Baraza litakuwa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA)

1.2 **MAKAO MAKUU YA BARAZA**

1.2.1 Makao Makuu ya Baraza yatakuwa Dar es Salaam na patakuwa na ofisi ya Baraza Zanzibar.

# SURA YA PILI

**2.0 MAADILI NA ITIFAKI**

Kauli mbiu ya Baraza

2.1 Maadili na Itifaki ni kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba na Kanuni za Chama

**2.2 KAULI MBIU YA BARAZA:**

2.2.1 Kauli mbiu ya Baraza itakuwa **"Wanawake" – "Chimbuko la Maendeleo".**

2.2.2 Kauli mbiu hii itakwenda sambamba na kauli mbiu ya Chama kwa kuanza na ile ya

Chama:"**CHADEMA"** – "VEMA"

"**CHADEMA"** – "MABADILIKO YA KWELI, UHURU WA KWELI"
"**WANAWAKE"** – "CHIMBUKO LA MAENDELEO"

# SURA YA TATU

## 3.0 LENGO KUU LA BARAZA

Malengo ya Baraza la Wanawake

Kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika masuala yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

## 3.1 KAZI ZA BARAZA

(a) Kutambua, kusimamia, kuendeleza na kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika masuala mbalimbali yanayohusu mustakabali wa Chama.

(b) Kusimamia, kuendeleza na kulinda maslahi ya Chama.

(c) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kueneza sera za Chama kupitia wanawake ndani ya jamii.

(d) Kubuni na kupanga mafunzo ya wanawake kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

(e) Kuhamasisha wanawake kushiriki

kugombeauongozi katika uchaguzi wa Chama na chaguzi za serikali.

(f) Kuhamasisha na kuunda timu za wanawake kwa ajili ya kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za serikali.

(g) Kuanzisha na kuendeleza ukuaji wa vikundi vya michezo na sanaa kwa wanawake wa Chama kama chombo cha mvuto kwa wanawake wengi kujiunga.

(h) Kushirikiana na wanawake wa vyama vingine vya siasa na visivyo vya siasa ndani na nje ya nchi kwa maelekezo ya chama.

# SURA YA NNE

Masharti ya Uana-chama wa Baraza

**4.0 Uanachama**

4.1 Uanachama wa Baraza la Wanawake inazingatia kuwa:

4.1.1 Lazima uwe mwanachama wa CHADEMA.

4.1.2 Utimize masharti ya Mwongozo huu..

**4.2 Haki na Wajibu**

4.2.1 Haki, wajibu kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba ya Chama.

**4.3 Kukoma kwa Uanachama**

4.3.1 Kukoma uanachama ni kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba ya Chama Ibara 5.4

4.3.2 Asipotimiza masharti ya Mwongozo huu.

**4.4 Ada na Kiingilio**

4.4.1 Kutakuwa na ada na kiingilio kwenye Baraza kama itakavyopangwa na Kamati ya Utendaji ya Baraza ngazi ya Taifa.

# SURA YA TANO

## 5.0 Muundo

Ngazi za Uongozi

5.1 Kutakuwa na ngazi saba za uongozi wa Baraza kama ifuatavyo:

(a) Msingi
(b) Tawi
(c) Kata/wadi
(d) Jimbo la uchaguzi/wilaya
(e) Mkoa
(f) Kanda
(g) Taifa

5.2 Uundaji wa ngazi moja ya juu utafanyika tu baada ya kuwa na Muundo wa uongozi katika ngazi ya chini kwa angalau 50% ya maeneo ya kiutawala yanayostahili kuwa na muundo wa uongozi wa Baraza katika ngazi hiyo.

5.3 Kwa kuzingatia kifungu 5.2 cha Mwongozo huu, ngazi ya juu ya Baraza itateua kamati ya muda kwa muda usiozidi mwaka mmoja itakayokuwa na wajibu wa kuratibu shughuli za Baraza na kuwaunganisha wanachama wanawake katika eneo lisilo na uongozi mpaka wanapofikia uwezo wa kuwa na uongozi.

# SURA YA SITA

## 6.0 VIKAO NA UONGOZI WA BARAZA

Vikao na Uongozi

6.1 Kutakuwa na vikao vitatu:-

(a) Vikao vya maamuzi, hii ni mikutano mikuu ya kila ngazi ya muundo wa Baraza.

(b) Vikao vya uongozi vinavyosimamia utekelezaji wa maamuzi ya Chama na Mikutano Mikuu ya Baraza. Hivi ni vikao vya Kamati ya Utendaji.

(c) Vikao vya utendaji wa shughuli za kila siku za Chama na Baraza vitakuwa vya utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya vikao vya uongozi. Hivi ni vikao vya sekretarieti ya kila ngazi.

## 6.2 UHALALI WA VIKAO KWA NGAZI ZOTE

(a) Kutahitajika akidi ya asilimia hamsini (50%) ya wajumbe wote halali wa ngazi husika.

(b) Isipokuwa vikao vya kurekebisha au kubadilisha Mwongozo au vya uchaguzi na sera za Baraza vitahitaji akidi ya asilimia sabini na tano (75%)

## 6.3 VIONGOZI NA WATENDAJI WA BARAZA

(a) Viongozi wa kuchaguliwa na mikutano mikuuya kila ngazi.

(b) Viongozi wa kuchaguliwa/kuteuliwa na vikao vya uongozi yaani Kamati za Utendaji za Baraza.

(c) Watendaji

## 6.4 MAJUKUMU YA VIONGOZI

**6.4.1** Majukumu ya viongozi kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Chama kifungu cha 7.7 pamoja na Mwongozo huu.

**i. Wenyeviti wa Baraza**

(a) Kuongoza vikao vya Baraza

(b) Kuwa msemaji Mkuu wa Baraza

(c) Kuwakilisha Baraza kwa kadiri inavyohitajika

(d) Kuhamasisha jamii kuunga mkono Baraza na Chama kwa ujumla

(e) Kuhamasisha jamii na wanachama wa Baraza kushiriki kugombea uongozi katika Chaguzi za Chama, Baraza na za kiserikali.

**ii. Makamu wenyeviti**

(a) Watakuwa wasaidizi wa wenyeviti

(b) Kuongoza vikao kama mwenyekiti hayupo

(c) Kumwakilisha mwenyekiti kila inapobidi.

**iii. Makatibu wa Baraza**

(a) Watakuwa watendaji wakuu wa shughuli za Baraza

(b) Watatakiwa kubuni na kutekelezamikakati ya kujenga vikundi katika jamii vya kiuchumi/kitamaduni au vinginevyo kama itakavyoamuliwa.

(c) Kuunda, kukuza na kusimamia vikundi vya jamii ili kufanikisha chaguzi za Chama, Baraza na za kiserikali ili Chama kipate viongozi imara wanaokubalika na jamii.

(d) Kubuni mbinu mbalimbali za uhamasishaji na uenezi wa Sera, Itikadi na Falsafa ya CHADEMA katika makundi mbalimbali ndani ya jamii.

(e) Kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza.

**iv. Manaibu Katibu Mkuu wa Baraza**

Watakuwa wasaidizi wa Makatibu wa Baraza

kwa mujibu wa Kanuni za Chama

**v. Waweka Hazina wa Baraza**

(a) Kusimamia mali na fedha za Baraza kwa kuzingatia Kanuni za fedha za Chama.

(b) Kubuni mikakati ya kuongeza mapato ya Baraza

(c) Kusimamia ukaguzi wa fedha, mapato na matumizi ya mwaka katika ngazi husika na kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya mwaka.

**vi. Mratibu wa Uenezi**

(a) Atahusika na propaganda ndani ya Baraza,
(b) Kuratibu shughuli zote za habari na uenezi ndani ya Baraza.
(c) Msimamizi mkuu wa vifaa vya uenezi vya Baraza
(d) Atakaimu nafasi ya Naibu Katibu wakati Naibu Katibu hayupo.
(e) Atakuwa mratibu wa Itifaki katika shughuli zote za Baraza kwa ngazi husika.
(f) Atatoa maelekezo kwenye ngazi za chini kuhusu masuala ya habari na uenezi.

## 6.5 MUDA WA UONGOZI

Muda wa uongozi utakuwa kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba ya Chama Ibara 6.3.2.

## 6.6 KUKOMA UONGOZI

Kukoma kwa uongozi ni kama ilivyoanishwa ndani ya Katiba ya Chama Ibara 6.3.4.

## 6.7 KUZIBA NAFASI WAZI ZA UONGOZI

Kamati ya Utendaji ya kila ngazi itaziba kwa muda nafasi yoyote ya kiongozi aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa ngazi husika kwa mujibu wa ibara ya 6.3.5 ya Katiba ya Chama.

## 6.8 UTARATIBU WA UCHAGUZI

Uchaguzi wa viongozi utazingatia taratibu na sifa za uongozi kama zilivyofafanuliwa katika Kanuni za Chama.

## 6.9 KUREKEBISHA TAREHE YA UCHAGUZI MKUU WA BARAZA

Tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Baraza inaweza kurekebishwa kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba ya Chama Ibara 6.3.3.

## 6.10 MAMLAKA YA NIDHAMU NA UWAJIBISHAJI

Mamlaka ya nidhamu na uwajibishaji ndani ya Baraza itakuwa kama ilivyoainishwa ndani ya katiba ya Chama Ibara 6.3.6

## 6.11 KAMATI YA USULUHISHI NA USHAURI YA BARAZA

(a) Kamati ya usuluhishi na ushauri itaundwa na wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi saba watakaoteuliwa na Kamati ya Utendaji ya ngazi husika.

(b) Majukumu ya Kamati yatakuwa ni:-

- (i) Kuwa chombo cha usuluhishi baina ya viongozi au wanachama
- (ii) Kuwashauri viongozi katika masuala mbalimbali yanayohusu Baraza

# SURA YA SABA

## 7.0. NGAZI, UONGOZI NA MAJUKUMU YA VIKAO

## 7.1 NGAZI YA MSINGI

Ngazi ya chini katika muundo wa Baraza ni ngazi ya msingi. Ngazi hii itaundwa katika eneo la kitongoji kwa vijijini, eneo la Mtaa wa Chama mijini kwa Tanzania Bara na katika eneo la Shehiya Tanzania Zanzibar yenye wanachama wanawake.

### 7.1.1 VIONGOZI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa uenezi
(d) Wajumbe watatu (3) waliochaguliwa na Mkutano Mkuu.

### 7.1.2 VIKAO

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji

### 7.1.3 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA MSINGI

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Msingi watakuwa wanachama wote wanawake katika ngazi ya Msingi.

### 7.1.4 KAZI ZAMKUTANO MKUU WA MSINGI

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kumchangua Katibu
(c) Kumchagua Mratibu wa Uenezi
(d) Kuchagua wajumbe watatu (3) kuingia Kamati ya Utendaji ya Msingi
(e) Kujadili kuzingatia masuala ya kijamii/ wanawake katika eneo la Msingi.
(f) Kikao cha Mkutano Mkuu kitafanyika mara nne kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

### 7.1.5 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uenezi
(d) Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu
(e) Viongozi wanawake wa Chama na wale wa Serikali ya Kitongoji/ Mtaa/Shehiya kupitia CHADEMA, ndani ya Msingi.

### 7.1.6 KAZI ZA WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI

(a) Kuendesha shughuli za kila siku za wanawake katika eneo la msingi.
(b) Kuandaa mikutano mikuu ya msingi
(c) Kutambua wanawake wanaoweza kugombea uongozi ndani ya chama na serikali na kuwashawishi wagombee.

(d) Kuhamasisha wanawake kujiunga na Chama pamoja na Baraza la Wanawake.(e) Kupokea

maagizo ya mikakati ya Chama itokanayo na vikao na kuitekeleza kwa ufanisi.

(f) Kubuni mikakati ya kuwajengea wanawake uwezo kisiasa, kiuchumi na kijamii.

(g) Kuweka kumbukumbu za wanachama wanawake katika eneo la msingi.

(h) Kuhimiza uanzishwaji wa miradi na vikundi vya hamasa.

(i) Wakati wa uchaguzi kushawishi wananchi nyumba kwa nyumba wakajiandikishe na kupata idadi yao pia kuwashawishi wakipigie kura Chama.

(j) Kutekeleza maazimio ya vikao vya Mkutano Mkuu wa Msingi.

(k) Kuwatambua na kuwakuza kisiasa vijana wa kike ndani ya Msingi.

(l) Kamati ya Utendaji itakutana mara sita kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

## 7.2 Ngazi ya Tawi

Tawi litaundwa katika kila eneo la Kijiji, Mtaa au Shehiya.

### 7.2.1 VIONGOZI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uenezi

## 7.2. VIKAO

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji ya Tawi

### 7.2.3 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAWI

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi watakuwa ni Wanawake wote wanachama waliopo kwenye Tawi husika.

### 7.2.4 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA TAWI

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kuchagua wajumbe wawili kuwakilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Kata
(c) Kujadili taarifa ya Kamati ya Utendaji ya tawi na kutoa maamuzi au maelekezo/ mwongozo wa utekelezaji.
(d) Kuzingatia na kutoa maelekezo/ mwongozo wa utekelezaji wa maamuzi na maagizo ya vikao vya juu.
(e) Kuzingatia na kujadili utekelezaji wa mipango ya wanawake kijamii kujikwamua kiuchumi na kisiasa.
(f) Kuchagua wajumbe watatu wa kuingia Kamati ya Utendaji ya Tawi.
(g) Kutoa mapendekezo ya awali ya wagombea wa nafasi za wajumbe wa viti maalum kwenye Serikali za Vijiji/ Mitaa na kuwasilisha kwenye Kamati ya Utendaji ya Chama ngazi ya Tawi.
(h) Mkutano Mkuu wa Tawi utakutana mara mbili kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

### 7.2.5 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA TAWI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uenezi
(d) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu (wawili wawakilishi kata, watatu Kamati ya Utendaji).
(e) Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa mwanamke anayetokana na Chama.

### 7.2.6 KAZI YA KAMATI YA UTENDAJI YA TAWI

(a) Kumchagua Mratibu wa Uenezi.
(b) Kupendekeza majina mawili ya Katibu na kupeleka Kamati ya Utendaji ya Kata kwa uteuzi.
(c) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Tawi.
(d) Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa mipango mbalimbali ya wanawake.
(e) Kuweka kumbukumbu ya orodha ya wanachama wa Baraza.
(f) Kubuni mipango mbalimbali na kuanzisha miradi ya kiuchumi.
(g) Kufanya utafiti wa kero za wanawake na kuziwekea mikakati ya kuzikwamua.
(h) Kutambua na kushawishi wanawake kugombea uongozi wa Chama na serikali.

(i) Kusimamia chaguzi ngazi ya msingi.
(j) Kutekeleza maamuzi ya vikao
(k) Kuandaa taarifa za Baraza la Tawi na kuziwasilisha ngazi ya Kata.

(l) Kupanga na kufanya ziara kwenye Tawi

(m) Kamati ya Utendaji itakutana mara nne kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

## 7.3 Ngazi ya Kata/Wadi

7.3.1 Ngazi ya Kata/Wadi itaundwa pale ilipo Kata/Wadi, ya kiserikali

### 7.3.2 VIONGOZI WA KATA/WADI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uenezi
(d) Mweka Hazina
(e) Diwani mwanamke anayetokana na Chama anayeishi kwenye Kata
(f) Mbunge mwanamke anayeishi katika Kata husika na anayetokana na Chama.

### 7.3.3 **VIKAO VYA KATA/WADI**

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji

### 7.3.4 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KATA

(a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya Kata
(b) Wajumbe wawili kutoka kila Tawi
(c) Viongozi wa serikali wanawake wanaotokana na Chama ngazi ya Kijiji/Mtaa na Kata

(d) Viongozi wa Chama wanawake kutoka kila Tawi na katika ngazi ya Kata

### 7.3.5 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA KATA

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kuchagua wajumbe wawili kuwakilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo/ Wilaya
(c) Kujadili taarifa ya Kamati ya Utendaji ya Kata na kutoa maamuzi au maelekezo/ mwongozo wa utekelezaji.
(d) Kuzingatia na kutoa maelekezo/ mwongozo wa utekelezaji wa maamuzi na maagizo ya vikao vya juu.
(e) Kuzingatia na kujadili utekelezaji wa mipango ya wanawake kijamii kujikwamua kiuchumi na kisiasa.
(f) Kuchagua wajumbe wawili wa kuingia Kamati ya Utendaji ya Kata.
(g) Kutoa mapendekezo ya uteuzi wa awali wa wagombea udiwani wa viti maalum na kuwasilisha kwenye Kamati ya Utendaji ya Chama ngazi ya Kata na Baraza ngazi ya Jimbo/Wilaya.
(h) Mkutano Mkuu wa Kata utakutana mara mbili kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

### 7.3.6 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA KATA/WADI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu

(c) Mratibu wa Uenezi
(d) Mweka hazina
(e) Diwani mwanamke anayetokana na Chama anayeishi katika Kata husika.
(f) Wajumbe Wawili wawakilishi Jimbo.
(g) Wajumbe wawili waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata

7.3.7 **KAZI ZA KAMATI ZA UTENDAJI ZA KATA/ WADI**

(a) Kumchagua Mratibu wa Uenezi na Mweka Hazina
(b) Kupendekeza majina mawili ya Katibu kwa Kamati ya Utendaji ya Jimbo
(c) Kuteua makatibu wa matawi
(d) Kusimamia chaguzi za matawi
(e) Kuandaa orodha ya majina ya wagombea udiwani viti maalum na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Kata
(f) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu
(g) Kuandaa mapendekezo ya mikakati na shughuli za uendeshaji na utekelezaji wake
(h) Kuweka kumbukumbu sahihi za wanawake
(i) Kutekeleza maamuzi ya vikao vya juu
(j) Kuhamasisha wanawake wajiunge na Chama na wagombee uongozi ndani ya Chama na serikali
(k) Kufanya ziara za mara kwa mara kwenye Matawi.
(l) Kuunda kamati mbalimbali kusaidia kampeni za wagombea wakati wa uchaguzi wa kiserikali.

(m) Kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanawake waliokiuka maadili naKanuni za Chama
(n) Kushawishi uanzishaji wa miradi ya kiuchumi katika jamii
(o) Kufanya mahusiano mema na mashirika na vikundi vya kijamii ndani ya Kata husika.
(p) Kamati ya Utendaji itakutana mara nne kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

## 7.4 **Ngazi ya Wilaya/Jimbo**

7.4.0 Ngazi ya Wilaya itaundwa mahali ilipo wilaya ya kiserikali.

### 7.4.1 VIONGOZI WA JIMBO/ WILAYA ZENYE JIMBO MOJA LA UCHAGUZI – :

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uenezi
(d) Mweka Hazina

### 7.4.2 VIKAO VYA JIMBO/WILAYA ZENYE JIMBO MOJA LA UCHAGUZI

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji
(c) Sekretarieti

### 7.4.3 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA JIMBO/WILAYA YENYE JIMBO MOJA

(a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji
(b) Wenyeviti wa Baraza wa Kata ndani ya Jimbo/Wilaya

(c) Makatibu wa Kata wa Baraza ndani ya Jimbo/Wilaya

(d) Wajumbe wawili wanawake waliochaguliwa kutoka kila Kata.

(e) Madiwani wote wanawake kwenye Jimbo/ Wilaya husika

### 7.4.4 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA JIMBO/ WILAYA

(a) Kumchagua Mwenyekiti

(b) Kumchagua Katibu

(c) Kumchagua Mratibu wa Uenezi

(d) Kumchagua Mweka Hazina

(e) Kuchagua wajumbe watatu watakaoingia Kamati ya Utendaji

(f) Kujadili taarifa za Kamati ya Utendaji na kutoa maamuzi au maelekezo ya utekelezaji

(g) Kupiga kura ya awali kwa wagombea udiwani viti maalum na kuwasilisha orodha yenye mapendekezo kwenye Kamati ya Utendaji ya Chama ngazi ya Jimbo/Wilaya na Baraza ngazi ya Taifa.

(h) Kupiga kura ya awali kwa wagombea ubunge viti maalum na uwakilishi viti maalum.

(i) Kuzingatia na kutoa maelekezo ya utendaji kwa Kamati ya Utendaji kuhusu maamuzi na maagizo ya vikao vya juu.

(j) Mkutano Mkuu utakutana mara moja kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

### 7.4.5 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA WILAYA ZENYE JIMBO MOJA.

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uenezi
(d) Mweka Hazina
(e) Mbunge/Mwakilishi mwanamke atokanaye na Chama ambaye Msingi wake uko kwenye Jimbo husika.

(f) Meya/Naibu Meya au Mwenyekiti/ Makamu Mwenyekiti mwanamke anayetokana na Chama.

(g) Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu

### 7.4.6 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI YA WILAYA ZENYE JIMBO MOJA.

(a) Kuteua makatibu wa kata/wadi
(b) Kuandaa orodha ya majina ya wagombea wa viti maalum na kupeleka kwenye Mkutano Mkuu.
(c) Kuchukua hatua za kinidhamu kwa viongozi wa ngazi za chini
(d) Kuweka orodha/kumbukumbu sahihi za wanachama wanawake na kutolea taarifa ngazi za juu
(e) Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Baraza Jimbo/Wilaya
(f) Kutambua kero zilizopo na kuziwekea mikakati ya kuzitatua
(g) Kujadili taarifa za sekretarieti na kutoa maamuzi au maelekezo ya utekelezaji

(h) Kusimamia chaguzi ngazi ya Kata/Wadi

(i) Kufanya ziara za mara kwa mara katika ngazi za chini.

(j) Kupendekeza majina ya makatibu wa Jimbo/ Wilaya.

(k) Kuteua wajumbe wawili wa Sekretariet kutokana na utaalam wao.

(l) Kamati ya Utendaji itakutana mara nne kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

### 7.4.7 WAJUMBE WA SEKRETARIETI

(a) Katibu

(b) Mratibu wa Uenezi

(c) Mweka Hazina

(d) Wajumbe wawili walioteuliwa na Kamati ya Utendaji.

### 7.4.8 KAZI ZA SEKRETARIETI

(a) Ndicho chombo cha Utendaji wa kazi za kila siku

(b) Kuweka kumbukumbu (orodha) ya wanachama wa Baraza.

(c) Kutekeleza majukumu yatakayotolewa na vikao vya juu

(d) Kutoa mapendekezo namna ya uboreshaji shughuli za wanawake kwa ngazi za juu

(e) Kubuni miradi ya kijamii na kiuchumi na kuisimamia kwa ufanisi

(f) Kutafuta marafiki na wadau mbalimbali ili kusaidia shughuli za Baraza.

(g) Kuandaa mafunzo kwa viongozi ngazi za chini.

(h) Kupendekeza kwa Kamati ya Utendaji majina mawili ya wataalamu wataoteuliwa kuwa wajumbe wa sekretarieti watakaoteuliwa kwa utaalam wao.

(i) Kuratibu shughuli za Madiwani wa Viti Maalum

(j) Sekretarieti itakutana angalau mara moja kila mwezi au wakati wowote inapobidi.

## 7.5 WILAYA YENYE JIMBO LA UCHAGUZI ZAIDI YA MOJA

Kutakuwa na Kamati ya Uratibu ya Wilaya.

7.5.1 Kamati ya Uratibu ya wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti

(b) Katibu

(c) Wenyeviti na Makatibu kutoka kila Jimbo

(d) Mbunge mwanamke anayetoka katika Wilaya husika.

(e) Meya/Naibu Meya au Mwenyekiti/ Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri mwanamke anayetokana na Chama.

## 7.5.2 KAZI ZA KAMATI YA URATIBU

(a) Kuwa kiunganishi baina ya majimbo na Wilaya.

(b) Kutoa ushauri wa kiutendaji kwa majimbo ndani ya Wilaya

(c) Kuratibu shughuli za kampeni kwa wagombea wa Chama katika chaguzi za Serikali.
(d) Kuratibu na kutoa taarifa kwa ngazi za juu, juu ya hali ya kisiasa, kijamii na kiutawala
(e) Kumchagua Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Uratibu
(f) Kamati ya Uratibu itakutana angalau mara moja kwa mwaka au wakati wowote inapobidi.

## 7.6 NGAZI YA MKOA

7.6.1 Ngazi ya Mkoa itaundwa katika kila eneo la Mkoa wa kiutawala wa Serikali au kama itakavyoamuliwa vinginevyo na Chama.

Ngazi hii itakuwa na Kamati ya Uratibu ya Mkoa.

### 7.6.2 WAJUMBE WA KAMATI YA URATIBU YA MKOA

Wajumbe wa kamati ya uratibu watakuwa ni:

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mweka hazina
(d) Wabunge wa Viti Maalum wanaowakilisha Mkoa husika
(e) Wabunge/Wawakilishi wa majimbo wanawake wanaotoka katika Mkoa husika.
(f) Wenyeviti kutoka kila Wilaya/Jimbo.

(g) Makatibu kutoka kila wilaya/Jimbo
(h) Waweka Hazina wa Wilaya/Jimbo
(h) Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu kutoka kila Jimbo/ Wilaya
(i) Viongozi Wanawake wa Umoja wa Madiwani
(j) Meya/Naibu Meya au Mwenyekiti/ Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mwanamke anayetokana na Chama.

### 7.6.3 KAZI ZA KAMATI YA URATIBU YA MKOA

(a) Kuratibu shughuli za Baraza katika Mkoa
(b) Kupanga na kusimamia program za Baraza kimkoa
(c) Kupokea na kuamua rufaa mbali mbali za Baraza kutoka katika majimbo.
(d) Kuunganisha Baraza katika majimbo yote ndani ya Mkoa.
(e) Kusukuma utekelezaji wa shughuli za Baraza katika Mkoa
(f) Kuratibu na kusimamia shughuli za kujengea uwezo wanawake katika Mkoa husika
(g) kuratibu kura za maoni ya wagombea wa Udiwani na ubunge viti maalum katika Mkoa kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa
(h) Kuandaa na kuwasilisha orodha ya wagombea wa Udiwani na Ubunge Vitimaalum kwa mujibu wa Vigezo vilivyowekwa na kuviwasilisha ngazi ya Kanda
(i) Kuandaa mpango kazi wa Baraza katika Mkoa

(j) Kuhakikisha baraza katika majimbo yote ya Mkoa liko hai na imara.
(k) Kuthibitisha uteuzi wa Makatibu wa Wilaya/Jimbo na kupeleka kanda.
(l) Kumchagua Mwenyekiti na Mwekahazina wa Kamati ya Uratibu.

#### 7.6.4 VIKAO VYA KAMATI YA URATIBU YA MKOA

Kamati ya uratibu ya Mkoa itakutana mara moja kwa mwaka, Vikao maalum vinaweza kuitishwa wakati wowote.

## 7.7 NGAZI YA KANDA

Ngazi ya Kanda itaundwa katika eneo la Kanda za

kiutawala ndani ya Chama. Ngazi hii itakuwa na Kamati ya Uratibu ya Kanda.

#### 7.7.1 Baraza litakuwa na viongozi wafuatao katika ngazi ya Kanda:-

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu
(d) Mweka Hazina

#### 7.7.2 Kutakuwa na Kamati ya Uratibu ya Kanda

#### 7.7.3 Wajumbe wa Kamati ya Uratibu ya Kanda:

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti

(c) Katibu
(d) Mweka hazina
(e) Wenyeviti wa Kamati za Uratibu za Mikoa ndani ya Kanda
(f) Makatibu wa Kamati za Uratibu za Mikoa ndani ya Kanda
(g) Waweka hazina kutoka kila Mkoa ndani ya Kanda
(h) Wajumbe wa Kamati Kuu wanawake ambao msingi wao uko katika Kanda husika.
(i) Viongozi Wakuu wa BAWACHA Taifa ambao msingi wao uko ndani ya Kanda husika.
(j) Wabunge/Wawakilishi wanawake ndani ya Kanda husika.
(k) Viongozi wanawake wa Umoja wa Madiwani wa Kanda.

**7.7.4 Kamati ya Uratibu Kanda itakuwa na majukumu yafuatayo:-**

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kumchagua Makamu Mwenyekiti
(c) Kumchagua Katibu
(d) Kumchagua Mweka Hazina.
(e) Kuthibitisha Makatibu wa Kamati za Uratibu za Mikoa.
(f) Kutathmini hali ya kisiasa ya Wanawake ndani ya Kanda na Kutoa Ushauri kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa.
(g) Kupokea orodha ya wagombea udiwani na Ubunge Vitimaalum kutoka Kamati za Uratibu za Mikoa.

(h) Kuandaa orodha ya wagombea wa Udiwani na Ubunge Viti Maalum na kuziwasilisha ngazi ya Taifa.

## 7.8 NGAZI YA TAIFA

Ngazi hii itaundwa katika eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Viongozi wakuu ngazi ya Taifa watakuwa kama**

**ifuatavyo:-**

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Wenyeviti
(c) Katibu Taifa
(d) Naibu Katibu Taifa (Bara)
(e) Naibu Katibu Taifa (Zanzibar)
(f) Mweka Hazina
(g) Mratibu wa Uenezi

**7.8.1 Viongozi waliotajwa kwenye kifungu (b), (d), (e), (f), & (g) watakuwa wajumbe wa Baraza Kuu Taifa.**

### 7.8.2 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU

(a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji
(b) Wajumbe wa Kamati Kuu wanawake
(c) Wenyeviti wa Majimbo
(d) Wabunge wote Wanawake
(e) Viongozi Wanawake wa Chama Taifa
(f) Meya/Manaibu Meya, Wenyeviti/ Makamu Wenyeviti wa Halmashauri ambao ni wanawake

(g) Wajumbe watano (5) wanaowakilisha wanawake kwenye Baraza Kuu la chama.

(h) Viongozi wa Umoja wa Madiwani Taifa ambao ni wanawake

(i) Mwenyekiti na Katibu na Umoja wa Madiwani ngazi ya Kanda ambaye ni mwanamke.

(j) Wajumbe 20, wanaochaguliwa na Mkutano mkuu kwa mujibu wa kifungu cha 7.8.3 (d)

(k) Makatibu wa Mikoa

**7.8.3 KAZI ZA MKUTANO MKUU**

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa Baraza Taifa.

(b) Kumchagua Makamu Wenyeviti wa Baraza.

(c) Kuchagua wajumbe watano (5) kuingia Baraza Kuu la Chama kwa uwiano wanne (4) Bara na mmoja Zanzibar

(d) Kuchagua wajumbe ishirini (20) kwa uwiano wa wajumbe kumi na tano Bara na watano Zanzibar kuwakilisha wanawake kwenye Mkutano Mkuu wa Chama. Uwiano wa Kanda uzingatiwe.

(e) Kujadili taarifa za Kamati ya Utendaji na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji.

(f) Kujadili na kuamua mipango ya muda mrefu ya Baraza kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Utendaji.

(g) Kujadili na kuthibitisha mapendekezo ya mabadiliko ya Mwongozo wa Baraza ili kuwasilisha kwenye Baraza Kuu la Chama.

(h) Mkutano Mkuu wa Taifa utafanyika mara moja kwa miaka mitano na wakati wowote inapobidi.

### 7.8.4 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI TAIFA

(a) Mwenyekiti wa Baraza Taifa
(b) Makamu Wenyeviti wa Baraza Taifa (Bara na Zanzibar)
(c) Wajumbe wote wa Sekretarieti
(d) Wenyeviti wa Kanda
(e) Wajumbe watano wa Baraza Kuu wanaotokana na Baraza
(f) Wenyeviti wa wanawake wa Mikoa
(g) Makatibu wa wanawake wa Mikoa
(h) Wajumbe watano wa Baraza Kuu wanaowakilisha Baraza
(i) Wabunge watatu (3) wanawake watakaopendekezwa na kikao cha wabunge wenyewe.
(j) Wenyeviti wastaafu wa Baraza Taifa ambao ni wanachama hai wa Chama.

### 7.8.5 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI TAIFA

(a) Kumchagua Katibu wa Baraza Taifa
(b) Kuchagua Naibu Katibu wa Baraza Taifa (Bara)
(c) Kuchagua Naibu Katibu Mkuu wa Baraza (Zanzibar)
(d) Kumchagua Mratibu wa Uenezi.
(e) Kuthibitisha uteuzi wa Makatibu wa Kamati za Uratibu za Mikoa na Kanda.
(f) Kuteua Makatibu wa Kamati za Uratibu za Wilaya.
(g) Kujadili na kupendekeza taratibu za kupata wagombea Udiwani na Ubunge wa Viti Maalum.

(h) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu wa Baraza marekebisho ya Mwongozo wa Baraza.

(i) Kujadili na kuridhia programu za muda mfupi za Baraza kwa kuzingatia mapendekezo ya Sekretarieti.

(j) Kusimamia Utendaji kazi wa Sekretarieti

Taifa

(k) Kusimamia chaguzi za viongozi ngazi ya Kanda na Mkoa

(l) Kuwa mamlaka ya nidhamu kwa viongozi.

(m) Kupitia na kutoa maamuzi kuhusu rufaa za wagombea uongozi ndani ya Baraza.

(n) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu

(o) Kujadili na kupitisha Sera za Baraza

(p) Kuweka viwango vya ada, kiingilio na michango mbalimbali ya Baraza.

(r) Kuthibitisha Mweka Hazina

(s) Kamati ya Utendaji itakutana mara moja kwa mwaka au wakati wowote itakapobidi.

## 7.8.6 WAJUMBE WA SEKRETARIETI YA BARAZA TAIFA

(a) Katibu wa Baraza ambaye ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti
(b) Naibu Katibu (Bara)
(c) Naibu Katibu (Zanzibar)
(d) Mweka Hazina
(e) Mratibu wa Uenezi
(f) Wataalam wasiozidi watatu watakaoteuliwa na Kamati ya Utendaji kulinganana mahitaji ya Baraza.

## 7.8.7 KAZI ZA SEKRETARIETI

(a) Kupendekeza Mweka Hazina

(b) Kupendekeza wataalamu wasiozidi watatu wa kuingia kwenye Sekretarieti.

(c) Kufanya kazi za kila siku za Baraza

(d) Kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Utendaji juu ya rufaa za viongozi na wanachama.

(e) Kuandaa program na mikakati mbalimbali ya uendeshaji wa Baraza na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Utendaji.

(f) Kutoa mapendekezo ya uteuzi mbalimbali zinazofanywa na kamati tendaji na uongozi.

# SURA YA NANE

## 8.0 MAPATO YA BARAZA

Mapato ya Baraza yatatokana na:-
(a) Michango ya hiari ya wanachama
(b) Michango hiari ya marafiki wa ndani na nje ya nchi (c) Michango ya Chama
(d) Mapato yatokanayo na miradi ya Baraza
(e) Viingilio na ada za wanachama wa Baraza

# SURA YA TISA

## 9.0 MAMBO YA JUMLA KUHUSU

## 9.1 MAREKEBISHO YA MWONGOZO

Mapendekezo ya mabadiliko ya mwongozo yatafanywa na Sekretarieti kisha kupelekwa kwenye Kamati ya Utendaji na Mkutano Mkuu kabla ya kupitishwa na Baraza kuu la Chama.

## 9.2. KUKASIMU MADARAKA YA SHUGHULI ZA UTENDAJI

(a) Kamati ya Utendaji inaweza kukasimu madaraka yake kwa Sekretarieti kwa azimio la wingi wa kura za wajumbe wa kikao.

(b) Mkutano Mkuu wa Baraza unaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati ya Utendaji ya Baraza kwa azimio la wingi wa kura za wajumbe wa kikao

## 9.3 WANAWAKE WENYE ULEMAVU

9.3.1 Wanawake wenye ulemavu watazingatiwa kama itakavyoelekezwa na Katiba na Kanuni za Chama katika uwakilishi wa uongozi.

# SURA YA KUMI

## 10.0 NAMNA YA KUMPATA MBUNGE/MWAKILISHI NA DIWANI WA VITI MAALUM

10.1 Kamati ya Utendaji ya Baraza Taifa itaandaa mapendekezo ya vigezo, utaratibu na mchakato wa namna ya kumpata Diwani, Mbunge na Mwakilishi wa Viti Maalum na kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati Kuu ya Chama.

10.2 Mapendekezo yatakayoandaliwa na Kamati ya Utendaji Taifa yatazingatia Katiba, Kanuni na Mwongozo huu.

# MWONGOZO WA BARAZA LA VIJANA WA CHADEMA (BAVICHA)

## UTANGULIZI

Kwa kuwa, CHADEMA ni Chama kinachoheshimu, kuzingatia, na kufuata misingi ya demokrasia ikiwa ni pamoja na uhuru wa makundi mbalimbali ya kijamii likiwemo kundi la vijana;

Kwa kuwa, vijana ndio kundi linaloathirika zaidi na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii yanayojiri ndani na nje ya nchi;

Na kwa kuwa, vijana ndio chachu ya mabadiliko katika taifa lolote duniani kutokana na nguvu, ubunifu, ushawishi, uthubutu na wingi wao;

Hivyo basi, Kwa kuzingatia Ibara ya 7.8 ya Katiba ya Chama inayotoa mamlaka ya uanzishwaji wa mabaraza ikiwa ni pamoja na Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA);

Sisi wajumbe vijana tuliohudhuria Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama tumekubaliana kukaa kama Mkutano Mkuu Maalumu wa vijana kutunga Mwongozo huu wa Baraza la Vijana kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zote zinazohusu Baraza la Vijana kuanzia ngazi ya Msingi mpaka Taifa.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 JINA

Jina, Fasili ya Ufafanuzi na Makao Makuu ya Baraza

1.1 Jina la Baraza litakuwa Baraza la Vijana wa **CHADEMA (BAVICHA)** kama lilivyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 7.8.2 (a) ya Katiba ya Chama.

## 1.2 FASILI NA UFAFANUZI

**a)** **"Baraza"** maana yake ni Baraza la Vijana wa CHADEMA kama linavyoanzishwa chini ya Ibara 7.8.2 ( a) ya katiba ya Chama.

**b)** **"Chama"** maana yake ni CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CHADEMA).

**c)** **"Viongozi wa Serikali"** maana yake ni viongozi wa Serikali wanaotokana na Chama.

**d)** **"Katiba"** maana yake ni Katiba ya Chama

**e)** **"Viongozi",** ni viongozi wa baraza kwa mujibu wa Kanuni hizi.

f) CHASO (Chadema Students Organization) maana yake ni Mtandao wa wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya juu, Kati na Sekondari.

## 1.3 MAKAO MAKUU YA BARAZA

Makao makuu ya Baraza yatakuwa Dar es Salaam na patakuwa na ofisi ya Makao Makuu Zanzibar.

# SURA YA PILI

## 2.1 MISINGI, MAADILI, ITIFAKI NA KAULI MBIU

Misingi na Itifaki ya Baraza

a) **Misingi ya Baraza ni-:**
Baraza la Vijana la Chama litaendeshwa kwa kufuata na kuzingatia misingi ya Utu, Uzalendo, Uadilifu, Uwajibikaji, Umakini, Ubunifu, Haki, Usawa, Uwazi na Umoja.

## 2.2 KAULI MBIU YA BARAZA

2.2.1 Kauli mbiu ya baraza itakuwa
**"Vijana – Nguvu ya Mabadiliko"**

2.2.2 Kauli mbiu hii itakwenda sambamba na kauli mbiu ya Chama kwa kuanza na ile ya Chama:-

2.2.3 Hivyo kauli mbiu hizi zitatumika kama ifuatavyo

**CHADEMA – "Mabadiliko ya kweli, Uhuru wa kweli;**
**VIJANA – "Nguvu ya Mabadiliko"**

# SURA YA TATU

## 3.1 LENGO KUU LA BARAZA

Lengo na Kazi za Baraza

Kuhakikisha vijana wanatoa mchango thabiti katika kukuza na kuendeleza madhumuni ya Chama kwa maslahi na ustawi wa Taifa la Tanzania.

## 3.2 KAZI ZA BARAZA

(a) Kutambua, kusimamia, kuendeleza na kuhamasisha ushiriki wa vijana katika masuala ya siasa.

(b) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kueneza sera za Chama kupitia vijana ndani ya jamii.

(c) Kubuni, kupanga na kutekeleza mafunzo ya vijana kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii ili kujenga msingi imara wa ajira kwa kuongeza uwezo na fursa za kujiajiri.

(d) Kuandaa vijana kuwa viongozi imara wa Taifa.

(e) Kuanzisha na kurutubisha ukuaji wa vikundi vya sanaa na michezo kwa vijana.

(f) Kubuni na kueneza mipango na mikakati ya kudhibiti mienendo inayoweza kuathiri vijana kama vile UKIMWI na madawa ya kulevya.

(g) Kuwa mshauri na msemaji mkuu juu ya masuala yote yanayohusu vijana ndani na nje ya Chama.

(h) Kushiriki harakati mbalimbali za vijana ndani na nje ya nchi.

(i) Kujenga na kuendeleza umoja na mshikamano miongoni mwa vijana wa Taifa la Tanzania.

(j) Kuhamasisha na kutetea heshima na haki za watoto na vijana.

(k) Kulinda maadili, uthamini wa tamaduni na ustawi wa Elimu nchini.

(l) Kuhamasisha vijana kulinda na kusimamia matumizi bora ya rasilimali za nchi kwa manufaa ya Taifa.

# SURA YA NNE

## 4.0 UANACHAMA

Uana-chama wa Baraza

4.1 Kutakuwa na aina tatu za wanachama

4.1.1 **WANACHAMA WA KAWAIDA**

(a) Hawa ni vijana wenye umri kati ya miaka 18 na 35
(b) Watakuwa na kadi rasmi za Baraza
(c) Watakuwa na wajibu na haki zote zilizoainishwa katika Mwongozo huu
(d) Hawa ndio wanacharna rasmi wa

Baraza**4.1.2 WANACHAMA WA**

**HESHIMA**

(a) Hawa ni wanachama wa CHADEMA wenye umri zaidi ya miaka 35.
(b) Watapewa kadi maalumu ya Baraza
(c) Hawatakuwa na haki ya kushiriki michakato ya uchaguzi na uongozi ndani ya Baraza
(d) Watakuwa washauri wa Baraza
(e) Watapendekezwa na Sekretariet ya Baraza Taifa kutokana na mchango wao kwa Baraza na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji.

(f) Bila kuathiri fasili
(e) katika kifungu hiki Kamati ya Utendaji itaweka vigezo na taratibu za kuwateua wanachama wa heshima.

**4.1.3 HAKI ZA MWANACHAMA**

(a) Kila mwanachama ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi yoyote ya uongozi wa Baraza

(b) Kila mwanachama wa Baraza ana haki ya kujieleza na kujitetea mbele ya kikao cha Baraza kinachohusika na maamuzi husika

(c) Mwanachama ana haki ya kukata rufaa katika ngazi ya juu kwenye Baraza dhidi ya maamuzi yaliyotolewa juu yake.

(d) Kila mwanachama ana haki ya kunufaika na fursa rnbalimbali za Baraza.

(e) Mwanachama ana haki ya kushiriki vikao vya Baraza vinavyomhusu.

**4.3 WAJIBU WA MWANACHAMA**

(a) Kujielimisha kuhusu haki na wajibu wake kama mwanachama wa Baraza na chama.

(b) Kueneza na kutetea Itikadi, Falsafa na Madhumuni ya Chama.

(c) Kushiriki shughuli mbalimbali za Baraza na Chama kwa kujitolea au kuagizwa

(d) Kuhudhuria vikao vya Baraza vinavyomhusu.

(e) Kuendelea kujielimisha kuhusu masuala ya siasa, uchumi na jamii
(f) Kulipa ada na michango yote ya Baraza kwa mujibu wa maazimio ya Baraza
(g) Kushirikiana na viongozi na wanachama katika kutekeleza Sera na Mipango mbalimbali ya Chama
(h) Kuwa tayari kupambana na aina yoyote ya uonevu, ukandamizaji na ubaguzi wa aina yoyote ndani na nje ya baraza
(i) Kwa ujumla kuwa kijana mzalendo kwa Baraza, chama na Taifa.

## 4.4 **KUJIANDIKISHA UANACHAMA**

4.4.1 Ili kijana aruhusiwe kujiunga na BAVICHA ni lazima awe na sifa zifuatazo
(a) Awe mwanachama wa CHADEMA
(b) Awe na umri kati ya miaka 18 na 35
(c) Awe anakubaliana na misingi ya mwongozo wa BAVICHA

4.4.2 Kijana aliyekidhi matakwa hayo hapo juu, atanunua kadi ya uanachama wa BAVICHA.

## **4.5 UKOMO WA UANACHAMA**

4.5.1 Mwanachama wa Baraza atakoma kuwa mwanachama endapo mojawapo ya haya yafuatayo yatatokea

(a) Kwa kujiuzulu
(b) Kutokana na kufariki
(c) Kuachishwa ama kufukuzwa

uanachama

(d) Mwanachama atakapo fikisha umri zaidi ya miaka 35

(e) Hatakuwa amelipa ada ya uanachama kwa muda wa miezi 36 mfululizo

(f) Kwa ujumla kama hatokubaliana na misingi ya mwongozo wa BAVICHA sanjari na Ibara ya 5.4 mpaka 5.4.6 ya Katiba ya Chama

## 4.6 ADA YA UANACHAMA

(a) Kutakuwa na kiingilio kwa kila mwanachama

(b) Kutakuwa na ada ya uanachama

(c) Utaratibu wa ulipaji na viwango vya ada utapangwa na Kamati ya Utendaji Taifa.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA VIONGOZI

Utaratibu wa Uongozi

## 5.1 NGAZI ZA UONGOZI

Kutakuwa na ngazi saba (7) za uongozi

(a) Msingi
(b) Tawi
(c) Kata/Wadi
(d) Jimbo/Wilaya
(e) Mkoa
(f) Kanda
(g) Taifa

5.1.1 Uundaji wa ngazi moja utafanyika tu baada ya kuwa na muundo wa uongozi katika ngazi ya chini kwa angalau asilimia 50. Kwa kuzingatia kifungu 5.1 cha Mwongozo huu, ngazi ya juu ya Baraza itateua kamati ya muda itakayodumu kwa muda usiozidi miezi 12 na itakuwa na wajibu wa kuwaunganisha wanachama kwa kutoa huduma za kiuongozi katika eneo hilo mpaka uongozi utakapoundwa.

## 5.3 UONGOZI

Kutakuwa na aina tatu za viongozi;
(a) Viongozi wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu (b) Viongozi wa kuteuliwa na Kamati ya Utendaji
(c) Watendaji wa kuteuliwa na Sekretarieti

## 5.4 VIKAO NA UONGOZI WA BARAZA

### 5.4.1 Kutakuwa na vikao vitatu:-

(a) Vikao vya maamuzi, hii ni mikutano mikuu ya kila ngazi ya muundo wa Baraza.
(b) Vikao vya uongozi vinavyosimamia utekelezaji wa maamuzi ya Chama na Mikutano Mikuu ya Baraza, hivi ni vikao vya Kamati ya Utendaji.
(c) Vikao vya Utendaji wa shughuli za kila siku za chama na Baraza vitakuwa vya utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya vikao vya uongozi, hivi ni vikao vya Sekretarieti ya kila ngazi.

## 5.5 MAJUKUMU YA VIONGOZI

### 5.5.1 Majukumu ya Mwenyekiti

(a) Ndiye Mwenyekiti wa vikao vyote
(b) Ndiye msemaji mkuu wa Baraza
(c) Ndiye Kiongozi mkuu wa Baraza katika ngazi husika,
(d) Mwakilishi wa Baraza katika shughuli zote ambazo baraza limealikwa
(e) Majukumu haya yasomwe pamoja na Ibara ya 7.7.1 ya Kanuni za Uendeshaji wa Kazi za Chama.

### 5.5.2 Makamu Mwenyekiti

(a) Ndiye Msaidizi Mkuu wa Mwenyekiti

(b) Atatakiwa kufanya kazi zote chini ya Mwenyekiti

(c) Atakaimu nafasi ya Mwenyekiti wakati Mwenyekiti hayupo

### 5.5.3 Katibu

(a) Ndiye Mtendaji Mkuu wa Baraza katika kila Ngazi husika

(b) Ndiye Katibu wa Vikao vyote vya Baraza (c) Ataitisha vikao vyote vya Baraza

(d) Ndiye mwandaaji wa taarifa zote za Chama za Baraza

(e) Atakuwa mwandishi wa kumbukumbu zote za Vikao

(f) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kujenga vikundi katika jamii vyakiuchumi/kiutamaduni au vinginevyo kama itakavyoamuliwa na Kamati ya Utendaji.

(g) Kuanzisha, kukuza na kusimamia vikundi vya Vijana ndani ya jamii ili kufanikisha chaguzi za Chama, Baraza na za kiserikali ili Chama kipate viongozi imara wanaokubalika na jamii.

(h) Kubuni mbinu mbalimbali za uhamasishaji na uenezi wa sera, itikadi na falsafa ya CHADEMA katika makundi ya Vijana ndani ya jamii.

### 5.5.4 Manaibu Katibu Mkuu

Watakuwa wasaidizi wa Makatibu wa Baraza kwa mujibu wa Kanuni za Chama

### 5.5.5 Mweka Hazina

(a) Atateuliwa na Sekretariat na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji
(b) Kusimamia miradi ya Baraza,
(c) Bila kuathiri fasili (a) katika kifungu hiki Sekretariat itafanya uteuzi wa Mweka Hazina baada ya kupokea maombi kutoka kwa wanachama ndani ya Baraza.

### 5.5.6 Mratibu wa Uhamasishaji

(a) Atateuliwa na Sekretariat na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji
(b) Atahusika na propaganda ndani ya Baraza,
(c) Kuratibu shughuli zote za habari na uenezi ndani ya Baraza.
(d) Msimamizi mkuu wa vifaa vya uenezi vya baraza
(e) Atakaimu nafasi ya Naibu Katibu wakati Naibu Katibu hayupo.
(f) Atakuwa mratibu wa Itifaki katika shughuli zote za Baraza kwa ngazi husika.

(g) Atakuwa Mratibu wa Chemchem na Mitandao ya wanachama wa Baraza Vyuo Vikuu na Sekondari.

(h) Atatoa miongozo kwenye ngazi za chini kuhusu masuala ya habari na uenezi.

## 5.6 MAMLAKA ZA NIDHAMU NA UWAJIBISHAJI

(a) Bila kuathiri utaratibu wa nidhamu kama ulivyoainishwa katika ibara ya 6.3.6 ya Katiba ya Chama; mfumo na utaratibu wa mamlaka za uwajibikashaji ndani ya Baraza utakuwa kama ifuatavyo;

(i) Kiongozi wa Ngazi ya Msingi na Ngazi ya Utendaji ya Tawi

(ii) Kiongozi wa Tawi na Kamati ya Utendaji ya Kata

(iv) Kiongozi wa Jimbo/Wilaya na Kamati ya uongozi ya Mkoa

(v) Kiongozi wa Mkoa na Kamati ya Uongozi ya Kanda

(vi) Kiongozi wa Kanda na Kamati ya Utendaji ya Taifa

(vii) Kiongozi wa Taifa wa Baraza na Kamati Kuu baada ya kupokea mapendekezo kutoka Kamati ya Utendaji ya Taifa

(b) Bila kuathiri masharti ya kipengele cha (a) katika kifungu hiki, kiongozi yeyote anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa au kuachishwa uongozi na kikao cha juu ya ngazi yake ya uongozi.`

(c) Kiongozi aliyechukuliwa hatua za nidhamu na mamlaka yake ya nidhamu atakuwa na haki ya kukata rufaa ngazi ya juu ya ile ya mamlaka yake ya nidhamu na uamuzi wa ngazi hiyo utakuwa wa mwisho isipokuwa kwa viongozi waliochukuliwa hatua na Kamati ya Utendaji Taifa.

(d) Kiongozi aliyechukuliwa hatua za kinidhamu na Kamati ya Utendaji Taifa atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati Kuu ya chama na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(e) Rufaa yoyote lazima ikatwe katika muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kupokea rasmi kwa maandishi maamuzi ya mamlaka iliyotoa adhabu.

(f) Viongozi wa ngazi ya kitaifa waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wanaweza kusimamishwa uongozi na kufukuzwa uanachama endapo zaidi ya nusu ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa watapiga kura ya siri ya kufikia maamuzi hayo kwa kiongozi husika. Kamati ya Utendaji itakuwa na wajibu wa kuteua atakayeshika nafasi hiyo kwa muda hadi uamuzi wa mwisho utakapofanywa na Mkutano Mkuu.

(g) Hatua za dharura zinaweza kuchukuliwa ikiwa maslahi ya Baraza na chama yatakuwa hatarini kwa mujibu wa kifungu cha 6.5.2 cha kanuni za Uendeshaji kazi za Chama.

## 5.7 MUDA WA UONGOZI

Muda wa uongozi ni kama ilivyoainishwa ndani ya katiba ya chama, Ibara ya 6.3.2 kifungu (a),(b),(c) na (d).

## 5.8 KUZIBA NAFASI ZILIZO WAZI ZA UONGOZI

Kamati ya Utendaji ya kila ngazi itaziba nafasi ya kiongozi yeyote aliyechaguliwa na mkutano mkuu wa ngazi husika. Hakuna nafasi yoyote itakayozibwa au kukaimishwa ndani ya miezi sita kabla ya muda wa uchaguzi ndani ya Baraza.

## 5.9 KUKOMA KWA UONGOZI

(a) Kwa Kiongozi kujiuzulu
(b) Kwa kufukuzwa uongozi wa Baraza
(c) Kwa kufukuzwa uanachama wa CHADEMA
(d) Kwa kufariki

Kiongozi atakoma kushika uongozi wa ngazi ya chini pale tu atakapochaguliwa kushika uongozi wa ngazi ya juu ndani ya Baraza.

## 5.10 UCHAGUZI WA VIONGOZI

(a) Utaratibu wa uchaguzi wa viongozi utazingatia sifa na misingi ya uchaguzi kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni za Uendeshaji Kazi za Chama.

(b) Maombi ya uongozi yatafanywa kwa kujaza fomu maalum zilizoandaliwa na Sekretariat ya Baraza zilizoidhinishwa na Kamati Kuu ya Chama.

(c) Maombi ya uongozi yatafanywa na Mwanachama yeyote isipokuwa awe na umri usiozidi miaka 30 wakati wa uchaguzi husika.

(d) Majina ya wagombea wenye sifa zilizotakiwa yatapigiwa kura za siri na kikao kinachohusika na mshindi atapatikana kwa wingi wa kura zisizopungua 50% ya kura halali za wajumbe waliohudhuria kikao.

### 5.10.1 Uchaguzi wa Ngazi ya Taifa

Kamati ya Utendaji itateua watu watano kuunda kamati maalum ya uchaguzi wa Baraza;

(a) Wajumbe wa Kamati Maalum ya uchaguzi wanaweza kuteuliwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ambao si wagombea, na mwanachama yeyote wa chama ambaye Kamati ya Utendaji itaona anafaa.

(b) Kamati maalum ya uchaguzi itakuwa na jukumu la kuchambua na kupendekeza wagombea kwa kamati kuu ya Chama.

### 5.10.2 Kurekebisha Tarehe ya Uchaguzi

Taratibu za kubadilisha tarehe ya uchaguzi ni kama zilivyoainishwa ndani ya katiba ya chama, ibara ya 6.3.6

# SURA YA SITA

## 6.0 NGAZI, VIONGOZI VIKAO NA MAJUKUMU YA VIKAO

Vikao na Majukumu ya Uongozi

## 6.1 NGAZI YA MSINGI

Hii ndio ngazi ya chini kabisa katika muundo wa Baraza, itaundwa katika eneo lenye msingi wa Chama na katika maeneo maalumu hata kama hakuna msingi wa Chama.

### 6.1.1 VIONGOZI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uhamasishaji

### 6.1.2 VIKAO

Ngazi ya msingi itakuwa na vikao vya aina mbili

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Uongozi

### 6.1.3 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU

(a) Viongozi wote wa msingi kama walivyobainishwa katika kifungu cha 6.1.1 hapo juu

(b) Wanachama wote ndani ya

Msingi.**6.1.4 KAZI ZA MKUTANO MKUU**

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa Msingi
(b) Kumchagua Katibu wa Msingi”
(c) Kumchagua Mratibu wa uhamasishaji wa msingi
(d) Kujadili na kufanya maamuzi ya kimwelekeo wa Baraza katika ngazi husika

(e) Kupitisha programu rnbalimbali za Baraza katika ngazi ya msingi
(f) Kupitia taarifa za utekelezaji wa kamati ya uongozi
(g) Kuchagua wajumbe watatu wanaoingia kwenye kamati ya uongozi

6.1.5 Mkutano Mkuu ngazi ya msingi utakutana mara nne kwa mwaka.

6.1.6 **WAJUMBE WA KAMATI YA UONGOZI**

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa uhamasishaji
(d) Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu.
(e) Viongozi vijana wa Chama na wale wa serikali ya kitongoji kupitia CHADEMA ndani ya msingi.

**6.1.7 KAZI ZA KAMATI YA UONGOZI**

(a) Kuendesha shughuli za kila siku za baraza(b) Kutambua na kushawishi vijana kugombea katika chaguzi mbalirnbali za Chama na serikali.

(c) Kuandaa mikakati ya uhamasishaji vijana kujiunga na CHADEMA.
(d) Kutekeleza maazimio ya vikao vya Mkutano mkuu
(e) Kubuni mikakati ya kuwajengea vijana uwezo kisiasa, kiuchumi na kijamii ndani ya msingi.

(f) Kuhimiza uundaji wa vikundi vya kiuchumi na vile vya hamasa kwa Chama.

6.1.8 Kamati ya Utendaji ya Msingi itakutana mara moja kwa mwezi na kamati maalumu inaweza kukutana wakati wowote inapobidi.

## 6.2 Ngazi ya Tawi

Ngazi hii itaundwa katika kila eneo lenye Tawi la Chama na katika maeneo maalumu hata kama hakuna Tawi la Chama.

6.2.1 **VIONGOZI**

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa uenezi

6.2.2 **VIKAO**

Kutakuwa na vikao vya aina mbili
(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji

6.2.3 **WAJUMBE WA MKUTANO MKUU**

(a) Viongozi wote wa Tawi
(b) Wanachama wote wa BAVICHA ndani ya tawi

6.2.4 **KAZIZA MKUTANO MKUU**

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kumchagua Katibu wa Tawi”
(c) Kumchagua Mratibu wa uhamasishaji wa Tawi
(d) Kuchagua wajumbe wawili wa kuwakilisha tawi kwenye mkutano mkuu kata

(e) Kuchagua wajumbe watatu wa kuingia kwenye kamati tendaji
(f) Kujadili taarifa za kamati tendaji na kutoa mwelekeo wa tawi
(g) Kupitia na kupitisha programu za baraza katika tawi

6.2.5 Mkutao Mkuu wa tawi utakutana mara mbili kwa mwaka na Mkutano Mkuu maalumu utakutana kila inapobidi.

**6.2.6 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI**

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa Uhamasishaji
(d) Viongozi wote vijana ndani ya chama na wale wa serikali kupitia CHADEMA katika tawi.

(e) Wajumbe watatu wa kuchaguliwa na Mkutano mkuu tawi.6.2.7

**KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI**

(a) Kusimamia na kutekeleza maazimio ya Mkutano Mkuu

(b) Kumteua Mratibu wa uhamasishaji ngazi ya Msingi

(c) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya Mkutano Mkuu

(d) Kubaini changamoto zinazo wakabili vijana ndani ya tawi na kuzitafutia ufumbuzi

(e) Kubaini na kuhamasisha vijana kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama na serikalini

(f) Kubuni miradi ya kuwasaidia vijana kiuchumi

(g) Kusimamia uchaguzi ngazi ya Msingi (h) Kupanga na kufanya ziara kwenye

Misingi kuhamasisha harakati za vijana.

6.2.8 Kamati ya Utendaji itakutana mara sita kwa mwaka

## 6.3 NGAZI YA KATA/WADI

Ngazi hii itaundwa katika kila eneo lenye kata ya chama.

### 6.3.1 VIONGOZI WA KATA/WADI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa uhamasishaji
(d) Mweka hazina

### 6.3.2 VIKAO

Ngazi hii itakuwa na vikao viwili

(a) Mkutano Mkuu

(b) Kamati ya Utendaji

### 6.3.3 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU

(a) Viongozi wote wa kata kama walivyoainishwa, katika kifungu cha 6.3.1

(b) Wawakilishi wawili kutoka kila tawi

(c) Viongozi wa serikali vijana kupitia CHADEMA ngazi ya kitongoji, kijijii, Mtaa na Kata.

(d) Viongozi wa Chama vijana kutoka kila tawi na katika ngazi ya kata.

### 6.3.4 KAZI ZA MKUTANO MKUU

(a) Kumchagua Mwenyekiti

(b) Kumchagua Katibu wa Kata

(c) Kumchagua Mratibu wa uhamasishaji wa Kata

(b) Kuchagua wajumbe wawili kuwakilisha kata jimboni

(c) Kuchagua wajumbe watatu wanaoingia kwenye kamati ya Utendaji ya Kata

(d) Kupitia na kupitisha programu za baraza

(e) Kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Baraza zilizowasilishwa na Kamati ya Utendaji na kutoa maelekezo.6.3.5 Mkutano Mkuu utakutana mara moja kwa mwaka

6.3.6 **WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI**

(a) Viongozi wote wa kata kama walivyobainishwa katika kifungu cha 6.3.1

(b) Wajumbe watatu wanaochaguliwa na Mkutano Mkuu.

(c) Makatibu wa matawi ndani ya kata

(d) Viongozi vijana wa chama na wa serikali watokanao na CHADEMA katika ngazi ya kata

6.3.7 Kamati ya Utendaji itakutana mara nne kwa mwaka. Mikutano maalum/ya dharura inaweza kuitishwa kutokana na mahitaji.

6.3.8 **KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI,**

(a) Kutekeleza maazimio ya Mkutano Mkuu wa baraza kata

(b) Kubunina kuandaa mikakati yakuwakwamua vijana kiuchumi kwa kubuni miradi

(c) Kusimamia uchaguzi ngazi ya tawi

d) Kusimamia shughuli za kila siku za baraza

(e) Kupanga na kufanya ziara kwenye matawi kuhamasisha harakati za vijana.

6.3.9 Kamati ya Utendaji itakutana mara nne kwa mwaka.

**6.4 Ngazi ya Wilaya/Jimbo**

Ngazi ya wilaya ina miundo ya aina mbili kutegemea na aina ya wilaya kwa msingi wa ama ni wilaya yenye jimbo moja au ni wilaya yenye zaidi ya jimbo moja.

## 6.4.1 WILAYA ZENYE JIMBO MOJA

### 6.4.1.1 VIONGOZI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mratibu wa uhamasishaji
(d) Mweka Hazina

### 6.4.1.2 VIKAO

Kutakuwa na vikao vya aina tatu
(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji
( c) Sekretarieti

### 6.4.1.3 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU

(a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji
(b) Viongozi wa serikali vijana wanao tokana na **CHADEMA** katika ngazi ya kata na jimbo

(c) Viongozi vijana kutoka kwenye chama ngazi ya jimbo
(d) Wajumbe wawili kutoka kila kata
(e) Wenyeviti na makatibu kutoka kila kata
(f) Mratibu wa Uhamasishaji na Mweka hazina kutoka kila Kata.

### 6.4.1.4 KAZI ZA MKUTANO MKUU

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kumchagua Katibu wa Jimbo
(c) Kumchagua Mratibu wa uhamasishaji wa Jimbo

(d) Kuchagua wajumbe watatu wa kuingia kwenye karnati tendaji.
(e) Kupitia na kupitisha mikakati ya baraza iliyopendekezwa na Kamati ya Utendaji
(f) Kutathmini utendaji kazi wa kamati ya utendaji na kutoa mwelekeo.

6 4.1.5 Mkutano Mkuu utakutana mara moja kwa mwaka

**6.4.1.6 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI**

(a) Viongozi wote wa jimbo kama walivyobainishwa katika kifungu cha 6.4.2.
(b) Wajumbe watatu wakuchaguliwa na Mkutano mkuu
(c) Makatibu wa vijana kata.
(d) Viongozi wa Serikali vijana ngazi ya Jimbo.
(
e) Viongozi wawili wa Mtandao wa Wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya Juu, Kati na Sekondari (CHASO) ngazi ya Mkoa wanaosoma kwenye Taasisi ya Elimu iliyo sehemu husika.

### 6.4.1.7 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI

(a) Kutathmini utendaji kazi wa sekretarieti ya jimbo
(b) Kupendekeza mikakati ya Baraza kwenye mkutano mkuu
(c) Kupanga na kufanya ziara kwenye kata ili kuhamasisha harakati za vijana.
(d) Kubuni na kupanga mikakati ya kuwakomboa vijana kiuchumi.
(e) Kutekeleza maazimio ya Mkutano mkuu.
(f) Kufuatilia, kuratibu na kusimamia shughuli za Vijana wa Mtandao wa Wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya Juu, Kati na Sekondari (CHASO) ndani ya Wilaya/ Jimbo.
(h) Kufuatilia, kuratibu na kusimamia shughuli za vijana wa mtandao wa wanafunzi wa CHADEMA wa elimu ya juu, kati na sekondari (CHASO) ndani ya wilaya/jimbo.

**6.4.1.8** Kamati ya Utendaji itakutana nne moja kwa mwaka. Mikutano maalum/ya dharura inaweza kuitishwa kutokana na mahitaji.

### 6.4.1.9 WAJUMBE WA SEKRETARIETI

(a) Katibu wa baraza
(b) Mratibu wa Uhamasishaji
(c) Mweka hazina
(d) Wajumbe wasiozidi wawili wanaoingia kutokana na utaalamu wao.
(e) Viongozi wa serikali vijana ngazi ya jimbo.

### 6.4.1.10 KAZI ZASEKRETARIETI

(a) Inahusika na utendaji wa shughuli za kila siku za baraza
(b) Kutekeleza maazimio ya kamati tendaji
(c) Kubuni na kupanga mikakati mbalimbali ya kuwasaidia vijana kiuchumi
(d) Kusimamia kwa karibu programu zote za siasa, uchumi na zile za kijamii zinazoendeshwa na baraza ndani ya jimbo

6.4.1.11 Sekretarieti ya jimbo itakutana kila mwezi mara moja. Mikutano maalum/ ya dharura inaweza kuitishwa kutokana na mahitaji.

## 6.4.2 WILAYA ZENYE ZAIDI YA JIMBO MOJA

6.4.2.1 Kwa wilaya zenye jimbo zaidi ya moja patakuwa na kamati ya uratibu.

6.4.2.2 Wajumbe wa kamati ya uratibu
(a) Mwenyekiti wa kamati
(b) Katibu wa kamati
(c) Wenyeviti kutoka kila jimbo
(d) Makatibu kutoka kila Jimbo
(e) Mratibu wa uhamasishaji kutoka kila Jimbo.
(f) Waweka Hazina kutoka kila Jimbo.

### 6.4.2.3 KAZI ZA KAMATI YA URATIBU

(a) Kuwa kiunganishi baina ya majimbo na wilaya
(b) Kutoa mchango wa kiushauri na kiutendaji kwa majimbo
(c) Kuratibu shughuli za jumla za baraza ndani ya wilaya
(d) Kutoa mwelekeo wa shughuli za baraza kiwilaya
(e) Kumchagua Mwenyekiti wa kamati ya uratibu
(f) Kupendekeza Katibu wa Kamati ya Uratibu kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

6.4.2.3 Kamati ya uratibu itakutana mara tatu kila baada ya miaka mitano.

## 6.5 NGAZI ZA MIKOA

Ngazi hii itakuwa na kamati ya Uratibu.

### 6.5.1 WAJUMBE WA KAMATI YA URATIBU

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Wenyeviti wa majimbo
(d) Makatibu wa Majimbo
(e) Wenyeviti wa Kamati za Uratibu za Wilaya
(f) Kwa mikoa ya Kichama ya Dar Es Salaam, Waratibu wa Uhamasishaji na Waweka Hazina wa Majimbo watakuwa wajumbe katika Kamati za Uratibu
(g) Mwenyekiti na Katibu wa mtandao wa wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya Juu, Kati na Sekondari (CHASO) ngazi ya Mkoa.

(h) Makatibu wa kamati za uratibu za wilaya
(i) Wawakilishi wasiozidi watano wa wabunge vijana
(j) Wawakilishi wasiozidi watano wa madiwani vijana
(k) Viongozi vijana wa chama taifa wanaoishi katika Mkoa husika
(l) Viongozi wa serikali vijana ngazi ya Taifa wanaotoka katika Mkoa husika.

### 6.5.2 KAZI ZA KAMATI YA URATIBU

(a) Kuwa kiunganishi cha Wilaya ndani ya Mkoa
(b) Kuwa Kiunganishi cha Mkoa na Taifa
(c) Kutoa Mchango wa kiushauri kuhusiana na utendaji wa Majimbo
(d) Kutoa mwelekeo wa shughuli za baraza kimkoa
(e) Kumchagua Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu
(f) Kumpendekeza Katibu wa Kamati ya Uratibu ya Mkoa kwa Kamati ya Uratibu ya Kanda.
(g) Kupendekeza Katibu wa Kamati ya Uratibu kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa.
(h) Kufuatilia, kuratibu na kusimamia shughuli za Mtandao wa wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya Juu, Kati na Sekondari (CHASO) ndani ya Mkoa.

6.5.3 Kamati ya Uratibu itakutana mara tatu ndani ya miaka mitano.

## 6.6 Kutakuwa na Ngazi ya Kanda ya Baraza kama Ifuatavyo:

### 6.6.1 VIONGOZI

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Mweka Hazina

### 6.6.2 VIKAO

Kutakuwa na Kikao kimoja tu cha Baraza katika ngazi ya Kanda

(a) Kamati ya Uratibu ya Kanda.

### 6.6.3WAJUMBE WA KAMATI YA URATIBU YA KANDA

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu
(c) Wenyeviti wa Kamati za Uratibu za Mikoa ndani ya Kanda
(d) Makatibu wa Kamati za Uratibu za Mikoa ndani ya Kanda
(e) Wajumbe wa Kamati Kuu Vijana wanaoishi ndani ya Kanda
(f) Viongozi Wakuu wa BAVICHA Taifa wanaoishi ndani ya Kanda
(g) Wabunge/Wawakilishi Vijana ndani ya Kanda
(h) Madiwani Vijana wasiozidi watatu(03) watakaochaguliwa na Baraza la Uongozi la Kanda la Vijana
(i) Mweka Hazina

### 6.6.4 KAZI ZA KAMATI YA URATIBU YA KANDA

Kamati ya Uratibu ya Kanda litakuwa na kazi zifuatazo;

(a) Kumchagua Mwenyekiti
(b) Kumchagua Katibu
(c) Kumchagua Mweka Hazina
(d) Kuthibitisha Makatibu wa Kamati za Uratibu za Mikoa.
(e) Kutathmini hali ya kisiasa ya Vijana ndani ya Kanda na Kutoa Ushauri kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa
(f) Kuwa kiunganishi kati ya Baraza na Chama ngazi ya Kanda
(g) Kutoa mwelekeo wa shughuli za Baraza kwenye Kanda

6.6.5 Baraza la Uongozi la Kanda litakutana mara mbili katika miaka mitano, Vikao vya dharura/ Maalum vinaweza kuitishwa kwa mahitaji maalum.

## 6.8 NGAZI YA TAIFA

### 6.8.1 VIONGOZI

(a) Mwenyekiti
(b) Makamu Mwenyekiti Bara
(c) Makamu Mwenyekiti Zanzibar
(d) Katibu Mkuu
(e) Naibu Katibu Mkuu Bara
(f) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar(g) Mratibu wa Uhamasishaji
(h) Mweka Hazina
(i) Viongozi wanaotajwa katika Kifungu cha 6.8.1(b), (c), (e), (f), (g) na (h) watakuwa wajumbe wa Baraza Kuu.

## 6.8.2 VIKAO

Kutakuwa na vikao vya aina tatu;

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati ya Utendaji
(c) Sekretarieti

## 6.8.3 Wajumbe wa Mkutano Mkuu

(a) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji (b) Wenyeviti wa Majimbo
(c) Wenyeviti wa Kamati za Uratibu za Wilaya
(d) Makatibu wa Mikoa
(e) Makatibu wa Kanda
(f) Wabunge/Wawakilishi Vijana
(g) Viongozi wa Chama Vijana ngazi ya Taifa
(h) Wawakilishi Madiwani Vijana watano watateuliwa na sekretariet na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji.

## 6.8.4 Kazi za Mkutano Mkuu

(a) Kumchagua Mwenyekiti Taifa
(b) Kumchagua Makamu Mwenyekiti Bara (c) Kumchagua Makamu Mwenyekiti Zanzibar
(d) Kuchagua wajumbe ishirini wa kuwakilisha vijana kwenye Mkutano Mkuu wa Chama Taifa. Kati yao, wajumbe kumi na tano watatoka Bara na watano watatoka visiwani.
(e) Kuchagua wajumbe watano wa kuwakilisha Vijana kwenye Baraza Kuu la Chama ambapo miongoni mwao wanne watatoka Bara na mmoja Visiwani.

(f) Kujadili taarifa ya Kamati ya Utendaji na kutoa mwelekeo.
(g) Kupitia na kuthibitisha programu za Baraza Kitaifa.
(h) Kujadili na kuthibitisha mapende-kezo ya mabadiliko ya Kanuni za Baraza ili kuwasilisha kwenye Baraza Kuu la Chama.
(i) Wawakilishi wa madiwani vijana watano watateuliwa na Sekretarieti na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji.

6.8.5 Mkutano Mkuu utakutana mara moja kwa miaka mitano na Mkutano Mkuu maalum unaweza kuitishwa wakati wowote ikibidi.

**6.8.6 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI TAIFA.**

(a) Wajumbe wote waliobainishwa kifungu cha 6.7.3 baada ya marekebisho.
(b) Wajumbe wote wa Sekretarieti
(c) Wenyeviti wa Mikoa
(d) Wenyeviti wa Kanda
(e) "Wajumbe watano wa Baraza Kuu wanaowakilisha Baraza.
(f) Wawakilishi wasiozidi watano wa Wabunge vijana watakaochaguliwa na Wabunge Vijana.
(g) Viongozi vijana wa Chama ngazi ya Taifa.
(h) Viongozi vijana wa Serikali ngazi ya Taifa.

Mwenyekiti na Katibu Mkuu waliomaliza muda wao mara baada ya Uongozi mpya kuchaguliwa watakuwa

wajumbe isipokuwa watakoma kuwa wajumbe mara baada ya kuwa na umri zaidi ya miaka 35.

**6.8.7 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI TAIFA.**

(a) Kumchagua Katibu Mkuu wa Baraza
(b) Kumchagua Naibu Katibu Mkuu Bara
(c) Kumchagua Naibu Katibu Mkuu Zanzibar
(d) Kusimamia chaguzi za Baraza kuanzia ngazi ya Mikoa hadi Kanda.
(e) Kumthibitisha Mratibu wa Uhamasishaji atakayependekezwa na Sekretarieti.
(f) Kuthibitisha watendaji watakaoteuliwa na Sekretarieti.
(g) Kuwa mamlaka ya nidhamu kwa viongozi wote ndani ya Baraza.
(h) Kupitia na kupitisha programu za Baraza ili zithibitishwe na Mkutano Mkuu
(i) Kupendekeza mabadiliko ya Mwongozo kwa Mkutano Mkuu.
(j) Kupanga taratibu za ada na bei za machapisho mbalimbali ya Baraza kama vile kadi.
(k) Kujadili taarifa za Sekretarieti na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji.
(l) Kuwa kiungo cha kudumisha mahusiano mema kati ya mabaraza na jumuiya za vijana za vyama vingine vya siasa nchini, Afrika na duniani.
(m) Kuandaa ajenda za Mkutano Mkuu
(n) Kuteua Tume ama Kamati kwa ajili ya kushughulikia masuala maalum ya Baraza kwa muda maalum.
(o) Kufanya uamuzi juu ya mapendekezo ya kufukuza mwanachama ndani ya Baraza.

(p) Kuchagua wawakilishi wasiozidi watano wa Madiwani Vijana.
(q) Kusimamia utendaji wa mtandao wa wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya juu na Sekondari.
(r) Kusimamia uhamasishaji wa vijana wa Chemchem.

6.8.8 Kamati ya Utendaji itakutana mara moja kwa mwaka

**6.8.9 WAJUMBE WA SEKRETARIETI.**

(a) Katibu Mkuu wa Vijana – Mwenyekiti wa Sekretarieti.
(b) Naibu Katibu Mkuu Bara
(c) Naibu Katibu Mkuu Zanzibar
(d) Mratibu wa uhamasishaji
(e) Mtunza Hazina
(f) Wajumbe watatu wa kuteuliwa na Sekretarieti na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji Taifa.

**6.8.10 KAZI ZA SEKRETARIETI.**

(a) Kuwa chombo cha utendaji wa shughuli za kila siku za Baraza
(b) Kuteua wataalam kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Baraza kwa kuzingatia mahitaji.
(c) Kuandaa Mikakati mbalimbali ya uendeshaji wa baraza na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Utendaji Taifa.
(d) Kuandaa programu mbalimbali

za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

(e) Kutoa mapendekezo ya uteuzi mbalimbali zinazofanywa na kamati tendaji.

(f) Kutekeleza maamuzi na maelekezo ya Kamati ya Utendaji na Uongozi.

(g) Kuandaa ajenda na nyaraka kwa ajili ya vikao vya Kamati ya Utendaji na uongozi na Mkutano Mkuu.

(h) Kumteua Mweka Hazina

(i) Kupendekeza Mratibu wa uhamasishaji kwa Kamati ya Utendaji

6.8.11 Sekretarieti itakutana mara moja kila mwezi na kila inapobidi.

## 6.9 AKIDI

(i) Kutahitajika akidi ya 50% ya Wajumbe wote halali katika kikao cha kila ngazi.

(ii) Kutahitajika asilimia 75 ya wajumbe wote halali kurekebisha au kubadilisha kanuni za Baraza au za uchaguzi.

# SURA YA SABA

## MAPATO NA MATUMIZI YA BARAZA

### 7.1 MAPATO

Mapato ya baraza yatatokana na ;

(a) Mauzo ya kadi za uanachama

(b) Ada za uanachama

(c) Michango hiari ya wanachama na wapenzi wa Baraza ndani na nje ya nchi

(d) Mapato yatokanayo na miradi ya Baraza

(e) Mapato yatokanayo na mchango wa chama kwa Baraza

### 7.2 MATUMIZI

Matumizi ya baraza ni kama yafuatayo

(a) Kuchapisha kadi za wanachama

(b) Uendeshaji wa shughuli za kila siku za Baraza

(c) Utekelezaji wa mikakati ya uendeshaji wa Baraza

(d) Uwekezaji katika miradi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

# SURA YA NANE

**MAMBO YA JUMLA KUHUSU MWONGOZO HUU**

(a) Kutakuwa na mtandao wa wanafunzi wa CHADEMA wa Elimu ya juu na Sekondari nchini kama itakavyoelekezwa na Baraza.

(b) Mwongozo huu ni sehemu ya Kanuni za Chama, hivyo endapo kipengele chochote cha mwongozo huu kitabainika kukinzana na Kanuni za Chama, basi Kanuni za Chama zitatamalaki

(c) Pia ieleweke kuwa Mwongozo huu utazingatia misingi ya Katiba ya Chama, na hivyo endapo kipengele chochote cha mwongozo huu kitakinzana na Katiba ya Chama, basi kipengele hicho kitakuwa batili na Katiba itatamalaki.